# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

### Kikao cha Saba – Tarehe 4 Septemba, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:

**MHE. LATIFA K. JUWAKALI K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano pamoja na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo

zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Reuben, kwa niaba yake Mheshimiwa John Sallu.

Na. 106

**Zahanati za Handeni Mjini Kuwa Vituo vya Afya**

**MHE. JOHN M. SALLU K.n.y MHE. REUBEN N. KWAGILWA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itazipandisha hadhi zahanati za Mkwajuni Chanika na Hedi Kwamagome kuwa Vituo vya Afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zahanati ya Hedi Kwamagome ina eneo la ekari 10 na inahudumia takribani wakazi 15,138. Zahanati hii ipo umbali wa kilometa 17 kutoka hospitali ya Halmashauri, hivyo inakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi kuwa kituo cha afya. Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na kuipandisha hadhi zahanati hiyo kuwa kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zahanati ya Mkwajuni Chanika ina eneo la ukubwa wa ekari Saba na ipo umbali wa kilometa mbili kutoka Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Handeni na hivyo haikidhi vigezo vya kuwa kituo cha afya. Aidha, zahanati hiyo itaendelea kuboreshwa kadri ya mahitaji ili iweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga kituo cha afya kwenye Kata ya Mabanda ambapo ni Kata ya kimkakati kiafya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ndani ya Handeni *DC* kuna Tarafa tatu hazina kabisa vituo vya afya. Je, ni lini Serikali itajenga vituo hivyo vya afya kwenye Tarafa ya Mkumburu, Magamba na Kwamsisi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Handeni Mjini Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, amefuatilia sana suala la Kituo cha Afya cha Kata ya Mabanda. Ninamhakikishia tu kwamba, kwa sababu alikwishawasilisha kwenye orodha ya vituo vya afya vya kimkakati, tayari imeshaingizwa kwenye orodha ya vituo vya afya vitakavyojengwa kila Jimbo na tutapeleka fedha kwenye Kata hii ya Mabanda kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Tarafa hizi tatu za Jimbo la Handeni Vijijini kwa Mheshimiwa Sallu, ni kweli hazina vituo vya afya, lakini tayari Serikali imeshaainisha kwenye Tarafa ya Kwamsisi zahanati ile itapandishwa hadhi na tayari ipo kwenye bajeti ya fedha za Benki ya Dunia, wakati wowote tunaamini kwamba fedha hizi zitapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Kata ya Mkumburu na Magamba, tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapeleka vituo vya afya, lakini Tarafa hii ya kumburu eneo la Segera na yenyewe imeingizwa kwenye mpango wa vituo vya afya kwa kila Jimbo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Kilango.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi. Ni takribani miaka miwili sasa tangu Mheshimiwa Waziri alipokuja Vunta kuona Zahanati ya Vunta na ukaahidi kwamba kunajengwa Kituo cha Afya pale Vunta lakini mpaka sasa hivi sijaona hatua yoyote iliyochukuliwa ya kuanza Kituo cha Afya cha Vunta. Je, Mheshimiwa Waziri, anaweza kuwaambia nini wananchi wa Kata ya Vunta?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mama Anne Kilango Malecela kwa namna ambavyo amefuatilia sana ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ile ya Vunta. Ni kweli mwaka 2022 mimi na yeye tuliongozana, tukafanya ziara na mikutano ya hadhara pale. Namhakikishia Mbunge kwamba, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapenzi yake makubwa kwa wananchi wa Same na Wananchi wa Vunta, tayari ameshatenga shilingi 623,000,000,

zitaingia wakati wowote kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Vunta. Kwa hiyo nawahakikishia wananchi wa Vunta kwamba kazi itaanza hivi karibuni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

Na. 107

**Ujenzi wa Barabara ya Sadala - Uswaa Hai**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Barabara ya Sadala - Uswaa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, barabara hiyo ilifanyiwa matengenezo ya sehemu korofi kwa gharama ya shilingi milioni 26.8 na mwaka 2024/2025, Shilingi milioni 35 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya maeneo korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini katika mwaka 2024/2025 imepanga kufanya usanifu wa kina kwa kilomita zote 9.87 za Barabara hii ya Sadala - Uswaa kwa lengo la kutambua gharama halisi zitakazotumika katika kuijenga. Hata hivyo, mara baada ya usanifu kukamilika na gharama halisi za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali kwa ujumla, kwa kweli wametuletea barabara nyingi za lami na kiwango cha changarawe, Mji wetu wa Bomang'ombe sasa hivi umezungukwa na lami na taa juu. Swali langu la kwanza; pamoja na kazi hii nzuri iliyofanyika, Barabara hii ya Kwa Sadala – Uswaa ni ahadi ya Hayati Rais Mtaafu Mheshimiwa Benjamin Mkapa, lakini Mheshimiwa Rais alivyotutembelea pia alituahidi na humu ndani nimeshaahidiwa zaidi ya mara tatu. Ninaomba sana Serikali ihakikishe hii barabara inajengwa kwa kiwango cha lami na taa juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ninaomba Barabara ya Kwa Sadala – Mula – Lemira – Uswaa kutokea Juweni, hii barabara ilijengwa kilometa 10 za lami, bado kilometa 25. Swali langu, ni lini sasa Serikali itajenga Barabara hii kuanzia pale Tema – Lemira kutokea Juweni njiapanda ya Sanya Juu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli amekuwa akisemea sana wananchi wake, akitaka kuona kwamba wanajengewa barabara nzuri.

Naomba sasa nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi kwamba Barabara hii ya Kwasadala – Uswaa yenye jumla ya kilometa 9.87 ipo katika usanifu. Usanifu ukikamilika na usanifu unafanyika kwa kilometa zote 9.87, lakini katika mwaka wa fedha ulioisha, ilitengwa jumla ya shilingi milioni 26.8 kwa ajili ya matengenezo katika maeneo korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka huu wa Fedha 2024/2025, barabara hii imetengewa jumla ya shilingi 35,000,000 kwa ajili ya matengenezo katika maeneo korofi. Ninaomba nimhakikishie, mara baada ya usanifu kukamilika, barabara hii itaingizwa katika mipango ili katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 iweze kujengwa kwa hadhi ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, barabara hii anayoizungumza Mheshimiwa Mbunge ya Juweni – Lemira, barabara hii ni ya jumla ya kilometa 35.06 ambayo ina kipande cha kilometa 10 ambacho ni cha lami. Kwa hiyo kilometa 25.06 ndiyo ambazo ni za changarawe. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inatafuta fedha ili ihakikishe kwamba kile kipande cha changarawe ambacho hakina lami, kinaweza kujengwa kwa lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka huu wa Fedha 2024/2025, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya barabara hiyo shilingi milioni 374.5 kwa ajili ya kurekebisha maeneo korofi na kujenga kivuko cha maji pamoja na kuiwekea changarawe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, Serikali ipo kazini, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba wananchi wanapata barabara zilizo bora.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itajenga Barabara ya Kata ya Kilakala ambayo ni reli kwa reli ambayo inakwenda kutokea Kata nyingine ya Vituka? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli amekuwa akisemea sana wananchi katika Jimbo lake ili waweze kujengewa

barabara zilizo imara na bora. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali tayari imekuwa ikitenga fedha kila mwaka wa bajeti kuhakikisha kwamba inaendeleza ujenzi na ukarabati wa barabara zetu hizi za *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mbunge, Serikali itaendelea na utaratibu huo kuleta fedha ili hii barabara uliyoitaja ya kutoka kwenye Kata hii ya Kilakala kwenda Vituka na yenyewe iweze kujengwa iwe kwenye hadhi nzuri, wananchi waweze kuitumia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Michael Mwakamo.

Na. 108

**Barabara ya Kuunganisha Kongani ya Viwanda Kwala na Stesheni ya *SGR* Ruvu**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya kuunganisha Kongani ya Viwanda ya Kwala na Stesheni ya *SGR* ya Ruvu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini imepanga kufanya usanifu wa kina wa barabara hii katika mwaka 2024/2025 kwa lengo la kutambua gharama halisi za mradi huu na ujenzi wake utategemea na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; sasa, kwa kuwa Serikali iko kwenye mkakati wa kufanya uchambuzi wa kujua gharama, je, imefanya mawasiliano na mkandarasi wa ujenzi wa eneo hilo ili wasifunge barabara ili wananchi waweze kuendelea kulitumia?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wakati wa ujenzi wa Reli ya *SGR*, limejengwa daraja pale kwenye Mto Ruvu ambalo limepitisha reli tu na hapakuzingatiwa eneo la kupita watu waendao kwa miguu na kwa magari. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja sasa la matumizi ya waendao kwa miguu na magari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mazuri kabisa haya kwa lengo la kuwasemea wapiga kura wake. Kuhusiana na swali lake la kwanza, ninaomba niendelee kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendelee kuwafahamisha na wananchi kwamba kufungwa kwa barabara hii ambayo ipo kando ya reli yaani kwa maana ya *SGR* ni takwa la kisheria. Ni takwa la kisheria kwa tafsiri ya kuimarisha usalama wa wananchi, watumiaji wa reli lakini pia kulinda ile miundombinu ya reli. Kwa hiyo naomba tuendelee kuwaelimisha wananchi ili waweze kufahamu kwamba hili ni suala ambalo linahusu usalama wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, naomba niendelee kumueleza Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua hoja uliyoisema na ni ya msingi. Kwa wakati huu Serikali

itafanya jitihada kuhakikisha inaimarisha miundombinu katika eneo hili la Ruvu ambalo mwisho wa siku litakuja kufanyiwa ujenzi kwa maana ya tafsiri tayari *SGR* inapita katika eneo hili. Tutaimarisha na tutatengeneza mazingira mazuri ili kuweza kutengeneza njia ya wananchi kupita, lakini pia magari kupita na kutengeneza suluhisho la kudumu. Kwa hiyo, hoja yako Mheshimiwa Mbunge tumeipokea na tunaifanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Subira Mgalu.

Na. 109

**Ujenzi wa barabara ya Mingoi-Kiembeni Kata ya Mapinga**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Mingoi - Kiembeni Kata ya Mapinga iliyoharibiwa na Mvua za *El-nino*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Serikali kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini ilijenga mfereji wa mita 500 kwa gharama ya shilingi milioni 62 kwa eneo lililoharibiwa na mvua. Katika bajeti ya mwaka 2024/2025, itajengwa mifereji mita 400 kwa gharama ya shilingi milioni 44.62 ili barabara hii iweze kupitika wakati wote wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, serikali imeweka kwenye mpango wa *Climate*

*Response Window (CRW)* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kujenga miudombinu ya kutolea maji katika Barabara ya Mingoi – Kiembei.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini itaendelea kuhudumia na kuboresha miundombinu ya barabara za Wilaya ya Bagamoyo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutujibu vizuri na naishukuru Serikali kwa kutupa matumaini kupitia majibu ya swali hili. Maswali yangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa, barabara hii ya Mingoi – Kiembeni ya kilometa sita inatumika na wakazi wengi takribani 17,000 wa mitaa kwa mfano Kiharaka, Kiembeni yenyewe, Mingoi, Tungutungu na kadhalika; na kwa kuwa wananchi wa maeneo haya wameunda mpaka Kamati ya Barabara chini ya uongozi wa Ndugu Mapunda ambayo imekuwa ikijichangisha mara kwa mara kutengeneza barabara hii. Sasa, ninamuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, je, yupo tayari kutembelea maeneo haya ili aone athari za mvua hizo za *El-Nino* na aone kama kiwango hiki kilichotengwa kwenye bajeti hii kama kitatosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa barabara hii linajengwa daraja kubwa la Mpiji Chini, chini ya *TANROADS* na Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Bashungwa alitembelea pale na kutoa ahadi kwamba kuna uwezekano wa kuipandisha hadhi barabara hii kwa kuwa ni kiungo kati ya Bagamoyo na Kinondoni.  Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yupo tayari kuisimamia *TARURA* ili ikamilishe mchakato wa vigezo ili barabara hii iende

*TANROADS* na ile ahadi ya kujengwa kwa kiwango cha lami iweze kutimia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, hakika Mheshimiwa Mbunge amekuwa akisemea sana Barabara hii ya Mingoi – Kiembeni na hasa kwa sababu ina wakazi wengi, kwa maana wakazi zaidi ya 17,000. Wengi ni wanawake na watoto wapo humo kwa hiyo amekuwa akisemea sana barabara hii ili kulinda maslahi ya makundi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza kama nipo tayari kuambatana na yeye kwenda kujionea hali halisi katika eneo hili ili kuona kama bajeti inatosheleza kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mara baada ya kutoka katika kujibu maswali haya, tutakaa, tutazungumza na tutapanga ratiba ili niweze kufika. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hata kwenye swali lake la pili, nikija kwenye ziara hiyo, nina imani hata suala hili la kuharakisha mchakato wa kuitoa barabara hii ya eneo la Mpiji Chini kwenye daraja hili linalojengwa na *TANROADS* kupandisha hadhi barabara hizi ili ziweze kutoka *TARURA* zihamie *TANROADS*, ninaamini tunaweza kulisimamia nikiwa nimefika kwenye eneo husika. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie kwamba nipo tayari na tutafanya kazi bega kwa bega kwa maslahi mapana ya watu wa Bagamoyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Wakati wa mvua za *El-Nino* barabara nyingi sana katka Jimbo la Ngara

ziliharibika, ikiwemo Barabara ya Kibirizi kwenda Keza ambapo daraja liliondolewa kabisa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kwenda kujenga barabara hizi ili kurudisha miundombinu iliyoharibika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumza kuhusiana na Barabara hii katika eneo hili la Kibirizi – Keza na hasa kwa sababu mawasiliano hapa yamekatika. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kipaumbele namba moja katika kuhudumia miundombinu hii ya barabara ni kuunganisha mawasiliano. Maeneo yote ambayo mawasiliano yamekatika yanapewa kipaumbele namba moja katika kuhakikisha kwamba Serikali inarudisha mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya mawasiliano na Meneja wa *TARURA,* ananisikia kwa wakati huu, ili kuona ni namna gani tunaharakisha kurudisha mawasiliano katika eneo hili ambalo amelitaja Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, unajibu vizuri na kwa ufasaha. Naomba tu iwe kwa kifupi. Mheshimiwa Butondo, jiandae Mheshimiwa Kigua.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mwaka wa 2024 ulikuwa ni mwaka wa mvua nyingi za *El-Nino* na bahati mbaya sana zimeathiri barabara nyingi na madaraja mengi yamevunjika; zaidi ya kilomita 50 zimeathirika katika Wilaya ya Kishapu na Serikali imefanya tathmini na kugundua kwamba zaidi ya bilioni 2.7 zinahitajika kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizo. Je, ni lini Serikali itatekeleza uletaji wa fedha wa

haraka na wa dharura ilimradi urudishaji wa miundombinu hiyo uweze kufanyika haraka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba mvua zilizonyesha, mvua za *El-Nino,* zimefanya uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara zetu na hasa hizi barabara za wilaya zinazosimamiwa na *TARURA*. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka wa bajeti ili kuhakikisha kwamba inafanya matengenezo ya barabara hizi ambazo zimeharibika. Nimhakikishie kwamba katika jimbo lake pia Serikali itaendelea kupeleka fedha kuhakikisha tunaziweka hizi barabara katika hadhi nzuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwenye eneo langu katika Jimbo la Kilindi kuna Kata inaitwa Kata ya Kilwa barabara inayoanzia Kata ya Kwediboma – Kilwa hadi Kwadundwa mvua za *El-Nino* za mwaka jana zimeharibu miundombinu na kata hiyo sasa hivi haifiki kabisa. Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kuhakikisha kwamba na eneo hilo linapitika kwa sababu lina uzalishaji mkubwa wa bidhaa nyingi sana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa barabara zetu hizi za *TARURA* hasa kiuchumi lakini pia kijamii; na inatambua kuwa mvua

zilizonyesha za *El-Nino* zimefanya uharibifu mkubwa. Kwa hiyo, Serikali imekua ikitenga fedha kila mwaka wa bajeti kuhakikisha kwamba inafanya matengenezo na inajenga barabara mpya hizi za *TARURA*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kupeleka fedha katika Jimbo lake kwa ajili ya kuhudumia barabara zake ikiwemo hii aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya kutoka Kigorogoro Kata ya Kibale kwenda Kishanda na pia kwenda Rulama katika Wilaya ya Kyerwa imeharibika sana. Je, ni ni lini hizi barabara zitatengenezwa kwa sababu hazifai kabisa? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatenga fedha kila mwaka wa bajeti; na sote ni mashahidi tunaona Bajeti ya *TARURA* imeongezeka kwa kiwango kikubwa kutoka bilioni 275 mpaka bilioni 710 kwa mwaka. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inaifikia barabara hii na kuijenga ili iwe katika hadhi nzuri na wananchi waweze kupata huduma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Makete ni moja kati ya majimbo ambayo yana changamoto ya mvua za muda mrefu; barabara nyingi ni za *TARURA* na sisi ndio tunaoongoza kwa uzalishaji wa vyakula ambavyo vinatumika mijini. Je. Serikali ina mkakati gani wa kurudisha miundombinu ya Barabara

iliyoharibika kwenye Jimbo la Makete hususan maeneo ya Matamba – Kikondo na maeneo ya Lupila? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amekuwa akisemea sana barabara hizi alizozitaja hasa katika maeneo hayo ya Lupila na maeneo ya Matamba. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka wa bajeti kwa ajili ya kuhudumia barabara zikiwemo barabara katika jimbo lake. Hata katika mwaka huu wa bajeti 2024/2025, Serikali imetenga fedha na itafikia barabara katika jimbo lake ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata barabara zilizo bora kwa ajili ya shughuli za uchumi na za kijamii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Baada ya mvua kubwa za *El-Nino* kuharibu barabara nyingi za Mjini Liwale; kwanza tunashukuru tuliletewa fedha kipindi kile, lakini ipo haja kwa Serikali kutuletea fedha kufungua Barabara za Mpigamiti – Liwale, Kikuyungu - Liwale, barabara ambazo bado mpaka sasa hivi hazipitiki kirahisi. Je, ni lini Serikali itatupatia fedha kwa ajili ya barabara hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara hizi za *TARURA* zinakuwa katika mazingira ya kupitika mwaka mzima. Tunafahamu kwamba mvua kubwa za *El-Nino* zimeleta uharibifu mkubwa wa

miundombinu ya barabara hizi. Kila mwaka wa bajeti Serikali inatenga fedha kuhakikisha kwamba inafanya ukarabati pamoja na kufanya ujenzi katika barabara hizi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hata Mwaka huu wa Bajeti wa 2024/2025, Serikali italeta fedha kwa ajili ya kuhakikisha inahudumia barabara katika jimbo lake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Profesa.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Barabara ya *International School* Kibosho - *KNCU* hadi Kwa Raphael ujenzi wake unakwenda taratibu sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha barabara hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilichukue swali hili. Nitafanya mawasiliano na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ili kufahamu changamoto iliyopo ambayo inapunguza kasi ya utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii inayotoka *International School* kwenda Kwa Raphael. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante. Unaongea sana kwa majibu sahihi. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunakwenda Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Hassan Kungu.

Na. 110

**Kutofanya Kazi Kiwanda cha Kubangua Korosho – Tunduru**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, kwa nini Kiwanda cha Kubangua Korosho Wilayani Tunduru kimeshindwa kufanya kazi kwa miaka saba mfululizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Kubangua Korosho cha Tunduru kilijengwa na Serikali mwaka 1981. Kutokana na mabadiliko ya kisera, Serikali ilibinafsisha kiwanda hicho kwa Kampuni ya Korosho *Africa Limited* mwaka 2001. Kiwanda hicho chenye uwezo wa kubangua wastani wa tani 3,500 kiliendelea na shughuli za ubanguaji hadi msimu wa 2019/2020 kiliposimamisha ubanguaji kutokana na kiwanda kubangua korosho kwa hasara tofauti na matarajio ya mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina imeanza kupitia upya hali ya uzalishaji wa viwanda vya korosho vilivyobinafsishwa kikiwemo kiwanda cha Tunduru ili kujadiliana na kuhakikisha kwamba wawekezaji waliopo wanavifufua viwanda hivyo kwa malengo yaliyokusudiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kungu.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; moja ya sababu ya kubinafsishwa viwanda vile ama kiwanda kile ni kumpata Mwekezaji mwenye uwezo wa kukiendeleza kiwanda kile. Je, Serikali haioni kuwa mwekezaji yule amekosa sifa zilizomfanya kubinafsishiwa kiwanda kile na kushindwa kukiendeleza kiwanda hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kiwanda kile kilikuwa kinatoa ajira kwa akina mama ama wanawake zaidi ya 600 na vijana zaidi ya 200. Je, ni kwa nini Serikali isimlazimishe Mwekezaji kukirejesha kiwanda kile Serikalini ili kumtafuta Mwekezaji mwingine mwenye uwezo mkubwa wa kukiendeleza na hatimaye akinamama wale waendelee kupata ajira za muda mfupi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zidadu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mimi mwenyewe nimetembelea kiwanda kile na nimefika kukiona na *infrastructure* iliyoko pale nimeiona kwa macho yangu. Ndiyo maana kwenye jibu la msingi tumesema kwamba tunaanza majadiliano na wenzetu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ambao walikasimiwa madaraka yaliyokuwa yanatekelezwa na *PSRC* ili tuweze kuona masharti ya ubinafsishaji ya viwanda vile yalikuwa namna gani. Tatizo hili la watu waliobinafsishiwa viwanda ambao *at the same time* ni *exporter* wa *raw material,* wengi walichukua viwanda vya korosho na wakavifunga, halafu wakawa ni wasafirishaji wa korosho ghafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote, tatizo hili tunalo kwenye korosho na kwenye chai. Watu wamechukua mashamba, wamechukua viwanda hawajamua kuendeleza toka walivyobinafsishiwa. Serikali tumeanza mchakato wa kuanza kuipitia mikataba ya ubinafsishaji na kuangalia kama wanakidhi masharti waliyopewa na Serikali wakati wanauziwa viwanda hivi na Serikali itachukua hatua.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Kama ilivyo katika kiwanda cha korosho ninajua katika jibu la msingi amezungumzia chai; Kiwanda cha Chai MO kilichopo Rungwe kimefunga na kuwaacha wafanyakazi ambao wengi hawajalipwa na chai inakaa hainunuliwi. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, atoe tamko leo tunafanyaje kwa sababu chai ni zao ambalo linaharibika sasa wanaanza kung'oa mazao ya chai na kupanda parachichi. Tunaomba msaada wa Waziri ili tuweze kujua.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema wakati najibu swali la Mheshimiwa Zidadu, changamoto ya aina hii tunayo kwenye korosho, changamoto ya aina hii tunayo kwenye chai. Kwenye chai kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba mwekezaji huyu amenunua mashamba na viwanda Rungwe na baadhi ya maeneo katika nchi yetu na vyote amevifunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nimhakikishie kwamba Wizara ya Kilimo tayari ilishamwandikia barua na ametujibu, lakini hatujakubaliana na majibu aliyotupatia. Wizara na Serikali

tunaendelea kufuatilia kuhakikisha yeyote aliyeuziwa shamba, aliyeuziwa kiwanda ambacho hakiendelezi atupe sababu za kutotimiza wajibu wake wa kimkataba wakati anabinafsishiwa maeneo haya na Serikali itachukua hatua. Ni jambo litakalotuchukua muda, lakini niwahakikishie tu kwamba tumeanza ku-*pursue* huu mwelekeo na tutafika nao mwisho. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Felix Kavejuru.

Na. 111

**Mkakati wa Kuvutia Wawekezaji wa Viwanda vya Kuchakata Zao la Migomba Nchini**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuvutia wawekezaji wa viwanda vya kuchakata zao la migomba nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru Felix, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuendeleza zao la migomba ikiwemo utafiti na uzalishaji wa miche bora, kuhamasisha uzalishaji wa ndizi kibiashara, kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vya kuongeza thamani na ujenzi wa vituo vya kuuzia na masoko ya kimkakati katika maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuvutia uwekezaji katika uchakataji wa mazao ya migomba, Serikali inaendelea kutoa elimu na kuhamasisha kuanzisha ushirika wa wakulima wa ndizi ili waweze kupata huduma mbalimbali kwa urahisi ikiwemo miundombinu ya kuongeza thamani na kupunguza kodi ya vifaa vya kuivishia ndizi *(banana ripening chambers)*. Pia ili kuhakikisha viwanda vitakavyoanzishwa vinapata malighafi Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti *(TARI)* pamoja na Sekta Binafsi inaanza ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche ya migomba kwa njia ya chupa *(tissue culture)* katika Kituo cha Maruku – Kagera. Hatua hiyo itawezesha Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* kuendelea kutafuta wawekezaji wa kimkakati ndani na nje ya nchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Kigoma ni wakulima wazuri wa migomba. Je, ni lini Serikali itajenga maabara ya uzalishaji wa miche bora ya migomba ili kuongeza uzalishaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; moja ya changamoto ya zao la ndizi ni ukosefu wa soko la uhakika kwa ndizi. Je, Serikali ina kauli gani juu ya uhakika wa soko la ndizi kwa wakulima wa ndizi Mkoani Kigoma? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Felix, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuweka maabara ya *tissue culture* ningemwomba Mheshimiwa Mbunge asubiri kwanza tumalize ujenzi wa *Tissue Culture Lab* iliyoko Maruku na nimhakikishie

tu kwamba ombi lake hili tutalichukua, tutaweza kuongeza *extension* kwenye mwaka ujao wa fedha pale Kihiga ili tuweze kujenga kituo kingine katika Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la soko. Nataka tu nitumie nafasi hii kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, changamoto yetu ya ndizi kwa ajili ya biashara ya *export* kwanza ni *variety* ambazo tumekuwa tukitumia. Kwa muda mrefu kama nchi tulikuwa hatujalipa thamani inayostahili zao la ndizi na kulijengea mazingira yanayotakiwa. Nataka tu nimwambie kwamba, Serikali imeshamaliza kufanya mambo mawili. Moja kufanya *mapping* ya kuangalia ugonjwa wa *banana virus* ulioko Mkoa wa Kigoma ambao sasa hivi Serikali imeanza kuufanyia kazi, na la pili tumeanza *mapping* na kuchakata *variety* ambazo zinafaa kwa ajili ya *export*. Buhigwe na maeneo mengine ya Mkoa wa Kigoma yako katika *mapping* ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ndani ya miaka miwili, mitatu, wakulima wa mazao ya ndizi, kwa maana ya Kigoma, Mbeya, Kilimanjaro, Arusha na maeneo mengine wataona mabadiliko makubwa sana katika zao hili. Kwa sababu tumeamua kama Serikali kulifanya moja ya zao la *export* na tunashirikiana na Taasisi ya *TAHA* na taasisi zingine kwa ajili ya kufanya kitu cha namna hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Malleko.

Na. 112

**Uhitaji wa Hatimiliki Kwenye Vituo, Taasisi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa kupata hatimiliki maeneo yanayomilikiwa na vituo vya wazee, watoto na taasisi za ustawi na maendeleo ya jamii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMIII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inayo mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kwamba vituo vya huduma za ustawi wa jamii na shughuli za maendeleo ya jamii vinapata hatimiliki za ardhi. Moja kati ya mikakati hiyo ni kutenga bajeti, ambapo katika Mwaka huu wa Fedha 2024/2025, Wizara imetenga shilingi milioni 75.7 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya vituo 29 vya Wizara, vituo 15 vimefanikiwa kupatiwa hati miliki na maeneo mengine 14 yapo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa upatikanaji wa hati hizo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni upi mkakati maalum wa Wizara wa kuhakikisha maeneo ambayo bado hayajapata hati miliki

yanaweza kupimwa na kupatiwa hati miliki ili kupunguza uvamizi kwenye maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa maeneo mengi bado hayajaendelezwa, je, ni upi sasa mpango jumuishi wa Wizara kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanatumika vyema kwa ajili ya jumuiya zinazozunguka maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Malleko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, Serikali imetenga shilingi milioni 75.7 kwa ajili ya ukamilishaji wa hatimiliki hizo ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, Serikali ina mpango jumuishi wa kuhakikisha maeneo yote ambayo yanazunguka jamii kuna vituo vya afya, vituo vya kulelea watoto, mashamba darasa na viwanja vya kuchezea michezo ili kudhibiti viwanja hivyo visivamiwe. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa changamoto ya ukosefu wa hati miliki na uzio katika maeneo haya ya wazee imekumba Makazi ya Wazee Nunge, Vijibweni, Kigamboni, hali ambayo imeleta mgogoro mkubwa baina ya wananchi wa maeneo yale. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko

tayari kufuatana na mimi kwenda kuona changamoto iliyopo katika Makazi ya Wazee ya Nunge, Kigamboni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMIII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kisangi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nipo tayari kufuatana na Mheshimiwa Mbunge nitakapomaliza Bunge hili kuona utaratibu mzuri wa Nunge ili tuweze kuukamilisha vizuri kwa kutenga fedha kwa ajili ya wananchi wetu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Toufiq Turky, kwa niaba yake Mheshimiwa Mtanda.

Na. 113

**Kongamano la Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Wafugaji Nyuki *(APIMONDIA)***

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y MHE. TOUFIQ SALIM TURKY** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha Watanzania wanashiriki Kongamano la Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Wafugaji mwaka 2027?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa Kongamano la Kimataifa la Wafugaji Nyuki Duniani *(Apimondia)* litakalofanyika mwaka 2027. Serikali imejipanga kwa njia mbalimbali kuhakikisha Watanzania wanashiriki kikamilifu pamoja na kunufaika na Kongamano hilo ikiwa ni pamoja na kuunda Kamati ya Maandalizi ya Kitaifa ambayo inajumuisha wajumbe kutoka Serikalini na sekta binafsi kwa lengo la kuratibu na kufanya maandalizi ya kutosha ili kufanikisha kongamano hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine inajumuisha uhamasishaji wa wananchi katika ufugaji, uzingatiaji ubora na kufungua masoko mapya ya mazao ya nyuki duniani. Serikali pia kwa kushirikiana na sekta binafsi imekuwa ikiandaa maonesho kama hamasa ya maandalizi. Miongoni mwa maonesho yaliyofanyika ni pamoja na siku ya nyuki duniani iliyofanyika tarehe 17 - 20 Mei, 2024 na Maonesho ya Kitaifa ya Asali Tanzania yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 19 hadi 22 Juni, 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza Serikali kwa majibu mazuri ambayo wameyatoa lakini nataka kufahamu tu kwamba, yapo maeneo mengi katika nchi yetu ambayo yanafaa sana kwa ufugaji wa nyuki. Ninashukuru wamesema wanaanza mikakati ya kuelimisha Watanzania, lakini naomba niulize; swali la kwanza; ni upi sasa mkakati ambao Serikali imejiwekea ili wale wananchi ambao wanaishi kule vijijini wapate kwa uhakika elimu hii ili ilete manufaa kwa wafugaji wa nyuki wanaoishi vijijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuongozana nami kwenda katika Jimbo la Newala Vijijini ili

aone namna ambavyo mazingira yetu ni mazuri kwa ufugaji wa nyuki na kuleta hamasa kwa wananchi wa Newala Vijijini? Nakushukuru *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tumekuwa na mipango mbalimbali ya kutoa elimu kwa wananchi na kama mnavyofahamu kwenye kila Halmashauri tunao Maafisa Nyuki. Kwa hiyo, tumekuwa tukiwajengea uwezo ili waweze kutoa elimu hiyo. Vilevile, kupitia makongamano ambayo tumekuwa tukiyaandaa tumekuwa tukitoa elimu kwa wananchi na pale ambapo kuna vikundi ambavyo vinahitaji kupatiwa elimu, tumeweza kuwasaidia Maafisa Nyuki waliopo kwenye Halmashauri zetu kuweza kutoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa wito kwa wananchi kujiingiza kwa nguvu kubwa katika ufugaji wa nyuki, kwa sababu biashara ya asali na bidhaa zinazoambatana nazo ni kubwa na hivi karibuni Serikali imefanya jambo kubwa. Tumeweza kupata soko kubwa kule Nchini China ambalo kwa mwaka wanahitaji tani 38,000,000. Kwa hiyo, hii ni fursa kwetu sasa kuweza kuchangamkia soko hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la pili, nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda Newala kuona jinsi ambavyo tunaweza kushirikiana, kuhamasisha ufugaji wa nyuki na biashara hii katika eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maji, Mheshimiwa Massare.

Na. 114

**Uchimbaji wa Visima vya Maji-Manyoni Magharibi**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:

Je, lini Serikali itachimba visima vya maji kwenye Vijiji vya Kayui, Kalangali, Makale na Mwamagembe – Manyoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na zoezi la utafiti wa maji ardhini pamoja na uchimbaji wa visima virefu katika Wilaya zote za Mkoa wa Singida ikiwemo Wilaya ya Manyoni, kupitia programu mbalimbali ikiwemo programu maalum ya uchimbaji wa visima 900.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wilaya ya Manyoni, Serikali imekamilisha uchimbaji wa visima katika vijiji vinne vya Makale, Jeje, Idodyandole na Mtakuja ambapo kazi ya upimaji wingi wa maji *(pumping test)* katika visima hivyo inaendelea. Aidha, kazi ya uchimbaji wa visima katika maeneo mengine ya Wilaya hiyo ikiwemo vijiji vya Kayui, Kalangali na Mwamagembe unaendelea ambapo unatarajia kukamilika Oktoba, 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali lakini nina maswali madogo mawili. Swali la kwanza; uchimbaji wa visima katika Halmashauri yangu ya Itigi katika Wilaya ya Manyoni, maeneo ya Kayui na Mtakuja wamechimba, lakini maji hamna kabisa. Je,

Serikali iko tayari sasa kuajiri wataalam wazuri wa *surveyors* ambao kabla ya uchimbaji waweze kutuainishia kabisa kwamba hapa tukichimba tutapata maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali ipo tayari sasa kwenda kuchimba kisima katika eneo la Kalangali ambapo kuna shida kubwa na tunajenga sasa hivi Sekondari ya Ufundi ya Amali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Massare kwa kazi kubwa anayoifanya na ufuatiliaji wa miradi ndani ya Jimbo lake. Kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi, baada ya kuchimba visima tunaanza kupima wingi wa maji kwa maana ya *pumping test* na baada ya kujiridhisha maji hayo hayatokuwa yanatosha, basi tutaangalia eneo lingine. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Wizara ya Maji inao wataalam na vifaa vya kutosha kuhakikisha kwamba kazi hii tunaifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande swali la pili kuhusu Kalangali, ninatumia fursa hii kumwelekeza *RM* Mkoa wa Singida, ahakikishe anaangalia kipaumbele cha Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba, akaanze na eneo hili ili liweze kuhakikisha kwamba lina upatikanaji wa maji ambapo itaweza kusaidia katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, uchimbaji wa kisima kwenye Kata ya Mwika Kusini ulikumbwa

na matatizo na maji hayakupatikana kwenye kina kinachokubalika. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kufikisha maji kwenye eneo la Kata hii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Dkt. Kimei kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata maji na hasa wananchi wa Mwika ambapo Serikali ikiona eneo fulani halina maji, inaangalia chanzo kingine ambacho kinaweza kusaidia kufikisha maji katika eneo lingine. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali tutalifanyia kazi, ili kubainisha chanzo kingine ambacho kitakuwa na wingi wa maji ambao utaweza kusaidia katika Kata ya Mwika. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Issa Mchungahela.

Na.115

**Kutoanza kwa Mradi wa Maji Mbangara**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

Je, nini kimesababisha Mradi wa Maji Mbangara –Lulindi kutoanza licha ya kutengewa fedha kwa misimu mitatu mfululizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha usanifu wa kina wa Mradi wa Maji Kijiji cha Mbagara kilichopo Jimbo la Lulindi, Wilayani Masasi. Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa nyumba ya kuendeshea mitambo *(pump house),* ujenzi wa matanki sita yenye jumla ya ujazo wa lita 800,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 165, ujenzi wa vituo 24 na vioski 51 vya kuchotea maji. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za muda mfupi, Serikali imekarabati pamoja na kufanya upanuzi wa Skimu za Maji za Lupaso na Lulindi na hivyo kuboresha huduma ya maji safi na salama katika vijiji 38 vya Jimbo la Lulindi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu, lakini hali halisi ni kwamba, wananchi wangu wa Jimbo la Lulindi wapo katika adha kubwa ya maji. Swali la kwanza; sasa, Naibu Waziri anasema nini kuhusiana na hali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; upo tayari kuongozana na mimi kwenda kujionea hali halisi ilivyo kule kwa sababu hayo majibu pamoja na kwamba ni majibu sahihi, hayakidhi hali ya changamoto waliyonayo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungahela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri kwanza kabisa tumekuwa na mjadala mrefu na Mheshimiwa Mchungahela kuhusu mradi huu. Kwa kweli kati ya watu ambao wanaufuatilia kwa karibu sana, Mchungahela amekuwa kinara katika kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Serikali ni kwamba, kwanza kabisa natumia fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Mheshimiwa Waziri ameandika *special request* ya mradi huu Wizara ya Fedha ili uweze kutangazwa na kuhakikisha kwamba mradi huu unaenda kuanza mara moja kwa ajili ya wananchi wa Lilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge mradi huu sisi kama Serikali tunafahamu kwamba, tunaendelea kuunga mkono kampeni ya Mheshimiwa Rais ya Kumtua Mama Ndoo Kichwani na tunafahamu kwamba, ahadi ni deni na Serikali itatimiza ahadi hiyo. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi Mheshimiwa Mbunge tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni majukumu yetu Serikali kuhakikisha kwamba, tunaitikia wito wa Waheshimiwa Wawakilishi wa Wananchi pale ambapo wanatuomba. Mheshimiwa Mchungahela nipo tayari kuongozana na wewe kwenda kujionea hali halisi ya upatikanaji wa maji ndani ya Jimbo la Lulindi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ziara yake aliyoifanya Wilayani Nyang'hwale na kuacha maagizo pale Kata ya Nyijundu kwamba, kufikia tarahe 19 maji yawe yanatiririka na tayari maji yanatirirka Kata ya Nyijundu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo

tayari kuzisukuma zile milioni 286 kwa ajili ya kukamilisha usambazaji wa maji kwenye Kijiji cha Iseni, Kabiga, Nyangaramila, Nyamikonze, Kasubuya, Kaboha, Shibuha na Shibumba? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge wa Nyang'hwale ameuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kuna hizo pesa ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziongelea na kwa kweli nampongeza sana kwa sababu tuliweza kuzunguka katika Jimbo lake karibu Kata kwa Kata tulijionea hali halisi. Kweli mradi huu ambao ameutaja unahitaji hizi fedha ili uweze kukamilika kwa haraka. Ninakuahidi kwamba Mheshimiwa Mbunge tutasukuma hizo fedha zitoke haraka ili mradi uweze kukamilika kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mradi wa Maji unaogusa Kata za Imbaseni, Maji ya Chai, Kikatiti hadi Samaria umesimama na mkandarasi amekimbia *site* kwa ukosefu wa fedha. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kule kwa ajili ya kukamilisha mradi huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Pallangyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa na tayari Serikali kupitia Wizara ya Maji tumeanza ku-*engage* na mkandarasi. Pia, tumeshakaa na wenzetu Wizara ya Fedha sasa tuweze kuanza kutoa fedha. Tayari kwa kipindi hiki tumepokea bilioni 16 kutoka *National Water Fund* na jana tumepokea bilioni tisa. Pia, tumeanza kupokea kutoka Serikali Kuu, tumepokea *exchequer* ya bilioni 105. Kwa hiyo, tunaamini kabisa miradi ambayo ilikuwa imekwamba pamoja na wakandarasi ambao walikuwa bado wanadai sasa wakati umefika wa kuanza kuwalipa ili warudi *site* na kuendeleza miradi ambayo ipo katika hatua mbalimbali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Nashoni William.

Na. 116

**Kupeleka Fedha Mradi wa Maji Kijiji cha Nyanganga - Kigoma Kusini**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kukamilisha mradi wa Maji uliokwama kwa muda mrefu Kijiji cha Nyanganga Kata ya Kazuramimba – Kigoma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu ya Maji ya Kijiji cha Nyanganga iliyopo Kata ya Kazuramimba, Wilaya ya Uvinza ilijengwa mwaka 1994 kwa lengo la kuhudumia wananchi 4,378 kwa wakati huo. Kwa sasa mahitaji ya maji katika kijiji hicho yameongezeka na kufikia lita 178,340 kwa siku, kutokana na

ongezeko la watu kufikia 8,917 mwaka 2024 sambamba na kuchakaa kwa miundombinu ya maji ya Skimu hiyo iliyodumu kwa takribani miaka 30 sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua changamoto hiyo, Serikali itakarabati Skimu ya Nyanganga kupitia bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, ili kurejesha ufanisi wake wa kuhudumia wananchi wa kijiji hicho. Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ukarabati wa tanki lenye ujazo wa lita 150,000, ukarabati wa mtandao wa mabomba umbali wa kilometa 3.2 na ukarabati wa vituo 10 vya kuchotea maji. Kazi ya ukarabati wa skimu hiyo inatarajiwa kuanza kufanyika Oktoba, 2024. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nashon.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ipo Miradi ya Maji ya Kijiji cha Mwakizega, Buhingu na Kandaga. Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; vipo Vijiji vilichimbiwa visima Basanza, Msebehi na Lemseni. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha sasa kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nashon, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza sana Mheshimiwa Nashon kwa kazi kubwa ambayo unaifanya kwa wananchi wa Uvinza, mimi ni shahidi kabisa kwamba, tulizunguka kijiji kwa kijiji, Kazuramimba, Uvinza yenyewe na maeneo mengine kujionea hali

halisi. Ninamhakikishia Mbunge kwamba, maeneo ya Basanza pamoja na maeneo mengine aliyoyataja, hatua ya kwanza tumechimba visima, hatua ya pili tunapima wingi wa maji na hatua ya tatu sasa tunaanza kufunga mitambo na kuhakikisha kwamba mtandao wa maji unakuwa unapatikana kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ambayo imesimama, Serikali kupitia Wizara ya Maji tumeshafanya tathmini ya miradi yote nchi nzima ambayo ipo katika hatua mbalimbali, tumeelekeza namna gani ya kwenda kuikamilisha. Kwa hiyo, kuanzia Mwezi wa Kumi mpaka wa Kumi na Mbili kuna baadhi ya miradi itakuwa imeshakamilika katika Mkoa wa Kigoma. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa mmesikia miradi yote ambayo ina changamoto mwezi wa Kumi na Mbili imekwisha. Kama mna maswali ya nyongeza swali hilo msiulize. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Byabato.

**MHE. STEPHEN L. BYABATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nimshukuru Dkt. Samia kwa utekelezaji wa mradi mkubwa wa upanuzi mtandao wa Maji Bukoba Mjini unaogharimu shilingi 3,300,000,000 na Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja kukagua na akatoa maelekezo. Kama alivyosema itaisha Desemba, lakini niliomba kujua ni lini 207,000,000 iliyobakia ya kuleta mabomba kwa ajili ya kukamilisha mradi wa maji zitaletwa Bukoba Mjini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Byabato, Mbunge wa Bukoba Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa tulifika Bukoba tukafanya ziara pia tukajionea hali ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi na hakika Bukoba kwa upande wa maji hali ni nzuri sana, lakini tunatambua kwamba uhitaji wa fedha hizo katika eneo hilo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutazisukuma haraka iwezekanavyo kuhakikisha kwamba, zinafika na mradi unakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, je ni lini Serikali itaanza kutekeleza mradi wa kimkakati katika Tarafa ya Nambisi, Halmashauri ya Mji wa Mbulu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kabisa naomba nilipokee swali la Mheshimiwa, ili nikawe na majibu ya uhakika ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria unatakiwa kuhudumia Jimbo la Rorya, Tarime Mjini – Vijijini, pale Sirari ujenzi wa tenki umesimama kabisa.

**NAIBU SPIKA:** Mwezi wa Kumi na Mbili, ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea, Dkt. Jasson Rweikiza.

Na. 117

**Miradi ya Maji Maeneo yenye Shida ya Maji Bukoba Vijijini**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka Miradi ya Maji maeneo ya Omubweya, Rugaze, Amani, Kamukole na Kitwe kwani kuna shida kubwa ya upatikanaji wa maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Vijiji vya Omubweya, Rugaze, Kitwe pamoja na Vitongoji vya Amani na Kamukole, Serikali imekamilisha utafiti wa maji chini ya ardhi, kwa ajili ya kuchimba visima virefu katika Vijiji vya Omubweya na Rugaze kupitia programu maalum ya uchimbaji wa visima 900. Aidha, kazi za uchimbaji wa visima na ujenzi wa miundombinu rahisi ya kutolea huduma *(point source)* katika vijiji hivyo itakamilika Desemba, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Serikali kupitia bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, itafanya upanuzi wa Skimu ya Maji ya Karabagaine kwa ajili ya kupeleka huduma ya maji katika vitongoji ambavyo havijafikiwa na mtandao wa maji katika Kijiji cha Kitwe ambapo utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika Oktoba, 2024 na Desemba, 2024 na kunufaisha wananchi wapatao 4,002 wa maeneo hayo. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya upanuzi wa Skimu ya Maji ya Kibirizi kupeleka huduma ya maji Vitongoji vya Amani na Kamukole.

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Rweikiza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninaishukuru sana Serikali kwa kuendelea kutuletea Miradi ya Maji Bukoba Vijijini, kwa kweli jitihada zinaonekana lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; miradi ya maji ya Bukoba Vijijini inajengwa na Wakala wa Maji Vijijini *(RUWASA)*. Je, Wizara ya Maji ina maslahi gani kwa kutaka kuhamisha miradi hii ambayo imekamilika ili iendeshwe na Mamlaka ya Maji ya Bukoba Mjini *(BUWASA)* kinyume na matakwa ya wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; pale Kemondo kuna mradi mkubwa sana wa maji ambao Serikali imejenga kupitia *RUWASA* hiyo hiyo (Wakala wa Maji Vijijini) wa shilingi bilioni 16 na sasa hivi umekamilika kwa 100% awamu ya kwanza. Ni kwa nini maji hayajaanza kutoka? Ni kweli kwamba kuna figisu za kutaka kuhamishia mradi huu Bukoba Mjini *(BUWASA)*? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa labda niseme hivi, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira na *RUWASA* kwa upande wa vijijini, vyote viko chini ya Wizara ya Maji. Ni dhamira ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kujikita kwenye utoaji wa huduma bora zaidi pamoja na kuhakikisha kwamba tunatoa maji safi na salama bila kujali kwamba yatatolewa na *RUWASA* ama yatatolewa na mamlaka yoyote. Lengo ni

kwamba, kwanza yawe na bei ambayo haitamuumiza mwananchi; hilo ndilo ambalo tunaliangalia kwa ukubwa wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha kuuchukua mradi mwingine kutoka *RUWASA* kwenda mamlaka tunaangalia ufanisi, hilo la kwanza. La pili, tunaangalia mahitaji ya wananchi wa eneo husika wanahitaji kuhudumiwa na nani; na la tatu tunaangalia utekelezaji jinsi ambavyo mradi ulianzishwa. Ninaomba kabisa kwamba kwenye hili lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunawaletea wananchi huduma iliyo bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la Kemondo, ni kweli kabisa nimefika pale Kemondo na nilipofika nilikuta kwamba kulikuwa na mitambo na *pump* zilikuwa hazijaletwa, nikatoa maelekezo. Tayari sasa hivi *pumps* zimeshaletwa na kilichobaki tunaongea na wenzetu wa *TANESCO*. Kuna mita fulani ambayo wanatakiwa kutufungia na baada ya kukamilisha; na mkandarasi wetu alikuwa anatudai pesa Fulani, wiki iliyopita tumemlipa hiyo pesa na anarudi *site*. Tutahakikisha kwamba mradi huo unakamilika na kuanza kutoa huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Francis Koka.

Na. 118

**Mradi wa Ujenzi wa Tenki la Maji la Pangani – Kibaha**

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa Ujenzi wa Tenki la Maji la Pangani – Kibaha utaanza kwa kuwa mkataba wa ujenzi ulishasainiwa tangu mwezi Desemba, 2023?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa *tank* la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita milioni sita katika Kata ya Pangani, Jimbo la Kibaha Mjini ambapo utekelezaji wake unatarajia kuanza Oktoba, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji *(Pump Station)*, sambamba na ununuzi na ufungaji wa pampu zenye uwezo wa kuzalisha maji lita 250,000 kwa saa, ujenzi wa *tank* la kukusanyia maji *(sump well)* lenye ujazo wa lita 540,000 na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 18.7. Muda wa utekelezaji wa mradi huo ni miezi 12 ambapo unatarajiwa kuhudumia wananchi 6,800 waishio kwenye Kata ya Pangani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Koka.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninampongeza Mheshimiwa Aweso, Waziri wa Maji kwa ziara aliyoifanya Disemba, 2023, ambapo tulisaini mikataba hii ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa baada ya kusaini mikataba hii ya utekelezaji wa mradi huu ni takribani sasa mwaka mmoja na ahadi ya Serikali ni mwezi wa 10. Je, Waziri yuko tayari mwezi Oktoba kufika Pangani ili kuzindua ujenzi wa mradi huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; katika kusaini ile mikataba, Mheshimiwa Waziri kupitia Mtendaji Mkuu wa *DAWASA* aliahidi kuwa ndani ya miezi mitatu utafanyika utaratibu wa

kutekeleza mradi mdogo wa kuhakikisha kwamba wananchi wa Kata ya Viziwaziwa na hususan Sagale Magengeni na Sagale Kambini na Viziwaziwa yenyewe wanapata maji; na ahadi iliyotoka pale ni kwamba kazi ile ilikuwa iko ndani ya uwezo wa Mtendaji Mkuu wa *DAWASA* na itafanyika ndani ya miezi mitatu na hadi sasa hivi ile kazi haijakamilika. Je, ni lini itafanyika ili wananchi wale wapate huduma kama ilivyoahidiwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Koka, kama ifuatavyo -

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wizara ya Maji hatupendezwi na hatutaki kuwa kikwazo kwa Watanzania kupata huduma ya maji safi na salama na sisi wenyewe hatuhitaji kuona miradi inasuasua. Kwa sababu ameliongea, ni suala *specific* sana, ninaomba niipokee changamoto hii ya Mheshimiwa Mbunge ili tukaifanyie kazi, tuone wapi mradi umekwama na tuweze kuchukua hatua stahiki. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Ikupa.

Na. 119

**Kujenga Vyumba vya Kujifungulia Wanawake Wenye Ulemavu**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Je, hospitali ngapi zimetenga vyumba vya kujifungulia wanawake wenye ulemavu nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali zote za rufaa za mikoa, hospitali 28 na hospitali sita za kanda (*CCBRT*, Mtwara, Chato Bugando, *KCMC* na *META* Mbeya) na Hospitali 184 za Halmashauri zina vyumba vya kujifungulia wanawake wakiwemo wanawake wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 21.1 kwa ajili ya kununua vifaatiba vitakavyowezesha kuboresha huduma za uzazi kwa akina mama wakiwemo wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga vyumba hivi kwa sababu ni ombi ambalo nililitoa ndani ya Bunge lako Tukufu katika kipindi hiki cha miaka mitatu; lakini pia Mheshimiwa Rais alipotualika watu wenye ulemavu pale Ikulu alielekeza vyumba hivi vitengwe. Jibu la msingi limeonyesha mafanikio makubwa sana; kwa hiyo, ninamshukuru sana Mheshiwa Rais Dkt. Samia Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya makubwa, je, Serikali ina mpango gani sasa kuhakikisha kwamba vyumba hivi vinatengwa kwenye ngazi ya vituo vya afya pamoja na zahanati?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nina ombi kwa Serikali. Katika hii shilingi bilioni 21.1 ambayo imetengwa kwa ajili ya kununua vifaatiba, basi iweze kuzingatia ununuzi wa zile *adjustable beds* ili ziweze kusaidia watu wenye ulemavu, wazee na wagonjwa ambao wanakuwa hawajiwezi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kulitazama hili eneo muhimu sana na amekuwa akifuatilia haya mambo kwa karibu. Nimwambie Mheshimiwa Mbunge, kwanza, moja tunaelekea kwenye dunia ya *inclusion,* kwa hivyo tusingependa kuona kwamba akina mama wanatengwa. Kwa sababu ukizungumzia akina mama wote ni akina mama, tofauti wana mahitaji tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, kwenye vyumba vile vya kujifungulia tunaweka mazingira ambayo yanahakikisha mama mwenye ulemavu mahitaji yake yamezingatiwa, yatakayom-*facilitate* yeye aweze kujifungua kwa usalama na bila kupata shida yoyote. Pia, kujenga *attitude* ya watumishi wetu kuhakikisha anapokuja mama mwenye ulemavu basi wanapelekwa kulingana na anavyokuwa, kwa sababu hata walemavu wenyewe wana mahitaji tofauti tofauti wanapokuja kwenye eneo la kutibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili la shilingi bilioni 21.1 ambazo zimetengwa na Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba zizingatiwe. Kwanza nimhakikishie, kama ambavyo yeye mwenyewe ameona; na hata Mheshimiwa Nderiananga, Naibu Waziri alikwenda kutembelea hospitali yetu ya mkoa hapa kuangalia mazingira hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, alijionea mwenyewe alichokisema Mheshimiwa Mbunge, kwamba sasa hivi kuna vitanda ambavyo Rais wetu ame-*supply*, unatumia *remote,* kinashuka kinamtolea mlemavu huduma kama ambavyo inatakiwa. Tutauzingatia huu ushauri wake aliousema hapa katika kwenda kununua hivyo vitanda na vifaa kama ambavyo ameshauri na tutaendelea kuchukua ushauri kutoka kwake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha vyoo vya watu wenye ulemavu vinawekwa kila wodi ya Mkoa wa Kagera, maana kuna vyoo vya kuchuchumaa tu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri na hasa kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia shughuli za afya kwenye Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia tu kwamba kwanza, moja, kwa hizi shilingi bilioni 21 ni mojawapo ya fedha zinazoenda kuhakikisha zinaboresha maeneo hayo ambayo yana shida. Hospitali yake ya Mkoa imekuwa ikikusanya kila mwezi zaidi ya shilingi milioni 300 mpaka shilingi milioni 400. Hivyo, ninamwelekeza Mganga Mfawidhi wa Hospitali, kwa kutumia mapato ya ndani aendelee kushughulikia maeneo yenye changamoto. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwa na unyanyapaa mkubwa sana wa watoa huduma wanaotoa huduma eneo la kujifungulia ama shughuli nyingine za hospitalini kwa watu wenye ulemavu. Je, Serikali ina mkakati gani, kama ilivyo kwenye elimu, wa kuhakikisha kwamba wale watoa huduma wanapata mafunzo rasmi kwa ajili ya kuwahudumia watu wenye ulemavu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge. Eneo hili ni nyeti sana na ndiyo maana unaona nimezungumzia hospitali za Taifa, kanda na wilaya. Ni maeneo ambayo tuna uhakika kwa 100% tayari mafunzo uliyoyasema yametolewa na miundombinu imewekwa pia. Sasa tunaelekea kwenye maeneo ya vituo vya afya na zahanati ili kuhakikisha si tu tunaboresha *infrastructure* lakini pia kubadilisha *attitude* ya watu na *attitude* ya wahusika wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli unapozungumzia walemavu kuna walemavu wasioona wanahitaji namna ya kuwasaidia, wasiosikia namna ya kuwasaidia. Kuna mama mwingine anakuja ana ulemavu lakini *pelvic girdle* yake imekaa kiasi kwamba unajua huyu ni moja kwa moja kwenye *operation* na chuma cha *operation* ni kile kila ambacho unatakiwa u-*operate* wote. Hutakiwi kuwa-*separate*, kila mama um-*treat* kama mama, lakini kila mmoja ana *specific need*. Hata wale ambao si walemavu wanapokuja kwenye eneo la tiba ambao kabisa hawana ulemavu wowote lakini wote wanahitaji *specific need* kulingana na yeye mwenyewe, kwa sababu kila mtu ana mambo yake yaliyojificha ambayo ni siri ya madaktari. Kwa hiyo, kikubwa ni *attitude* lakini kum-*attend* kila mtu *individually* kulingana na mahitaji yake.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Shally Raymond.

Na. 120

**Vituo Vinavyotoa Elimu ya Watu Wazima**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Je, kuna vituo vingapi vinavyotoa elimu ya watu wazima nchini na ni watu wazima wangapi wanapata elimu hiyo ikiwemo wanawake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha elimu ya watu wazima kupitia programu mbalimbali zilizo chini ya Sekta Ndogo ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu nje ya Mfumo Rasmi. Kulingana na Taarifa ya Tathmini ya Sekta ya Elimu *(ESA 2024)*, katika Programu ya Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA) mwaka 2023, jumla ya wanakisomo 97,217 wamenufaika katika vituo 1,851 ambapo wanaume ni 39,789 na wanawake ni 57,428.

Mheshimwa Naibu Spika, kupitia programu ya Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) mwaka 2023, jumla ya wanafunzi 57,843 wamenufaika katika vituo 2,557 ambapo wavulana ni 32,141 na wasichana ni 25,702.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika programu ya Mpango wa Elimu Changamani Baada ya Elimu ya Msingi *(Integrated Post Primary Education)*, jumla ya wanafunzi 9,368 wamenufaika katika

vituo 89 ambapo wanaume ni 5,036 na wanawake ni 4,332. Aidha, katika programu ya Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule *(Integrated Programme for Out of School Adolescents)*, jumla ya vijana 42,183 wamenufaika kupitia katika vituo 85, ambapo wanaume ni 20,195 na wanawake ni 21,988.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika, katika programu ya elimu ya sekondari kwa njia mbadala, wanafunzi 11,721 ikijumuisha wavulana 5,529 na wasichana 6,192 walidahiliwa kwa mwaka wa masomo wa 2023, ikitolewa katika vituo 777; vituo vya Serikali ni 160 na vituo vya wadau binafsi 617. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na hayo, kwa kuwa hadi sasa kuna vijana wanaomaliza darasa la saba hawajui kusoma na kuandika; na kwa kuwa hilo ni takwa maalum katika nchi yetu. Je, Serikali iko tayari sasa kurejesha ule mpango wa kutoa elimu na madarasa ya jioni kwa watu wazima ambao hawakufanikiwa kujifunza kusoma na kuandika katika shule ya msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, sambamba na elimu hiyo ya K.K.K, je, Serikali iko tayari kutoa mafunzo ya stadi za elimu ikiwepo kupika, kushona, kupasi kwa akina mama saa za jioni katika kata zetu na vijiji vyetu kupitia kwa Maofisa Maendeleo ya Jamii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya mama yangu, Mheshimiwa Shally Raymond kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Shally Raymond kwa maswali yake na vilevile kwa juhudi zake kwa kuwasemea akina mama wa Kilimanjaro pamoja na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la kwanza ambalo Mheshimiwa Mbunge anauliza kuhusiana na suala la maboresho ya elimu hii ya watu wazima katika kata zetu, ninaomba kwanza nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu. Katika matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi, eneo hili vilevile limeangaliwa, la kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa za sensa za mwaka 2022 inaonyesha kwamba, sasa hivi katika nchi yetu 17% ya Watanzania hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu. Asilimia hii imeshuka kutoka 22% ya mwaka 2012. Kwa hiyo, imeshuka kwa kiasi fulani, lakini bado tunasema asilimia hii ni kubwa kulingana na maisha ya sasa hivi na karne ya sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge. Katika maboresho ya Sera ya Elimu pamoja na mitaala tuliyofanya mwaka jana (2023), jambo hili limeingizwa. Hivi sasa katika halmashauri zetu zote tumeanzisha idara pamoja na vitengo vya elimu ya watu wazima, kwa maana ya elimu ya msingi na sekondari kwa kuteua Maafisa Elimu ya Watu Wazima ngazi ya msingi na Maafisa Elimu ya Watu Wazima ngazi ya sekondari. Sasa tunakwenda kuanzisha madarasa yale katika kata zetu na vijiji vyetu kule kote na hawa maafisa wetu ndio watakaokuwa wasimamizi wakuu katika eneo hilo. *(Makofi)*

Katika eneo la pili analolizungumza, kwamba sasa tuanzishe programu mbalimbali wa ajili ya akina mama, nimwondoe wasiwasi, Serikali yetu inatekeleza programu inayoitwa *integrated approach*. Katika programu hii ina elimu changamani ambapo stadi hii za K.K.K

zinafundishwa pia zinachanganywa na stadi nyingine za ujasiriamali, stadi za maisha, upishi na masuala ya uhifadhi wa mazingira na maeneo mengine. Kwa hiyo, tayari Serikali inalifanyia kazi jambo hili na tunaendelea kulifanyia kazi kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Taska Mbogo.

Na. 121

**Ujenzi wa Reli ya Kisasa kutoka Mpanda – Bandari ya Karema**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Mpanda Mjini kwenda Bandari ya Karema, Ziwa Tanganyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa Serikali inaendelea na utekelezaji wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa kutoka Dar es Salaam – Mwanza kilometa 1,219 kwa awamu ya kwanza na kutoka Tabora – Kigoma kilometa 506 na Uvinza Musongati kilometa 282 kwa awamu ya pili. Ujenzi huu uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo kipande cha Dar es Salaam – Dodoma kilometa 444 kimeanza uendeshaji kwa safari za abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* linaendelea na maandalizi ya ujenzi wa reli ya kisasa kutoka

Kaliua – Mpanda – Bandari ya Karema ambapo upembuzi yakinifu umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inaendelea kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Kaliua – Mpanda – Karema yenye urefu wa kilometa 321 kwa kiwango cha *standard gauge (SGR)*. Reli hii inatarajiwa kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Bandari ya Karema kwa upande wa Tanzania na Bandari ya Kalemie kwa upande wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Ujenzi huo utaanza mara baada ya kupatikana kwa rasilimali fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza tunaishukuru Serikali kwa ujenzi wa bandari. Swali la kwanza; kwa kuwa bandari imeshakamilika na kwa kuwa ujenzi wa reli hii unakwenda kuunganisha Nchi yetu ya Tanzania na Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, pia inakwenda kutoa fursa kwa wananchi wa Tanzania hususan wananchi wa Mkoa wa Katavi kufanya biashara na Nchi ya Congo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupata fedha kuharakisha ujenzi wa reli hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa upembuzi yakinifu umeshakamilika wa kilometa 321 kutoka Kaliua Mpanda hadi Kalema kwa ajili ya ujenzi wa reli hii, lakini katika ujenzi huo kuna wananchi ambao watapisha ujenzi wa reli hii. Je, ni lini wananchi wanaopisha ujenzi wa reli hii watalipwa fidia yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama utaridhia kabla sijajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Taska

Mbogo, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa tukio kubwa linaloendelea sasa hivi Nchini China, ambapo yeye pamoja na Marais wenzake, Rais wa China pamoja na Mheshimiwa Rais wa Zambia, wamesaini hati ya makubaliano ya kuboresha reli yetu ya *TAZARA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Bungeni mara kadhaa hoja hii imeulizwa kila wakati, ni lini *TAZARA* itaboreshwa, leo hati maalum ya makubaliano imesainiwa ili kuifumua *TAZARA* iweze kubeba mzigo na kufungua biashara kati ya nchi yetu na Nchi za Congo na nchi ya Zambia na sote tunafahamu tuna *potential* ya mzigo wa *ten million metric tons Congo* pamoja na *seven million metric tons* upande wa Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye swali la Mheshimiwa Taska Mbogo, namba moja anauliza mkakati wa kupata fedha. Serikali ya Tanzania imejitambulisha kwamba ndiyo Serikali inayoongoza Barani Afrika kwa kuwa na agenda maalum kwenye reli, ndiyo maana tunajenga reli ndefu kuliko reli nyingine yoyote katika Bara letu na duniani tukiwa ni nchi ya tano. Ninamwomba Mheshimiwa Mbogo pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wa mikoa hiyo wavumilie kidogo, tupo kwenye kipande cha saba sasa kwa maana kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza wakandarasi wapo *site* tayari na kutoka Tabora mpaka Kigoma wapo *site* tayari na kutoka Kigoma Uvinza kuelekea mpaka Burundi tupo kwenye hatua za kumpata mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbogo avumilie, tukimaliza hapa tutarudi kwenye vipande vingine vinavyoendelea ikiwa ni pamoja na kwake Kaliua - Mpanda, pamoja cha Mtwara *Corridor* ambacho najua Wabunge wa Mtwara lazima wangeuliza, leo pamoja na kutoka Rusumo kwenda mpaka Kigali na kutoka Tanga, Arusha na Musoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya pili, Serikali hii inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, inajali wananchi wake. Nimhakikishie pale itakapobainika kunahitaji fidia wananchi hawa kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi yetu watapewa fidia zao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Geoffrey Mwambe.

Na. 122

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi – Masasi**

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo kipya na cha kisasa cha Polisi na kuboresha Makazi ya Askari Polisi Wilayani Masasi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Masasi Mjini, kama ifutatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetenga fedha kiasi cha Shilingi 798,000,000 kutoka kwenye bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Masasi. Aidha, tathmini kwa ajili ya ukarabati wa nyumba 13 za makazi ya Askari Polisi imefanyika na kiasi cha Shilingi 123,172,200

zinahitajika. Fedha hizo zinatarajiwa kutengwa kutoka Mfuko wa Tuzo na Tozo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Napenda kuishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kutokana na umuhimu wa kituo hiki cha polisi cha Masasi, ambacho kinahudumia Wilaya za jirani pamoja na Nchi jirani ya Msumbiji, *especially* pale kwenye mpaka. Wizara ipo tayari sasa kutoa mgao maalum wa angalau magari mawili ili kuongeza nguvu ya hilo jengo ambalo litajengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, hivi karibuni tulipata dhahama kubwa sana pale Masasi Mjini kwa soko kubwa la Masasi kuungua moto. Je, Wizara hii ya Mambo ya Ndani ipo tayari kutoa mgao wa gari ya zimamoto ya kisasa kabisa ili kuweza kuongeza nguvu kwa wananchi wetu kuokoa mali zao? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutenga magari kwa ajili ya Wilaya ni nia ya Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, hususani Jeshi la Polisi, kuhakikisha Wilaya zake zote zinapata vitendeakazi yakiwemo magari, pikipiki na vifaa vingine. Kwa hivyo nimhakikishie tu kwamba sasa hivi tukamilishe ujenzi wa hicho kituo, lakini hatua itakayofuata ni kuwawezesha kwa vitendeakazi yakiwemo magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu soko lililoungua ni dhamira ya Serikali, hususani Wizara ya Mambo ya Ndani, Jeshi la Zimamoto na Uokozi kupeleka vifaa vya kisasa katika Wilaya zake zote na Mikoa ambayo haikuwa nayo. Nadhani limejibiwa mara kadhaa hapa

kwamba, Serikali imeingia makubaliano na nchi wahisani kwa ajili ya kupata fedha zitakazowezesha ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto kwa ajili ya mikoa yote na wilaya zake zote. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Conchesta.

Na. 123

**Kuanzisha Mfuko Maalum wa Kuhudumia Jeshi la Magereza**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Je, kwa nini Askari wa Jeshi la Magereza wasihudumiwe na Mfuko Maalum kama Majeshi mengine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi wa Jeshi la Magereza wanachangia na kupata huduma za mafao kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma *(PSSSF)* kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma Na. 2 ya 2018 *(The Public Service Social Security Fund Act No. 2 of 2018)*. Kwa kuzingatia utofauti uliopo kati ya Watumishi wa Jeshi la Magereza na Watumishi wengine wa Umma hususan umri wanaoutumia kazini, kwenye utumishi kwa kuzingatia umri wa ajira na kustaafu kwa vyeo, muda wa kazi (masaa 24), asili ya kazi (mazingira hatarishi), Serikali imeanza kuchukua hatua kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali ili kupata maoni na mapendekezo ya namna bora ya kushughulikia uchangiaji na ulipwaji wa mafao

ya wastaafu wa vyombo vya usalama walio chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wakiwemo wa Jeshi la Magereza. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ni mara ya tatu nauliza swali hili na Askari Magereza wamekuwa na kilio cha muda mrefu, kwa sababu wapo chini ya utumishi, wanapenda kulipwa kupitia Mfuko wa *consolidated*. Ni kwa nini Serikali imechelewesha jambo hili na hapa wanasema kuwa wanatafuta wadau, ni wadau gani ambao Serikali wenyewe wanashindwa kuhakikisha kwamba hao watu wanapata haki kupitia Mfuko huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo chini ya Utumishi, Askari Magereza wamekuwa hawapandi vyeo kwa wakati na wakati mwingine hata madaraja yao hayapandi kwa sababu wao wanahudumiwa na Tume ya Utumishi. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba jambo hili sasa linakamalika na wao wanapata haki yao kama Askari wengine? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, najua mama Conchesta na baadhi ya wabunge wamekuwa wakizungumzia suala hili na hisia hizi ni za msingi kwamba wangependa walipwe kutoka *consolidated fund*. Kimsingi nasema linatekelezwa kwa mujibu wa sheria kama nilivyojibu katika jibu la msingi. Ili sheria iweze kufanyiwa marekebisho huhusisha uhusikaji wa wadau mbalimbali wakiwemo Wabunge, Jeshi la Magereza, wadau wengine ni muhimu ili kuwezesha jambo hilo kufanyika. Kwa hiyo ndiyo maana tunasema mjadala unaenda kwa kuwashirikisha

wadau ili muafaka utakapofikiwa waweze pia kuwa *elevated* kutoka huku ili waweze kulipwa *consolidated fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niseme *the way* anavyoiongea Mheshimiwa Mbunge ni kama vile wanaolipwa kupitia Utumishi wanaonewa, si kweli. Kwa mfano, amezungumzia kupanda vyeo, Magereza kama vilivyo vyombo vingine vya Wizara ya Mambo ya Ndani, hawapandishwi vyeo na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, badala yake ipo Tume ya Utumishi wa Magereza, *Fire*, Uhamiaji, pamoja na Polisi wenyewe ambapo Tume hukaa kila mwaka kwa ajili ya kuwaona waliokuwa *due* kupanda wanapandishwa. Kwa hivyo, si kwamba kwa sababu hawapo chini ya *consolidated fund* basi kule Utumishi wanaonewa. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Maige, Mheshimiwa Almas.

Na. 124

**Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Uyui**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Uyui uliopangwa katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania, imeendelea kuimarisha majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujenga

majengo mapya na kukarabati yaliyopo. Kutokana na uhaba wa majengo ya Mahakama, majengo haya yanajengwa na kukarabatiwa kwa awamu kwa kuzingatia mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama na kadri ya fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Mpango huo, jengo la Mahakama ya Wilaya ya Uyui linajengwa kwa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kwa sasa taratibu za ununuzi wa kumpata mkandarasi zinaendelea. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Maige.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ni sababu gani zilifanya mradi huu usitekelezwe katika Mwaka wa Fedha wa 2023/2024?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali sasa ipo tayari kuongeza mradi wa kujenga nyumba za watumishi wa Mahakama katika mradi huu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mradi huu awali ulipangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, lakini kutokana na kwamba fedha za mradi huu zinapatikana kutoka kwa wadau wetu wa maendeleo hususani Benki ya Dunia, utekelezaji wa vigezo kwa ajili ya kupata fedha hii ulichelewa kukamilishwa na hivyo kusababisha fedha hizi kuvuka mwaka. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, sasa hivi fedha zimeshapatikana na ndiyo maana tupo kwenye hatua ya manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, juu ya kujenga nyumba katika mradi huu, naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu mradi umeshapangwa ni kwa ajili ya kujenga Mahakama, kutakuwa na awamu nyingine ya kushughulikia nyumba za watumishi wa Sekta ya Mahakama. Kwa hivyo, awe na subira katika awamu itakayofuata tumeweka pia uboreshaji wa nyumba zikiwemo watumishi wa Mahakama upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, kwa niaba yake Mheshimiwa Mheshimiwa Kabati.

Na. 125

**Muswada wa Sheria ya Adhabu ya Kifo kwa Wabakaji**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuleta Muswada wa Sheria utakaotoa adhabu ya Kifo kwa wabakaji wa watoto walio chini ya miaka tisa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 131(1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 imeainisha adhabu ya makosa ya kubaka kuwa ni kifungo kisichopungua miaka 30, viboko na Mahakama inaweza kutoa amri ya kumlipa fidia muathirika wa tukio. Aidha, Kifungu 131(3) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu kimeainisha kuwa ikiwa muathiriki wa tukio ni mtoto mwenye umri

chini ya miaka 10 adhabu pekee iliyokuwepo ni kifungo cha maisha jela.

Mheshimiwa Naibu Spika, adhabu ya kifungo cha maisha kwa mujibu wa sheria zetu ni muda wote wa uhai wa mkosaji ambayo ni adhabu ya pili kwa ukubwa ukiachilia adhabu ya kifo inayotolewa kwa makosa ya uhaini na kuua kwa kukusudia. Hata hivyo, Serikali inalichukua suala la Mheshimiwa Mbunge, kama sehemu ya maeneo ya kufanyiwa kazi na kuona kama ipo haja ya kuongeza adhabu kwa wanaobaka watoto chini ya miaka 10 au tuendelee na adhabu iliyopo ya kifungo cha maisha jela, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, sasa hivi ubakaji umeshika kasi sana na hasa katika Mkoa wetu wa Iringa, imetokea hata vijana kwa vijana wanabakana wenyewe kwa wenyewe ambao wapo chini ya umri wa miaka 18. Je, sheria inasemaje kwa watoto wanaobakana wao kwa wao shuleni?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; tatizo hili limekuwa kubwa sana hapa nchini na tumeona mpaka muuliza swali anasema kwamba wauawe, lakini naona je, kuna uwezekano labda wahasiwe, maana yake imekuwa ndiyo tatizo kubwa sana? *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, kufuatia kumomonyoka kwa maadili, baadhi ya matendo ambayo huko nyuma hatukuzoea kuyasikia Watanzania yameongezeka kwa kasi

ikiwemo matukio ya ubakaji na sasa amesema kwa watoto pia shuleni yanafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kosa hata kama limefanywa na mtoto ni kosa, lakini kwa maana ya sheria zetu mtoto atahukumiwa chini ya Sheria ya Watoto na hivyo ikitokea mmoja kamfanyia vitendo visivyo vya maadili kama hilo, taarifa zikipelekwa kwenye vyombo vya dola na ikapelekwa Mahakamani, mtoto atahukumiwa kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja kama ni kifungo atafungwa kwenye Mahakama ya watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la pili, Mheshimiwa naona analiongea kwa hisia, ni kweli kwamba jambo hili linaudhi lakini sasa hicho anachokisema hakipo kwenye sheria zetu, kama tutafika hatua hiyo ni pale ambapo Bunge lako litakuwa limerekebisha sheria na kuruhusu hicho anachokisema Mheshimiwa Mbunge. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni kama ifuatavyo:-

Wageni waliokaa jukwaa la Spika, wageni wawili wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambao ni Dkt. Alli Said Yusufu, Mhadhiri Mwandamizi (*Anaesthesia and Critical Medicine)* Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar; Ndugu Fatma Kikkides, Mratibu wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania (JMT) na Balozi wa Amani Duniani kwa tiketi ya *IWPG*. Karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni mgeni wa Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, ambaye ni ndugu yake kutoka Jijini Arusha. Karibu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dodoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Katibu wa Umoja wa Vijana Chama Cha Mapinduzi, Kata ya Matevesi, kutoka Jijini Arusha. Karibu. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi, Tawi la Tasani kutoka Jimbo la Makunduchi Kusini Unguja. Karibu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, viongozi wa Chama Cha Wamiliki Ardhi na Nyumba Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, marafiki zake kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, kikundi cha wananchi wa Masasi kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 60 wa Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, wafanyabiashara kutoka Jimbo la Ngara Mkoa wa Kagera. Karibuni. *(Makofi)*

Pia wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wageni kutoka Taasisi ya Tanzania *Artist Unity for Community Development (TAFOSDE)* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni sita wa Kituo cha Maendeleo ya Mtoto na Kijana kutoka Iramba Mkoa wa Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 28 wa Kikundi cha Wanautalii Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 120 na Walimu tisa wa Shule ya Sekondari ya Kiislam ya Daarul – Arqam kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 74 na walimu watano wa shule ya Awali na Msingi ya Libermann kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Katibu wa Wabunge wanawake wa CCM anawatangazia Wabunge wanaweka wa CCM kuwa leo baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge kutakuwa na kikao cha Wabunge Wanawake wa CCM katika ukumbi wa Msekwa B. Tangazo hili limetolewa na Mheshimiwa Subira Mgalu, Katibu wa Kamati ya Wabunge Wanawake wa CCM.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano, pamoja na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, namwita Mwenyekiti.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – KAMATI YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo 38 zilizowekwa mezani wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge. Taarifa hii inajumuisha uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo 22 zilizowekwa Mezani wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kuona umuhimu wa kuiweka taarifa hii kwenye orodha ya shughuli za Bunge *(order paper)* za leo kwa mamlaka uliyonayo kwa mujibu wa Kifungu cha 10(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Bila shaka uamuzi huu umetokana na uongozi wako mahiri na azma yako madhubuti ya kuliwezesha Bunge kutimiza wajibu wake wa kusimamia misingi ya kidemokrasia kupitia usimamizi wa madaraka ya Bunge ya kuziweka sheria ndogo katika mfumo wa sheria. Kwa ajili ya changamoto ya muda naomba kusoma taarifa hii kwa muhtsari, lakini niombe taarifa yote na viambatisho vyake kama vilivyoko mezani iingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba inalipa Bunge mamlaka ya kutunga Sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Kwa mantiki hiyo utungaji wa sheria zote upo kwenye mamlaka ya Bunge. Bunge linaruhusiwa kukabidhi kwa mtu yeyote au kwa idara yoyote ya Serikali madaraka ya kuweka kanuni zenye nguvu ya kisheria au kuzipa nguvu za kisheria kanuni zozote zilizowekwa na mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali. Kwa msingi huo sheria na kanuni zinapaswa kuzingatia masharti ya Ibara ya 8(1)(a) kwamba, wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na kwamba Serikali imepata madaraka yake na mamlaka yake kutoka kwa wananchi.

Hivyo, sheria zote za nchi zinapaswa kuweka masharti yanayolinda na kuzingatia ipasavyo maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, mambo yanayozingatiwa wakati wa uchambuzi; ili kufikia tija iliyokusidiwa pamoja na matarajio ya Bunge yapo mambo yaliyozingatiwa wakati wa uchambuzi wa taarifa za utekelezaji na uchambuzi wa sheria ndogo. Naomba kulijulisha Bunge mambo hayo kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio hayo. Udadisi wakati wa uchambuzi ulilenga kufahamu yafuatayo:-

(a) Iwapo hakuna kabisa utekelezaji wa maazimio.

(b) Iwapo utekelezaji wa maazimio umefikia hatua ya rasimu ya marekebisho katika ngazi ya Wizara.

(c) Iwapo utekelezaji wa maazimio umefikia hatua ya rasimu ya marekebisho kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki; na

(d) Iwapo utekelezaji wa maazimio umefikia hatua ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa sheria ndogo kipimo kikuu kilichotumika ni masharti ya Katiba, sheria mama na sheria nyingine za nchi. Kamati ililenga kujiridhisha na mambo makuu matano yafutayo:-

(a) Iwapo sheria hizo ndogo zina masharti yanayokizana na Katiba.

(b) Iwapo sheria ndogo zina masharti yanayokizana na sheria mama na sheria nyingine za nchi.

(c) Iwapo sheria ndogo zina makosa ya kutoendana na misingi ya uandishi.

(d) Iwapo sheria ndogo zina masharti yasiyo na uhalisia kwa kiasi cha kusababisha changamoto katika utekelezaji wake; na

(e) Iwapo sheria ndogo zina majedwali yenye dosari kama vile: -

(i) Kutofautiana na vifungu vya sheria ndogo vinayaanzisha.

(ii) Kutokukamilika ilivyostahili.

(iii) Kutajwa katika sheria ndogo inayohusika lakini yakakosekana.

(iv) Kujitokeza bila kuwa na kifungu cha sheria ndogo kinachoyaanzisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matokeo ya uchambuzi. Katika sehemu ya matokeo ya uchambuzi Kamati inalijulisha Bunge kuhusu yaliyobainika wakati wa shughuli kuu mbili kama ifuatavyo:-

Matokeo kwa shughuli ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji; ni wajibu wa Bunge kuhakikisha kwamba madaraka yake ambayo yamekabidhiwa kwa mamlaka nyingine yanatumika inavyostahili. Kutokana na wajibu huo Bunge halipaswi kuishia kutoa maazimio yanayotaka marekebisho ya sheria ndogo bali pia linapaswa kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Bunge linaituma Kamati ya Sheria Ndogo kusimamia utekelezaji bora wa madaraka ya sheria ndogo yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine Kamati hii ilifuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Lengo ni kuona hatua inayofikiwa na kulinganisha na hatua inayostahili ili kulishauri Bunge uamuzi unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo hayo yanaonesha kwamba hatua zilizoripotiwa za kusahihisha dosari ili kutekeleza maazimio ya Bunge zinagawanyika katika makundi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la kwanza, hatua ya rasimu ya marekebisho kuwasilishwa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki. Marekebisho ya sheria ndogo zote yanatarajiwa kufikishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki kabla ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi umebainisha kwamba hadi wakati Kamati ilipokutana na Wizara zinazohusika ni sheria ndogo tatu tu zilizo chini ya Wizara ya Nishati, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Wizara ya Fedha zilikuwa zimefikia hatua hii. Hatua iliyofikiwa inakabiria kutangazwa kwa marekebisho katika Gazeti la Serikali. Kwa maelezo yaliyowasilishwa kwenye Kamati marekebisho yatakamilika katika muda mfupi ujao. Itakapofikia hatua hiyo changamoto zilizobainika na kero miongoni mwa sheria hiyo ndogo zitakuwa zimetatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la pili, hatua ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali; Marekebisho yoyote ya sheria ndogo hayawezi kuanza kutekelezwa kabla ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Tathmini imeonesha kwamba hadi tarehe 23 Agosti, 2024 sheria ndogo 19 zilikuwa zimefikia hatua ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Wizara zinazohusika na sheria ndogo hizo ni: Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Waziri wa Habari,

Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wizara ya Kilimo; Wizara ya Nishati; Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu; Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Fedha; Wizara ya Uchukuzi; na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla hatua kuu mbili zilizofikiwa kama zinavyofafanuliwa katika Kiambatanisho cha mbili ni sehemu ya juhudi za kurekebisha dosari zilizokuwa zimejitokeza. Dosari hizo zinahusu sheria ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge hili. Kwa juhudi hizo ni jambo jema kuanza mchakato wa kuondoa madhara ya dosari kama ilivyoazimiwa na Bunge. Hata hivyo, ni muhimu kwa mamlaka zinazokasimiwa na Bunge madaraka ya kuweka sheria ndogo kufanya marekebisho kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge yanaonesha dosari za namna tano kama inavyoonekana katika kiambatanisho namba moja. Ninaomba jedwali hilo lisomwe kwa pamoja na taarifa hii na liingizwe kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. Aidha, dosari zilizobainisha katika jedwali hilo zinajitokeza kwenye sheria ndogo zaidi ya moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuliwezesha Bunge kufikia uamuzi unaostahili, ninaomba kufafanua dosari zilizotajwa hapo juu kwa mifano halisi kama ilivyobainika wakati wa uchambuzi. Ufafanuzi huo ni kama ifuatavyo:-

(a) Namna ya kwanza, ni dosari ya masharti yanayokizana na masharti ya Katiba. Nia ya sheria ndogo ni kufanikisha lengo kuu la sheria mama inayotungwa na Bunge. Aidha, sheria ndogo kama zilivyo sheria nyingine za nchi zinatarajiwa kuendana na masharti ya Katiba ambao ni msingi mkuu wa

sheria za nchi zikiwemo sheria mama. Hata hivyo uchambuzi unabainisha baadhi ya sheria ndogo zenye maudhui yanayotofautiana na matakwa ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa sheria ndogo zenye dosari hiyo ni Sheria Ndogo ya Udhibiti wa Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024, Tangazo la Serikali Namba 38 la Tarehe 19 Januari, 2024. Kifungu cha 26 cha sheria ndogo hii kinataja makosa mbalimbali yanayokatazwa ikiwemo kosa kwa mtu yeyote kufanya shughuli za kisiasa ikiwa ni pamoja na kupandisha bendera ya chama cha siasa. Katazo hilo limewekwa pasipo kufafanua maeneo yaliyoguswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna katazo lilivyowekwa inaweza kutafsiriwa kwamba watu wote wanakatazwa kufanya shughuli za kisiasa, jambo ambalo ni kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, sheria ndogo kuwa na masharti yasiyoenda na Katiba kama ilivyo kwa sheria ndogo hii ni dosari kubwa katika sheria za nchi. Madhara yake ni pamoja na sheria inayohusika; mosi, kutokuwa halali; pili, kukiuka misingi ya utawala wa sheria; na tatu kuathiri vibaya masharti ya misingi ya demokrasia nchini. Njia pekee ya kusahihisha dosari hiyo ni kuirekebisha sheria ndogo iliyobainika kuwa na dosari hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, namna ya pili, ya dosari ni kuwa na masharti yanayokinzana na sheria mama na sheria nyingine za nchi. Kama tunavyofahamu sheria ndogo zinazotokana na mamlaka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa sheria iliyotungwa na Bunge. Hivyo katika hali ya kawaida sheria ndogo hazitarajiwi kukiuka masharti ya sheria ambayo inaipa nguvu.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo ikiwa sheria ndogo yoyote itakuwa na maudhui yanayokinzana na yale ya sheria mama itakuwa imejipa nguvu isiyotokana na ithibati ya mamlaka yake. Zaidi ya maelezo hayo uandishi wa sheria za nchi ni zao la misingi iliyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinakataza sheria ndogo kukinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi. Vilevile, Kifungu hicho kinabatilisha sheria ndogo itakayokinzana na masharti ya sheria mama au sheria nyingine ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya masharti hayo ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, uchambuzi umeonesha kuwa zipo sheria ndogo zenye dosari ya kukinzana na sheria mama. Mfano wa Sheria ndogo hizo; Ni Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira, Halmashauri ya Kibondo, 2023, Tangazo la Serikali Namba 920 la Tarehe 22 Disemba, 2023, Kifungu cha 16 (e) cha sheria ndogo hii kinaweka katazo kwa mtu yeyote aliye ndani ya gari kudondosha taka ngumu nje ya gari ikiwa ndani au nje ya kituo cha magari na sehemu yoyote ile ambapo gari hilo litapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ndogo hii imekataza utupaji wa taka ngumu pekee yake bila kujumuisha taka laini na nyinginezo. Kutokutajwa kwa taka laini na nyinginezo kunaweza kufatsiriwa kuwa ni ruhusa kwa kutupa taka laini au taka nyinginezo. Tafsiri hiyo inaathiri vibaya lengo la sheria ndogo na utekelezaji wa sheria ya Bunge ambayo ni sheria ya usimamizi wa mazingira hususani lengo la kuweka mazingira kwenye hali ya usafi na usalama.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, namna ya tatu, ya dosari ni kuweka mashari yasiyo na uhalisia. Pamoja na masuala mengine waandishi wa sheria hulenga kuweka masharti

mbalimbali ambayo ni zao la utekelezaji wake na ni kulishughulikia, kufanikisha na kutatua jambo fulani miongoni mwa wanaolengwa na masharti yanayohusika. Pamoja na hivyo matokeo ya uchambuzi yanabainisha kuwa yapo masharti yaliyowekwa na sheria ndogo ambayo utekelezaji wake hauna uhalisia ikilinganishwa na lengo la sheria inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari hiyo imebainika katika katika Sheria Ndogo ya Afya, Usafi wa Mazingira na Usimamizi wa Halmashauri ya Iringa ya 2024, Tangazo la Serikali Namba 30 la Tarehe 12 Januari, 2024. Dosari ya kukosa uhalisia ilibainika katika kifungu cha 7 kinachohusu udhibiti wa kelele kwa shughuli mbalimbali za kijamii. Kifungu hicho kimeweka sharti kuwa mtu yeyote anayetaka kutumia kinga vuke *(generator)* kupata kubali cha Halmashauri. Sharti hilo halifafanuliwi iwapo muda wa kibali hicho ni kwa siku, wiki, mwezi, mwaka na wala mazingira yanayosabisha kuomba kutumia kinga vuke. Uwekaji masharti hayo unasababisha mkanganyiko miongoni mwa wasimamizi na walengwa. Hivyo ni kukwamisha dhima ya kufafanua utekelezaji wa sheria mama na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari nyingine za kukosa uhalisia inatokana na kifungu kuweka sharti la kupata kibali cha halmashauri kwa kitu kingine chochote pasipo kubainisha kitu kinachohusika. Masharti haya yamewekwa bila kuwa na mipaka ya mambo hayo. Kwa namna hiyo masharti yaliyowekwa yanagusa upana mkubwa usiokusudiwa na sheria ndogo hii, jambo ambalo linaweza kutaabisha walengwa bila sababu.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, namna ya nne ni dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria. Misingi ya

uandishi wa sheria inalenga kuwezesha sheria za nchi kufanikisha hatua za sheria za Serikali, kisera na kisheria. Lengo hili linafikiwa kwa sheria kueleweka kwa urahisi miongoni mwa wananchi wanaoguswa pamoja na wanaosimamia na wenye jukumu za kuzitafsiri. Bunge linapotunga sheria huzingatia misingi ya uandishi ambayo huwezesha mawazo ghafi kuwekwa katika ukamilifu unaoeleweka na wenye namna halisi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nzuri ya Mwandishi Mkuu wa Serikali nchi inaliwezesha Bunge kuzingatia misingi ya uandishi wa Sheria. Iwapo Bunge ambalo ndilo lenye mamlaka kamili ya utungaji wa sheria huzingatia misingi ya uandishi, sheria ndogo zinazotokana na Sheria za Bunge, nazo zipaswa kuandikwa kwa kuzingatia misingi dhati ya uandishi wa sheria. Hata hivyo, uchambuzi umeonekana kwamba zipo sheria ndogo zenye dosari za kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa sheria ndogo zenye dosari hiyo ni *Regulations Under the Atomic Energy Protection from Ionizing and Non-Ionizing Radiation, 2023*, Tangazo la Serikali Namba 840 la Tarehe 17 Disemba, 2023. Tatizo la uandishi lilibainika katika Kanuni ya 8(1). Kanuni hiyo inaweka masharti kwamba, mtu yeyote anayehusika kufanya jambo linalotajwa bayana katika kanuni hizi atalazimika kuitaarifu Tume kwa namna inayoelekezwa na Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, isivyo bahati Kanuni hazina maelekezo yanayowekwa utaratibu unastahili kufuatwa katika utekelezaji masharti ya kuitaarifu Tume kuhusu kusudio la kufanya jambo linalobainishwa kwenye kanuni hizi. Hivyo, dosari hiyo ya kiuandishi inaathiri ukamilifu wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa dosari za uandishi hazitarekebishwa upo uwezekano wa dosari hizo kukwamisha utekelezaji mzuri wa sheria zilitotungwa na Bunge.

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, namba tano, ni dosari ya uandishi wa majedwali. Kwa kawaida majedwali katika sheria yoyote hulenga kutoa ufafanuzi zaidi na kutimiza malengo ya kifungu cha sheria kinachohusika. Kwa minajili hiyo jedwali likiwa na dosari kwenye uandishi wake linaweza kukwamisha ufafanuzi uliokusudiwa na hatimaye kukwamisha lengo la sheria inayohusika. Licha ya ukweli huo uchambuzi umeonesha kwamba kuna sheria ndogo zenye dosari ya uandishi wa majedwali.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari hizo ni pamoja na: Mosi, kutorejea vifungu sahihi vinavyoainisha majedwali hayo; na pili, kutokamilika katika maudhui au jedwali kuwa na maudhui yanayokanganyana. Mfano wa sheria wa ndogo zenye dosari za uandishi wa majedwali ni Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024, Tangazo Namba 39 la Tarehe 19 Januari, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la kwanza linalohusu utozaji wa ada na ushuru kwa ajili ya huduma mbalimbali imebainika kuandikwa kwa namna inayoacha utata. Sehemu ya kwanza ya jedwali hilo inaweka ada ya vibali vya burudani ya kandanda kwa viwango vya shilingi 1,000 kwa mtu mzima na shilingi 500 kwa mtoto. Uandishi wa namna hiyo unaacha utata kuhusu burudani inayohusika kwenye ada inayotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, kipimo kikuu kilichotumika ambacho kinagusa masharti ya Katiba, sheria

mama na sheria nyingine za nchi kimesaidia kubaini jumla ya sheria ndogo 36 zenye dosari za namna kuu nne kama ilivyobainishwa kwenye kiambatisho namba moja. Jambo muhimu kwa Bunge ni kuazimia kufanyika kwa marekebisho ili kuepuka madhara ya dosari hizo katika mfumo wa sheria na kwa maisha ya wananchi wanaowakilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na mapendekezo; Maoni; kwa kuwa sheria ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya wananchi katika utekelezaji wake, ninaliomba Bunge lipokee mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii na kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni hayo, naomba kudhihirisha mtazamo wa Kamati unaojenga misingi ya mapendekezo hayo kama ifuatavyo:-

(i) Dosari ya Sheria Ndogo kukinzana na masharti ya Katiba inaathiri uthabiti wa mfumo wa sheria za nchi. Hivyo, kuwa na madhara wakati wa utekelezaji, madhara hayo ni kama vile: Mosi, ukiukaji wa haki za kimsingi na uhuru unaohakikishwa na katiba; pili, matumizi mabaya ya mamlaka; tatu, ukiukwaji wa uhuru wa raia; na nne, kudhoofika kwa utawala wa sheria.

(ii) Dosari ya sheria ndogo kuwa na masharti yanayokinzana na Sheria Mama au na Sheria nyingine za nchi inaweza kukwamisha azma ya sheria mama au sheria nyingine za nchi. Hivyo, kuvuruga mfumo wa sheria za nchi.

(iii) Sheria ndogo kuwa na masharti yasiyo na uhalisia inasababisha mkanganyiko katika utekelezaji wa masharti hayo. Hali hiyo inaweza kuwa ni chanzo cha kukwamisha malengo ya sheria mama pia uwezekano wa mazalia ya kero kwa wananchi.

(iv) Dosari ya sheria ndogo kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria inaathiri ubora wa sheria kwenye ufasaha, usahihi, ukamilifu na kueleweka. Hivyo, kuwa na madhara wakati wa utekelezaji, jambo ambalo halikuwa lengo la Bunge wakati wa kukasimu madaraka yake.

(v) Dosari za uandishi wa majedwali katika sheria inaweza kusababisha sheria iliyoandikwa isieleweke ipasavyo kutokana na kukosekana kwa ufafanuzi uliokusudiwa kwenye Jedwali. Hivyo, kukwamisha utekelezaji wa baadhi ya masharti ya sheria ndogo na sheria mama.

(vi) Kutokamilisha utekelezaji kwa maazimio ya Bunge kuhusu marekebisho ya sheria ndogo kunachelewesha ufafanuzi na utatuzi wa kero za wananchi. Hivyo, Bunge ambalo ni mamlaka kuu ya utungaji wa sheria, halipaswi kuruhusu ucheleweshaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo: Kwa msingi wa maoni ya Kamati yanayotokana na shughuli za uchambuzi wa sheria ndogo na uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, Kamati inapendekeza mambo saba (7) kwa mfumo wa hoja Bungeni kama inavyoelekeza Kanuni ya 61 ya Kanuni za Bunge. Mambo hayo ni kama ifuatavyo: -

(i) Sheria Ndogo kuwa na masharti yanayokinzana na masharti ya Katiba

KWA KUWA dosari ya Sheria Ndogo ya kukinzana na masharti ya Katiba, kama ilivyobainika kwenye Sheria Ndogo zilizochambuliwa ikiwemo Sheria Ndogo ya (Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 ni ukiukwaji wa masharti ya Ibara ya 64(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

NA KWA KUWA Ibara ya 64(5) ya Katiba inakataza sheria yoyote zikiwemo sheria ndogo kukinzana na masharti ya Katiba,

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga sheria ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi kama ilivyooneshwa kwenye Kiambatisho Na.1 cha taarifa hii, zirekebishe dosari za sheria ndogo zinazohusika.

(ii) Dosari ya kuwa na masharti yanayokinzana na Masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

KWA KUWA dosari ya sheria ndogo kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, kama ilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2023 inaweza:-

(i) Kukwamisha azma ya sheria mama au sheria nyingine za nchi;

(ii) Kuvuruga mfumo wa sheria za nchi, jambo ambalo halipaswi kuruhusiwa na Bunge; na

NA KWA KUWA matokeo ya dosari hizo yanakwamisha azma ya Bunge kutunga sheria mama na kukasimu sehemu ya madaraka yake kwa mamlaka nyingine serikalini ili kufanya ufafanuzi wa sheria mama kwa namna inayotekelezeka kwa urahisi na kiufundi,

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga sheria ndogo zenye kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi kama ilivyobainishwa katika Kiambatisho Na.1 cha Taarifa hii, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hiyo.

(iii) Dosari ya kuweka Masharti yasiyo na Uhalisia.

KWA KUWA dosari ya sheria ndogo kuwa na masharti yasiyo na uhalisia kama ilivyoonekana katika sheria ndogo zilizochambuliwa ikiwemo Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, 2024; na

NA KWA KUWA dosari hiyo inaweza: -

(i) Kukwamisha utekelezaji wa sheria ndogo yenyewe;

(ii) Kukwamisha utekelezaji wa masharti ya sheria mama; na

(iii) Kuwa chanzo cha kero miongoni mwa wananchi.

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na dosari ya kuweka masharti yasiyo na uhalisia kama ilivyooneshwa kwenye Kiambatisho Na.1, zirekebishe dosari hiyo ili kufikia malengo yoliyokusudiwa.

(iv) Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria.

KWA KUWA dosari ya sheria ndogo kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria, kama ilivyobainika kwenye sheria ndogo zilizochambuliwa ikiwemo *Regulations under The Atomic Energy (Protection from Ionizing and Non-Ionizing Radiation), 2023 (TS Na. 840/ 17 Novemba, 2023),* inaathiri ubora wa sheria kwenye ufasaha, usahihi, ukamilifu na kueleweka kwake; na

NA KWA KUWA athari hizo mbaya kwenye sheria: -

(i) Zinaathiri azma ya Bunge kufanikisha utekelezaji wa hatua za serikali kisera kupitia sheria za Bunge na sheria ndogo;

(ii) zinakwamisha nia ya Bunge kuwezesha sheria kueleweka kwa urahisi miongoni mwa watekelezaji wa sheria au wanaoguswa na masharti ya sheria inayohusika; na

(iii) Zinaonesha ukiukaji wa misingi isiyopaswa kukiukwa na Bunge lenyewe ambalo ndilo mamlaka kuu ya utungaji wa sheria.

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria kama ilivyooneshwa kwenye Kiambatisho Na.1, zirekebishe dosari hizo ili kuleta tija iliyokusudiwa.

(v) Dosari za Uandishi wa Majedwali.

KWA KUWA dosari za uandishi wa majedwali katika sheria ndogo kama ilivyobainika kwenye uchambuzi unaoripotiwa na kuoneshwa kwenye Jedwali Na.1 la Taarifa hii ikiwemo Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 inaweza kukwamisha kueleweka kwa sheria,

NA KWA KUWA mkwamo huo unaotokana na dosari za uandishi wa majedwali unaweza kusababisha:-

(i) Changamoto katika utekelezaji wa sheria ndogo inayohusika, jambo ambalo halikuwa lengo la Bunge kukasimu madaraka yake ya kutunga sheria kwa mamlaka nyingine; na

(ii) Kufifia kwa madhumuni ya Bunge kutunga sheria inayotekelezwa ikitegemea ufafanuzi unaopaswa kutolewa na sheria ndogo.

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zilibainika kuwa na majedwali yenye

dosari za kiuandishi kama inavyobainishwa kwenye Kiambatisho Na. 01, zifanye marekebisho ili kuepusha madhara ya dosari hizo.

(vi) Kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio kuhusu Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na Dosari.

KWA KUWA dosari zote zilizobainika katika uchambuzi kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Uchambuzi, ambalo ni Kiambatisho Na.1 zinahitaji kurekebishwa inavyostahili;

NA KWA KUWA kutokurekebishwa kwa dosari zilizobainika kutokana na uchambuzi ni jambo ambalo: -

(i) Linakiuka misingi ya sheria za nchi na kuathiri tija na ufanisi katika utekelezaji;

(ii) Litaendeleza madhara ya dosari hizo katika mfumo wa sheria za nchi; na

(iii) Halistahili kuachwa na Bunge liendelee kuwepo kwa kuwa mamlaka yenye dhima na uzuri au ubaya wa sheria za nchi ni Bunge.

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zote zinazohusika na sheria ndogo zenye dosari kama zilivyotajwa katika Kiambatisho Na.1 cha Taarifa hii, ziwasilishe Taarifa ya utekelezaji wa maazimio yote kuhusu dosari za sheria ndogo kwa Katibu wa Bunge ifikapo saa 9.30 ya tarehe 20 Disemba, 2024.

(vii) Kutokamilika kwa Utekelezaji wa Maazimio ya Kurekebisha Sheria Ndogo.

KWA KUWA maazimio ya Bunge yaliyohusu kurekebisha dosari ishirini na tisa (29) katika sheria ndogo, yalilenga kuondoa madhara

ya dosari hizo, ikiwemo uwezekano wa kusababisha kero kwa wananchi;

NA KWA KUWA kutokamilisha maazimio ya Bunge yanayolenga kuondoa dosari za sheria ndogo ni jambo ambalo:-

(i) Linachelewesha utatuzi wa kero za wananchi wanaolitegemea Bunge kusimamia maslahi yao.

(ii) Halizingatii dhima ya Bunge katika sheria za nchi likihusika kwa sheria mbaya au nzuri nchini,

KWA HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka ambazo hazijakamilisha utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, zikamilishe mchakato wa marekebisho na kwamba, ifikapo saa 9.30 ya tarehe 27 Septemba, 2024, ziwe zimewasilisha kwa Katibu wa Bunge, taarifa za utekelezaji wake zenye ushahidi wa kurekebishwa kwa dosari zilizobainika katika sheria ndogo zinazohusika.

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti kengele ya pili hiyo, maliza mapema.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia.

Mheshimiwa Spika, Shukurani; napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuweka utaratibu wa taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Vikao vya Bunge. Kwa namna ya pekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua sheria ndogo na taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru Mheshimiwa William Vanging'embe Lukuvi, Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa uratibu wake uliowezesha mawasiliano mazuri kati Wizara na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja; sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano pamoja na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KWENYE MKUTANO WA KUMI NA NNE NA MKUTANO WA KUMI NA TANO, PAMOJA NA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE KUHUSU SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KWENYE MKUTANO WA KUMI NA MBILI NA MKUTANO WA KUMI NA TATU KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo naomba kuwasilisha Taarifa ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowekwa mezani wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge. Taarifa hii inajumuisha uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu

sheria ndogo zilizowekwa Mezani wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kuona umuhimu wa kuiweka Taarifa hii kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge (Order paper) ya leo, kwa mamlaka uliyonayo kwa mujibu wa Kifungu cha 10 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Bila shaka uamuzi huu umetokana na uongozi wako mahiri na azma yako madhubuti ya kuliwezesha Bunge kutimiza wajibu wake wa kusimamia misingi ya kidemokrasia kupitia usimamizi wa madaraka ya kuweka na Sheria Ndogo katika mfumo wa Sheria. Bunge ambalo ni chombo muhimu cha kidemokrasia linajivunia uongozi wako adhimu hususani katika kusimamia madaraka maalumu ya Bunge yanayohusu sheria za nchi.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 42 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hivyo, unaendana na matarajio ya Bunge kwa Kamati ili liweze kutekeleza madaraka yake ipasavyo. Kwa madhumuni ya kurahisisha mtiririko na ufuatiliaji, naomba kutambulisha sehemu hizo za Taarifa hii ambayo imegawanyika katika sehemu kuu tatu na ya nne ni kutoa hoja na shukurani. Sehemu hizo ni ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inayohusu utangulizi inaonesha maelezo ya jumla kuhusu taarifa yenyewe, lengo la Kamati kuripoti Bungeni, mantiki ya Bunge kufuatilia Sheria Ndogo na mambo mengine ya jumla kuhusu Taarifa ya Kamati;

(ii) Sehemu ya Pili inayohusu uchambuzi inabainisha shughuli za uchambuzi na misingi yake pamoja na matokeo ya

uchambuzi. Katika sehemu hii sheria ndogo zilizochambuliwa na vigezo vya uchambuzi ni mambo yanayofafanuliwa.

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni ya Kamati kuhusu Matokeo ya Uchambuzi pamoja na kutoa Mapendekezo ili Bunge likiyapitisha yawe maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, muundo huo utawezesha wafuatiliaji kubaini mzizi wa mapendekezo na muktadha wake. Waheshimiwa Wabunge wataona dhahiri kila pendekezo linavyofaa kuungwa mkono kwa lengo la kufanikisha dhima ya Bunge kuwa na sheria bora za nchi.

### 1.3 Lengo la Kamati Kuripoti Bungeni kuhusu Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kama ilivyo kwa Kamati nyingine za Bunge, inafanya kazi kwa niaba ya Bunge na kwa kutumwa na Bunge. Matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo na uamuzi stahiki kwa matokeo hayo ni stahili ya Bunge kuamua kwa njia ya maazimio. Ili kufanikisha jambo hilo, taarifa hii inalenga kuliwezesha Bunge lifanikiwe katika mambo yafuatayo: -

(i) Kupata tathmini ya jumla na ya kina inayochangiwa na Wabunge kwa ujumla ili kuwa na uelewa na msimamo wa pamoja kuhusu madaraka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali za kiutendaji;

(ii) Kuwezesha ulingo (*forum*) muhimu unaoruhusu mitazamo tofauti (*diverse perspectives*) ya Wabunge ili nchi iwe na Sheria zinazokidhi matarajio ya wananchi;

(iii) Kujenga makubaliano ndani ya Bunge kuhusu hatua stahiki kulingana na uhalisia wa sheria ndogo zilizofanyiwa uchambuzi;

(iv) Kutumia mchakato wa kidemokrasia na kuwezesha uwazi kwa njia ya mjadala Bungeni unaotoa nafasi kwa Wabunge kuongeza maoni yao katika matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo;

(v) Kuzingatia dhana ya uwajibikaji kwa umma (*Public Accountability*) kwa kuuwezesha Umma kufuatilia kiwango cha umakini unaojitokeza kwenye uchambuzi wa sheria ndogo zinazogusa moja kwa moja maisha ya wananchi; na

(vi) Kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa mapendekezo yanayolenga kuondosha dosari za sheria ndogo, kutokana na uchangiaji wa Wabunge unaoongezea ufafanuzi kwa watekelezaji.

### 1.4 Sababu za Bunge Kufuatilia Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika**, kama sote tunavyofahamu, Bunge ndilo lenye mamlaka ya kutunga Sheria zote za nchi. Hivyo, ubaya au uzuri wa sheria za nchi unabebwa na Bunge. Iwe sheria mama au sheria Ndogo, matokeo yake kwa maisha ya watu ni dhima ya Bunge. Aidha, Ibara 8 (1) (a) inasisitiza kuwa wananchi ndio msingi wa mamlaka yote.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano imeelekeza lengo kuu la Serikali ambalo ni ustawi wa watu. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linapaswa kuhakikisha kuwa sheria ndogo zote kama ilivyo kwa Sheria za Bunge, haziweki ugumu wa kupata maisha bora wala

hazizalishi kero kwa wananchi ambao ni msingi wa mamlaka yote ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo, Bunge kupitia Kamati yake ya Sheria Ndogo linafuatilia sheria ndogo kwa sababu kuu zifuatazo: -

(i) Kudumisha ukuu wa watu (*People's sovereignity*) kwa kuhakikisha kwamba, mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kuweka sheria ndogo hazizidi mamlaka ya utungaji sheria yaliyotolewa na watu kwa wawakilishi wao (Bunge);

(ii) Kuhakikisha kwamba, madaraka ya kuweka sheria ndogo katika mfumo wa sheria za nchi, yaliyokasimiwa na Bunge kwa mamlaka mbalimbali hayavunji haki za watu na wala hayavuki mipaka;

(iii) Kuzuia masuala ya kiufundi na utaalamu yasivuke mipaka na kuathiri maisha ya watu au kuvuruga haki na usawa miongoni mwa watu; na

(iv) Kuhakikisha kwamba Sheria zinazotokana na Bunge kukasimu madaraka yake, zinaakisi maslahi ya umma kwa upana wake, maadili ya jamii pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya ustawi wa watu.

**Mheshimiwa Spika**, katika muktadha huo, Bunge hili linatarajiwa kujadili ipasavyo Taarifa hii na kutoa maazimio yanayolenga kuondosha dosari zilizobainika katika sheria ndogo. Kwa msingi huo, Kamati imefanya uchambuzi wa kina, imekuwa makini na imeweka wazi matokeo ya uchambuzi katika Jedwali la kwanza ambalo ni **Kiambatisho Na. 01** na Jedwali la pili la matokeo ya uchambuzi wa utekelezaji wa maazimio ya Bunge ambalo ni

**Kiambatisho Na. 02.** Majedwali yote hayo ni sehemu ya Taarifa hii na yameambatishwa.

### 1.5 Mbinu Zilizotumika Kupata Matokeo

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua umuhimu wa mbinu inayotumiwa na Kamati, Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, imeweka masharti kwamba, kila Taarifa inayowasilishwa Bungeni itabainisha njia iliyotumika. Kwa kawaida, njia iliyotumika inapobainishwa kwenye taarifa ya Kamati Bungeni, inasaidia mambo yafuatayo: -

(i) Kuweka wazi muktadha wa matokeo ya uchambuzi na hivyo kujenga msingi wa uhalali wa matokeo yanayowasilishwa Bungeni;

(ii) Kuweka uwazi wa vigezo na mchakato uliotumika na hivyo kulisaidia Bunge tathmini ya uhalali wa mapendekezo yanayotolewa;

(iii) Kuwezesha tathmini ya ubora wa matokeo yanayoripotiwa Bungeni kulingana na ubora wa njia na hivyo kuwezesha tathmini ya msingi wa mapendekezo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla kuonesha njia katika Taarifa za Kamati ni jambo linawezesha Bunge kujiridhisha na kiwango cha kazi iliyofanywa na Kamati. Kwa mantiki hiyo, naomba kubainisha mbinu zilizotumika ambazo ni:-

(i) Kupitia Magazeti ya Serikali yaliyotangaza sheria ndogo na kuwekwa mezani Bungeni;

(ii) Kubainisha sheria ndogo zinazofaa kujadiliwa kwa kipaumbele na kufanya mapitio ya sheria ndogo hizo;

(iii) Kubainisha sheria ndogo zenye hoja za kiuchambuzi na kuzipitia kwa undani ili kufanya tathmini kwa umakini Zaidi;

(iv) Kusoma matini (*text*) ya sheria ndogo na matini ya sheria mama kwa lengo la kuoanisha masharti ya kisheria;

(v) Kuchunguza dhamira ya sheria mama ili kujiridhisha iwapo sheria ndogo zinaendana na nia ya Bunge;

(vi) Kutafakari dhamira ya sheria ndogo inayohusika kwa kulinganisha na nia ya Bunge kukasimu madaraka yake kwa mamlaka inayohusika;

(vii) Kutathmini sheria ndogo kwa muono wa miongozo ya uandishi wa sheria iliyotolewa katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1; na

(viii) Kufungamanisha Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba inayobainisha lengo kuu la Serikali kwa upande mmoja na maudhui, dhamira na masharti ya Sheria Ndogo kwa upande mwingine ili kutathmini kwa vigezo vya uchambuzi.

**Mheshimiwa Spika**, nilithibitishie Bunge lako tukufu kuwa matumizi ya mbinu hizo, yamefanikisha matokeo ya uchambuzi. Naamini Bunge likijadili ipasavyo, uchambuzi uliofanyika utakuwa na tija kwa maisha ya Watanzania. Naomba kusisitiza kwamba, Wabunge na wananchi tukumbuke vizuri kuwa, sheria ndogo zilizochambuliwa na matokeo yake kuripotiwa, kwa sehemu kubwa zinagusa maisha ya kawaida na ya kila siku ya wananchi. Hivyo, ni muhimu kufuatiliwa kwa umakini.

### 1.6 Majumuisho ya Sehemu ya Kwanza

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yanayotolewa katika sehemu ya kwanza yanaweka muktadha wa Taarifa. Katika maelezo hayo muundo wa taarifa na msingi wake umebainishwa ili kuonesha mtiririko wa maudhui. Aidha, lengo la Kamati kuripoti Bungeni limewekwa bayana ili kuwezesha ufuatiliaji wa mambo makuu katika taarifa. Vilevile, sababu za Bunge kufuatilia sheria ndogo zimedhihirishwa ili kuonesha mantiki ya taarifa. Zaidi ya hivyo, sababu za Bunge kufuatilia sheria ndogo zimebainishwa ili kushajiisha mjadala wa taarifa hii. Pia zimeelezwa mbinu zilizotumika kwa lengo la kuwezesha tathimini ya matokeo yanayoripotiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla jambo kuu la kuondoka nalo katika sehemu hii ni madhumuni ya taarifa ya Kamati Bungeni. Imeelezwa kwamba, Bunge ndilo lenye mamlaka ya kutunga sheria na ni chombo cha uwakilishi wa Wananchi. Hivyo, linategemewa kuhakikisha kuwa sheria zote za nchi zinawezesha ustawi wa maisha yao kuliko kuwa kero kwao. Aidha, Bunge kwa utaratibu wake linategemea matokeo ya kazi ya Kamati hii kuona kuwa kuna taratibu bora za utekelezaji wa sheria. Jambo lingine muhimu ni kuzingatia dhima ya Bunge ambayo inaliweka Bunge kwenye kuhusika na ubaya au uzuri wa sheria za nchi. Ikumbukwe kuwa wananchi hawatarajii Bunge liache dosari za sheria yoyote ya nchi iwe kikwazo kwa ustawi wao.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZA UCHAMBUZI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Kamati hii inategemewa na Bunge katika azma yake ya kuhakikisha sheria za nchi zinajali ustawi

wa wananchi, Taarifa hii ni zana ya msingi kutimiza azma ya Bunge. Kwa kuwa Bunge ni mamlaka kamili ya kutunga sheria kwa mujibu wa Katiba, halipaswi kung'atuka katika utungaji wa sheria ndogo. Badala yake, Bunge linapokasimu madaraka yanayohusika, linapaswa kufuatilia kwa kuchambua sheria ndogo na kutoa maazimio kutokana na uchambuzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo inahakikisha kuwa Bunge linapokasimu sehemu ya madaraka yake ya kutunga sheria, haling'atuki. Kamati imefanya hivyo kwa shughuli zake kuu mbili zifuatazo: -

(i) Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano. Lengo ni kuhakikisha kuwa dhima ya Bunge inabaki kama ilivyo na inavyotarajiwa kusaidia nchi kuwa na sheria za nchi zinazostahili; na

(ii) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu. Lengo ni kusimamia uzingatiaji wa Madaraka ya Bunge ya kutunga sheria na kuhakikisha kuwa Bunge linayatawala madaraka hayo yasiyotakiwa kutelekezwa.

### 2.2 Msingi wa Shughuli za Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi mkuu wa shughuli za uchambuzi umejengwa kwenye Ibara ya 4 (1), Ibara ya 8 (1(a) na (1)(b) na Ibara ya 97 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, masharti na lengo la jumla la Sheria ya Taafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The interpretation of Laws Act, Cap.* 1) kwa pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge, yanazatiti umuhimu wa shughuli za uchambuzi zilizofanywa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 4 (1) ya Katiba imelipatia Bunge shughuli za mamlaka ya nchi zinazohusu kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Hivyo, katika nchi utungaji wa sheria zote upo chini ya mamlaka ya Bunge. Hata hivyo, Bunge linaruhusiwa kukabidhi kwa mtu yoyote au kwa Idara yoyote ya Serikali, madaraka ya kuweka Kanuni zenye nguvu ya kisheria au kuzipa nguvu ya kisheria Kanuni zozote zilizowekwa na mtu yoyote au Idara yoyote ya Serikali. Sheria na Kanuni kwa msingi huo, zinapaswa kuzingatia masharti ya Ibara ya 8 (1) (a) kwamba, Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na kwamba Serikali imepata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa Wananchi. Hivyo, sheria za nchi zinalazimika kuweka masharti yanayolinda na kuzingatia ipasavyo maslahi ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, ndiyo inayotoa mwongozo kuhusu uandishi wa sheria. Sheria hii ina lengo la kuzatiti sheria kwenye muundo wa uandishi. Aidha, inaweka mwongozo wa tafsiri na masharti kuhusu matumizi ya sheria zote. Hivyo, inajenga msingi wa uchambuzi ikiwemo kubainisha masharti ya sheria ndogo kuwekwa mezani Bungeni. Kwa masharti hayo, sheria hii kwa pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge ni mwongozo wa msingi katika shughuli za uchambuzi zinazofanywa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa msingi nilioueleza hapo juu, Taarifa hii inafafanua shughuli za Kamati ambazo zinahusu uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge na Uchambuzi wa Sheria Ndogo.

### 2.2.1 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo **ishirini na mbili** (22) zilizowasilishwa

Bungeni tarehe 5 Septemba, 2023, kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili na tarehe Tarehe 07 Novemba, 2023 kwenye Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge. Ufuatiliaji huo ulioambatana na upokeaji na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji, ulilenga kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa uamuzi wa Bunge kuhusu mamlaka yake ya kutunga sheria.

**Mheshimiwa Spika**, mantiki ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio inatokana na umuhimu wa Bunge kutekeleza jukumu la kutunga sheria pasi na kusahau wajibu wake kikatiba kuhusu sheria za nchi ikiwemo sheria ndogo. Nilikumbushe Bunge lako tukufu kuwa, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo hizo yaliwasilishwa Bungeni tarehe 16 Februari, 2024 kwenye Mkutano wa Kumi na Nne. Matokeo hayo yalihusu dosari mbalimbali na pia yalionesha madhara yake dhidi ya misingi ya sheria na ustawi wa watu uliosisitizwa katika Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio unalisaidia Bunge kufuatilia hatua mbalimbali zilizofikiwa ili kurekebisha dosari kwenye sheria ndogo. Kufanya hivyo ni muhimu na lazima kwa kuwa Bunge ndilo mamlaka kuu ya utungaji wa sheria za nchi. Hivyo, maoni ya Kamati kutokana na uchambuzi huo yanajenga msingi mzuri utakaowezesha mjadala na tathmini ya Bunge kuhusu namna madaraka yake yanavyotumiwa na mamlaka nyingine za serikali.

**Mheshimiwa Spika,** shughuli za uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge zilifanyika kwa hatua mbalimbali za Kamati. Hatua hizo zinaelezwa kama ifuatavyo: -

**(a) Kupokea Taarifa za Utekelezaji kabla ya kukutana na Mamlaka Zilizohusika**

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kukutana na mamlaka zilizoandaa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge, Kamati ilijiwekea

utaratibu wa kuzichambua. Nia ni kuoanisha utekelezaji ikilinganishwa na maazimio yaliyopitishwa na Bunge. Kwa mantiki hiyo, hatua hii ilisaidia katika mambo makuu mawili yafuatayo: -

(i) Kutathmini iwapo kuna mkwamo au kusuasua katika hatua mbalimbali za utekelezaji; na

(ii) Kuoanisha hatua ya utekelezaji na madhara ya dosari yaliyonusurika.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulithibitishia Bunge hili kuwa, mambo hayo mawili, yanasaidia kulionesha Bunge iwapo utekelezaji umeendana na matarajio yake. Hivyo, kuliweka Bunge katika nafasi muhimu ya kutekeleza na kusimamia madaraka yake liliyoyakasimu kwa mamlaka nyingine serikalini.

**(b) Kukutana na Mamlaka Zilizotakiwa Kutekeleza Maazimio ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kupokea taarifa za utekelezaji na kufanya mapitio ya jumla, Kamati ilikutana na mamlaka zinazohusika ili kujadiliana yaliyobainika katika taarifa hiyo. Lengo la hatua hii ni kuzingatia utaratibu mzuri wa misingi ya asili kisheria ili kufikia msimamo wa kutumainiwa juu ya jambo linalohusika. Aidha, hatua hii iliiwezesha Kamati kupata ufafanuzi wa kina kwa mbambo yaliyobainika baada ya mapitio ya taarifa.

**2.2.2 Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 2 Februari, 2024 wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Serikali iliwasilisha Mezani Bungeni matoleo ya Magazeti ya Serikali kumi na Mbili (12) yakiwa na jumla ya Sheria Ndogo **Mia moja Sabini na Tisa (179).** Aidha,

tarehe 8 Aprili, 2024 katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, Serikali iliwasilisha Mezani jumla ya Magazeti Kumi yenye jumla ya sheria ndogo **Mia Moja Sitini na Tatu (163).**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya sheria ndogo zinazohusika kuwasilishwa mezani, kwa mamlaka yako ulizileta kwenye karakana ya sheria ndogo ambayo ni Kamati hii inayoripoti leo Bungeni. Ni wazi kuwa madhumuni ya hatua yako ni kufanikisha azma ya Bunge kutunga sheria za nchi zenye misingi sahihi na madhubuti zinazolenga kuangalia maslahi mapana ya wote wanaoguswa na sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kazi kubwa iliyofanyika kwenye Kamati ikiwa ni karakana ya sheria ndogo ni kubainisha hitilafu kwenye matumizi ya madaraka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini. Shughuli hiyo ilijumuisha kuonesha dosari katika sheria ndogo na madhara yake kwa wananchi, sambamba na kupendekeza hatua stahiki ya kuchukuliwa na Bunge ili kusahihisha kasoro zilizopo.

**Mheshimiwa Spika,** kipimo kikuu kilichotumika ni masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Kamati ililenga kujiridhisha na mambo makuu matano (05) yafuatayo: -

(a) Iwapo sheria ndogo zina masharti yanayokinzana na Katiba;

(b) Iwapo sheria ndogo zina masharti yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi;

(c) Iwapo sheria ndogo zina makosa ya kutoendana na misingi ya uandishi;

(d) Iwapo sheria ndogo zina masharti yasiyo na uhalisia kwa kiasi cha kusababisha changamoto katika utekelezaji wake; na

(e) Iwapo sheria ndogo zina majedwali yenye dosari kwa:-

(i) kutofautiana na vifungu vya sheria ndogo vinavyoyaanzisha au:

(ii) kutokamilika ilivyostahili au;

(iii) kutajwa katika sheria ndogo inayohusika lakini yanakosekana; na

(iv) kujitokeza bila kuwa na kifungu cha sheria ndogo inayoyaanzisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla shughuli za Kamati zililenga maeneo makuu mawili. Eneo la kwanza ni hatua zilizofikiwa katika marekebisho ya dosari za sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na tatu. Eneo la pili ni dosari katika sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na tano.

**Mheshimiwa Spika,** maeneo yote hayo yanahusu madaraka ya Bunge kwenye sheria za nchi. Tathmini ya hatua iliyofikiwa katika maazimio ya Bunge ni muhimu ili kuhakikisha kuwa madaraka ya Bunge yametekelezwa inavyostahili. Kujiridhisha na sheria ndogo ni shughuli muhimu kwa kuwa Bunge linatarajiwa na wananchi kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakuwepo kwa namna isiyokiuka misingi muhimu ya sheria.

## 2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako linao wajibu wa kuhakikisha kwamba, madaraka yake ambayo yamekabidhiwa kwa mamlaka nyingine yanatumika inavyostahili. Wajibu huo unalitaka Bunge kutokuishia kutoa maazimio kuhusu urekebishwaji wa sheria ndogo bali pia kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake. Ili kutimiza wajibu huo ni jukumu la Bunge lenyewe kufuatilia ipasavyo namna madaraka hayo yanavyotumika. Kwa maneno mengine, Bunge halipaswi kuishia kwenye kubainisha dosari katika sheria ndogo na kuamua kwa njia ya maazimio. Kwa kawaida, Bunge linapaswa kujiridhisha iwapo dosari hizo zimerekebishwa kwa namna ilivyoazimiwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Bunge linaituma Kamati ya Sheria Ndogo kusimamia utekelezaji bora wa madaraka ya sheria ndogo yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine, Kamati hii inawajibika kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Lengo ni kuona hatua inayofikiwa na kulinganisha na hatua iliyostahili ili kulishauri Bunge uamuzi unaofaa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa sheria ndogo ni sehemu ya Sheria za nchi, dosari zinazojitokeza katika Sheria hizo, zinapaswa kufanyiwa kazi kwa utaratibu unaoendana na desturi za Bunge. Bila kufanya hivyo, madhara ya dosari zote yanavyoendelea yanaweza kuliweka Bunge kwenye kulaumiwa na wananchi. Bunge ambalo ni chombo halisi cha wananchi haliwezi kuacha kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake kuhusu dosari katika sheria ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio uliangalia hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio hayo. Uangaliaji na ufuatiliaji wa hatua hizo za utekelezaji ulidadisi mambo yafuatayo:-

(i) Iwapo hakuna kabisa utekelezaji wa maazimio;

(ii) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya Rasimu ya marekebisho katika ngazi ya Wizara;

(iii) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya Rasimu ya marekebisho kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki; na

(iv) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, udadisi ulioegemea katika vigezo hivyo, uliiwezesha Kamati kutathmini hali ya utekelezaji wa kila azimio lililotolewa na Bunge na hatimaye kupata matokeo halisi ya hatua zilizofikiwa katika utekelezaji. Matokeo hayo yataliwezesha Bunge kuamua kuhusu hatua inayofuata.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu dosari za sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, yanafaa kuripotiwa. Nia ni kuonesha hatua iliyofikiwa ili kusahihisha dosari kama ilivyoamuliwa kupitia maazimio ya Bunge. Matokeo hayo yanaonesha kwamba, hatua zilizoripotiwa za kusahihisha dosari ili kutekeleza maazimio ya Bunge, zinagawanyika katika makundi makuu yafuatayo:-

(i) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki; na

(ii) Hatua ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kufafanua hatua hizo sambamba na kubainisha Wizara tisa (09) zinazohusika. Lengo la ufafanuzi huu ni kuliwezesha Bunge kubaini kiwango cha utekelezaji wa maazimio yake na kufanya uamuzi stahiki. Ili kuweka bayana wahusika wa utekelezaji wa maazimio, naomba kubainisha Wizara zinazohusika na utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo. Wizara hizo ni:-

(i) Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji iliyokuwa na sheria ndogo **moja** (01) iliyobainika kuwa dosari **mbili** (02);

(ii) Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu iliyokuwa na sheria ndogo **mbili** (02) zilizobainika kuwa na dosari **sita** (06);

(iii) Wizara ya Kilimo iliyokuwa na sheria ndogo **moja** (01) zilizobainika kuwa dosari **kumi na sita** (16);

(iv) Wizara ya Uchukuzi iliyokuwa na sheria ndogo **sita** (06) zilizobainika kuwa dosari **thelathini** (30);

(v) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliyokuwa na sheria ndogo **mbili** (02) zilizobainika kuwa dosari **kumi na mbili** (12);

(vi) Wizara ya Maji iliyokuwa na sheria ndogo **moja** (01) iliyobainika kuwa dosari **moja** (01);

(vii) Wizara ya Nishati iliyokuwa na sheria ndogo **tatu** (03) zilizobainika kuwa dosari **ishirini na nne** (24);

(viii) Wizara ya Fedha iliyokuwa na sheria ndogo **nne** (04) zilizobainika kuwa dosari **kumi na nane** (18); na

(ix) Wizara ya Viwanda na Biashara iliyokuwa na sheria ndogo **mbili** (02) zilizobainika kuwa dosari tisa (09).

**Mheshimiwa Spika,** hali halisi ya hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge inabainishwa katika Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu, ambalo ni **Kiambatisho Na. 02**. Jedwali hilo linafafanua hatua iliyofikiwa na kila Wizara. Pamoja na hivyo, kwa madhumuni ya kuweka mtiririko huo kwa ajili ya kuwezesha majadiliano juu ya hoja hii, naomba kufafanua hatua hizo kama ifuatavyo:

(i) Maazimio ya Bunge kutokuwa yametekelezwa.

(ii) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho katika ngazi ya Wizara.

(iii) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki.

(iv) Hatua ya Marekebisho Kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yanayoripotiwa katika Taarifa hii yameonekana kuwa katika hatua mbili zilizofikiwa na Wizara na Taasisi mbalimbali katika kutekeleza Maazimio ya Bunge. Hatua hizo zinahusisha marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali na Rasimu ya Marekebisho ya sheria ndogo kuwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki ili kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Kimsingi hatua hizi ni za juu kabisa katika utekelezaji wa Maazimio Bunge na zinastahili kupongezwa, kwani Kamati ilijiridhisha kuwa hakuna Wizara au Taasisi ambayo haijaanza

kabisa utekelezaji wala kuwa katika hatua ya Rasimu ya marekebisho iliyo katika ngazi ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Bunge lako tukufu kufahamu kuhusu hatua za utekelezaji na hatimaye kufanya uamuzi sahihi kuhusu hoja zitakazoazimiwa kutokana na Taarifa hii, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu hatua zilizofikiwa.

### 2.3.1 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho Kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho ya sheria ndogo zote yanatarijwa kufikishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki kabla ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Uchambuzi umebainisha kwamba, hadi wakati Kamati ilipokutana na Wizara zinazohusika, ni **sheria ndogo tatu** (**03**) tu, zilizokuwa na hoja **ishirini na tisa** (**29**) kati ya sheria **ndogo ishirini na mbili** (**22**) zilizokuwa na hoja **thelathini na mbili (32)** zilifika hatua hii. Sheria ndogo hizo ni: -

(i) Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelekaji na Usambazaji Umeme, 2023 **(TS Na. 452 la tarehe 7 Julai 2023)** zilizo chini ya Wizara ya Nishati ambazo zilizokuwa na jumla ya hoja 16;

(ii) Kanuni za Ukusanyaji na Uchakataji wa Taarifa Binafsi,2023 **(TS Na. 349 la tarehe 12 Mei 2023)** ambazo zinasimamiwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari zikiwa na hoja sita (06); na

(iii) *The Accountants and Auditors (Training and Examinations) By Laws, 2023* **(TS Na. 486 la terehe 21 Julai 2023)** zilizo chini ya Wizara ya Fedha zenye hoja saba (07).

**Mheshimiwa Spika**, hatua iliyofikiwa inakaribia kutangazwa kwa marekebisho katika Gazeti la Serikali. Kwa maelezo yaliyowasilishwa kwenye Kamati marekebisho yatakamilika katika kipindi kifupi kijacho. Itakapofika hatua hiyo, changamoto zilizobainika na kero miongoni mwa wanaolengwa na sheria ndogo zitakuwa zimetatuliwa.

### 2.3.2 Hatua ya Marekebisho Kutangazwa katika Gazeti la Serikali

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho yoyote ya sheria ndogo hayawezi kuanza kutekelezwa kabla ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Tathmini iliyofanywa na Kamati imeonesha kwamba, hadi tarehe 23 Agosti, 2024, sheria ndogo **kumi na tisa (19)** zilikua zimefikia hatua ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Naomba kuzitambua Wizara zinazohusika na sheria ndogo hizo kama ifuatavyo:-

(a) Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji iliyotangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 83 la tarehe 9/2/2024 imefanya marekebisho ya hoja mbili (02) kupitia The *Tanzania Investment (Amendment) Regulations*, 2024;

(b) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliyotangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 407 la tarehe 24/5/2024 hoja sita (06) kwenye Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Taratibu za Kushughulikia Malalamiko ya Ukiukwaji wa Misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi za Mwaka 2024;

(c) Wizara ya Kilimo iliyotangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 344 la tarehe 3/5/2024 jumla ya hoja kumi na sita (16) kwenye *The Plant Health (Amendment) Regulations, 2024*;

(d) Wizara ya Nishati iliyotangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali sheria ndogo mbili (02) ambazo ni: -

(i) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Usuluhishi wa Migogoro Itokanayo na Shughuli za Mkondo wa Juu Wa Petroli za Mwaka 2024, iliyorekebisha kasoro tatu (03) kupitia Tangazo la Serikali Na. 643 la Tarehe 26/7/ 2024; na

(ii) *The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Internal Review Procedure) (Amendment) Rules, 2024* iliyorekebisha hoja tano (05) kupitia Tangazo la Serikali Na. 643 la Tarehe 26/7/ 2024.

(e) Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu iliyotangaza marekebisho ya sheria ndogo mbili (02) katika Gazeti la Serikali. Sheria hizo ni: -

(i) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Mazingira ya Kazi za Mwaka, 2024 iliyorekebisha hoja tatu (03) kupitia Tangazo la Serikali Na. 24 la Tarehe 16/8/2024; na

(ii) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Egonomia za Mwaka, 2024 iliyorekebisha hoja tatu (03) kupitia Tangazo la Serikali Na. 25 la Tarehe 16/8/2024.

(f) Wizara ya Viwanda na Biashara iliyotangaza marekebisho ya sheria ndogo mbili (02) katika Gazeti la Serikali. Sheria hizo ni: -

(i) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Utoaji wa Leseni za Biashara za Mwaka 2024 iliyorekebisha hoja saba

(07) kupitia Tangazo la Serikali Na. 147 la Tarehe 8/3/2024; na

(ii) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Umiliki Manufaa za Mwaka 2024 iliyorekebisha hoja mbili (02) kupitia Tangazo la Serikali Na. 148 la Tarehe 8/3/2024.

(g) Wizara ya Fedha iliyotangaza marekebisho ya sheria ndogo tatu (03) katika Gazeti la Serikali. Sheria ndogo zinazohusika ni: -

(i) *The Foreign Exchange (Bureau De Change) (Amendment) Regulations, 2024* iliyorekebisha hoja nne (04) kupitia Tangazo la Serikali Na. 417 la tarehe 31/5/2024;

(ii) *The Banking and Financial Instiotutions (Prompts Corrective Actions) (Amendment) Regulations, 2024* iliyorekebisha hoja mbili (02) kupitia Tangazo la Serikali Na. 148 la Tarehe 31/5/2024; na

(iii) *The Capital Markets and Securities Tribunal (Amendment) Rules, 2024* iliyorekebisha hoja tano (05) kupitia Tangazo la Serikali Na. 468 la tarehe 14/6/2024.

(h) Wizara ya Uchukuzi iliyotangaza marekebisho ya sheria ndogo sita (06) katika Gazeti la Serikali. Sheria hizo ni: -

(i) *The Tanzania Shipping Agencies (Cargo Security and Safety of Terminal Operations) (Amendment) Regulations, 2024* imerekebisha hoja tisa (09) kupitia Tangazo la Serikali Na. 394 la tarehe 24/5/2024;

(ii) *The Merchant Shipping (Establishment and Operation of Aids to Navigation) (Amendment) Regulations, 2024* imerekebisha hoja nne (04) kupitia Tangazo la Serikali Na. 395 la tarehe 24/5/2024;

(iii) *The Merchant Shipping (Medical Examinations) (Amendment) Regulations, 2024* imerekebisha hoja mbili (02) kupitia Tangazo la Serikali Na. 396 la tarehe 24/5/2024;

(iv) *The Tanzania Shipping Agencies (Shippers Registration) (Amendment) Regulations, 2024* imerekebisha hoja kumi (10) kupitia Tangazo la Serikali Na. 397 la tarehe 24/5/2024;

(v) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Ulinzi wa Mizigo na Usalama wa Shughuli za Kibandari za Mwaka 2024 imerekebisha hoja nne (04) kupitia Tangazo la Serikali Na. 406 la tarehe 24/5/2024; na

(vi) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Usajili wa Wasafirishaji kwa Njia ya Maji za Mwaka 2024 imerekebisha hoja moja (01) kupitia Tangazo la Serikali Na. 408 la tarehe 24/5/2024.

(i) Wizara ya Maji iliyotangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 392 la tarehe 24/5/2024 hoja moja (01) kwenye Kanuni za *The Water Supply and Sanitation (Commercial and Community Boreholes Operations) (Amendment) Rules, 2024*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hatua kuu mbili zilizofikiwa ni sehemu ya juhudi za kurekebisha dosari zilizokuwa zimejitokeza kwenye sheria ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Kumi na

Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge. Kwa juhudi hizo, ni jambo jema kuanza mchakato wa kuondoa madhara ya dosari kama ilivyoazimiwa na Bunge. Hata hivyo, ni muhimu kwa mamlaka zinazokasimiwa na Bunge madaraka ya kuweka sheria ndogo, kufanya marekebisho kwa wakati pale ambapo, chombo kikuu chenye mamlaka kuhusu sheria za nchi kinapoazimia kufanyika kwa marekebisho. Haifai kuchelewa kutekeleza maazimio ya Bunge hususan yanayolenga kurekebisha dosari katika sheria ndogo.

### 2.4 Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, yanaonesha dosari mablimbali kama inavyoenekana katika **Kiambatisho Na.1**. Naomba Jedwali hilo lisomwe kwa pamoja na taarifa hii na liingizwa kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Dosari zinazobainishwa katika Jedwali hilo zinajitokeza kwenye sheria ndogo zaidi ya moja. Kwa msingi huo, idadi ya dosari haitalingana na jumla ya idadi ya sheria ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa idadi ya Sheria ndogo kulingana na aina ya dosari unaoesha kategoria zifuatazo: -

(i) Sheria ndogo mbili (02) zina masharti yanayokinzana na Katiba;

(ii) Sheria ndogo kumi (10) zina masharti yanayokinzana na Sheria Mama na sheria nyingine za nchi;

(iii) Sheria ndogo ishirini na mbili (22) zina masharti yasiyo na uhalisia;

(iv) Sheria ndogo kumi na tatu (13) zina makosa ya kutoendana na misingi ya uandishi; na

(v) Sheria ndogo kumi na tatu (13) zina dosari katika Majedwali.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuliwezesha Bunge kufikia uamuzi unaostahili, sehemu hii inafafanua dosari zilizotajwa hapo juu kwa mifano halisi kama ilivyobainika wakati wa uchambuzi. Ufafanuzi huo ni kama ifuatavyo: -

### 2.4.1 Dosari ya Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Masharti ya Katiba

**Mheshimiwa Spika,** Nia ya sheria ndogo ni kufanikisha lengo kuu la sheria mama inayotungwa na Bunge. Aidha, sheria ndogo kama zilivyo sheria nyingine za nchi, zinatarajiwa kuendana na masharti ya Katiba ambayo ni msingi mkuu wa sheria za nchi zikiwemo sheria mama. Hata hivyo, uchambuzi unabainisha baadhi ya sheria ndogo zenye maudhui yanayotofautiana na matakwa ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa sheria ndogo zenye dosari hiyo ni **Sheria Ndogo ya (Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 (TS Na. 38/19 Januari, 2024)**. Kifungu cha 26 cha sheria ndogo hii kinataja makosa mbalimbali yanayokatazwa, ikiwemo kosa kwa mtu yeyote kufanya shughuli za kisiasa ikiwa ni pamoja na kupandisha bendera ya Chama cha Siasa. Katazo hilo limewekwa pasipo kufafanua maeneo yanayoguswa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna katazo hilo lilivyowekwa, inaweza kutafsirika kwamba, watu wote wanakatazwa kufanya shughuli za kisiasa, jambo ambalo ni kinyume cha Katiba ya Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania. Aidha, sheria ndogo kuwa na masharti yasiyoendana na Katiba kama ilivyo kwa sheria ndogo hii, ni dosari kubwa katika sheria za nchi. Madhara yake ni pamoja na sheria inayohusika kutokuwa halali, kukiuka misingi ya utawala wa shera na kuathiri vibaya masharti ya misingi ya demokrasia nchini. Njia pekee ya kusahihisha dosari hiyo ni kuirekebisha sheria ndogo iliyobainika kuwa na dosari.

### 2.4.2 Dosari ya Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi

**Mheshimiwa Spika,** Kama tunavyofahamu, sheria ndogo zinatokana na mamlaka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa sheria mama iliyotungwa na Bunge. Hivyo, katika hali ya kawaida sheria ndogo hazitarajiwi kukiuka masharti ya sheria ambayo inaipa nguvu. Kwa msingi huo, ikiwa sheria ndogo yoyote itakuwa na maudhui yanayokinzana na yale ya sheria mama, itakuwa imejipa nguvu isiyotokana na ithibati ya mamlaka yoyote.

**Mheshimiwa Spika,** zaidi ya maelezo hayo, uandishi wa sheria za nchi ni zao la misingi iliyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Tafsiri ya Sheria. Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinakataza sheria ndogo kukinzana na sheria mama au sheria nyingine ya nchi. Vilevile, kifungu hicho kinabatilisha sheria ndogo inayokinzana na masharti ya sheria mama au ya sheria nyingine ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya masharti hayo ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, uchambuzi umeonesha kuwa, zipo sheria ndogo zilizochambuliwa ambazo zina dosari ya kukinzana na sheria mama. Mfano wa sheria ndogo hizo ni **Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2023 (TS Na. 920 22 Disemba, 2023).** Kifungu cha 16 (e) cha sheria ndogo hii kinaweka katazo kwa mtu yeyote aliye ndani ya gari kudondosha taka ngumu nje ya gari

likiwa ndani au nje ya kituo cha magari na sehemu yoyote ile ambapo gari hilo linapita.

**Mheshimiwa Spika,** sheria ndogo hii imekataza utupaji wa taka ngumu peke yake bila kujumuisha taka laini na nyinginezo. Kutokutajwa kwa taka laini na nyinginezo kunaweza kutafsirika kuwa ni ruhusu ya kutupa taka hizo. Tafsiri hiyo, inaathiri vibaya lengo la sheria ndogo na utekelezaji wa Sheria ya Bunge ambayo ni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, hususan kufikiwa kwa lengo la kuweka mazingira kwenye hali ya usafi na usalama.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mwingine wa sheria ndogo iliyobainika kuweka masharti yanayokinzana na sheria nyingine za nchi ni **Sheria Ndogo ya Usafi, Afya na Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, 2023 (TS Na. 921/22 Disemba, 2023)**. Kifungu cha 3 cha sheria ndogo hii kinatafsiri maneno mbalimbali yaliyotumika katika sheria ndogo ikiwemo kifungu cha maneno "**taka ngumu**. Tafsiri hiyo inatofautiana na tafsiri ya "**taka ngumu** katika Kifungu cha 3 Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Kwa kufanya hivyo, sheria ndogo inakinzana na sheria mama inayoweka utaratibu wa usimamizi wa mazingira nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge linapokabidhi kwa mamlaka za serikali madaraka ya kuweka sheria ndogo au kanuni, halikusudii kuruhusu mamlaka hizo zitunge sheria ndogo zinazokinzana na masharti yanayowekwa na sheria ya Bunge. Kwa mantiki hiyo, sheria ndogo zote zenye masharti yanayokinzana na masharti yaliyowekwa na sheria za Bunge, zinakuwa ni batili kwa kiwango zinavyokinzana na sheria mama kama inavyoelekezwa na Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

### 2.4.3 Dosari ya kuweka Masharti yasiyo na Uhalisia

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na masuala mengine, uandishi wa sheria hulenga kuweka masharti mbalimbali ambayo zao la utekelezaji wake ni kushughulikia, kufanikisha au kutatua jambo fulani miongoni mwa wanaolengwa na masharti yanayohusika.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya uchambuzi wa Kamati yanabainisha masharti yaliyowekwa na sheria ndogo ambayo utekelezaji wake hauna uhalisia ikilinganishwa na lengo la sheria ndogo. Dosari hiyo imebainika katika **Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, 2024 (TS Na. 30 la 12 Januari, 2024).**

**Mheshimiwa Spika,** dosari ya kukosa uhalisia ilibainika katika **Kifungu cha 7** kinachohusu udhibiti wa kelele kwa shughuli mbalimbali za kijamii. Kamati ilibaini Kifungu kimeweka sharti kwa mtu yeyote anayetaka kutumia kangavuke kupata kibali cha Halmashauri pasipo kuonesha muda wa kibali hicho kutumika kama ni kwa siku, wiki, mwezi, mwaka au kipindi cha muda wa kutumia Kangavuke na mazingira yanayosababisha kuomba kutumia kangavuke.

Uwekaji masharti hayo unaleta mkanganyiko miongoni mwa wasimamizi na walengwa wa kifungu hicho na hivyo kutokidhi dhima ya kufafanua utekelezaji wa sheria mama na sheria nyingine za nchi.

**Mheshimiwa Spika, aidha dosari nyingine ya kukosa uhalisia inatokana na kifungu kuweka sharti la** kupata kibali cha Halmashauri kwa kitu kingine chochote pasipo kubainisha kitu kinachohusika. Masharti hayo yamewekwa bila kuwa na mipaka ya mambo hayo, jambo linaloweza kugusa upana mkubwa usiokusudiwa na sheria ndogo hii au kutoka nje ya wigo wa mambo

yaliyokusudiwa au kutafsiriwa hadi kwenye mambo mengine yanayowekewa utaratibu na sheria nyingine ikasababisha ukinzani au mkanganyiko.

### 2.4.4 Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya misingi ya uandishi wa sheria ni kuwezesha sheria za nchi kufanikisha hatua za serikali kisera na kisheria ili kueleweka kwa urahisi miongoni mwa watu au wananchi wanaoguswa pamoja na wanaosimamia au wenye jukumu la kuzitafsiri. Bunge linapotunga sheria huzingatia misingi ya uandishi ambayo huwezesha mawazo ghafi kuwekwa katika ukamilifu unaoeleweka na wenye maana halisi kiutekelezaji. Kazi nzuri ya Mwandishi Mkuu wa Sheria Nchini inaliwezesha Bunge kuzingatia misingi ya uandishi wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,** iwapo Bunge ambalo ndilo lenye mamlaka kamili ya utungaji wa sheria huzingatia misingi ya uandishi, sheria ndogo zinatokana na sheria za Bunge nazo zinapaswa kuandikwa kwa kuzingatia misingi thabiti ya uandishi wa sheria. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha kwamba, zipo sheria ndogo zenye dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria. Athari za dosari hiyo, ni sheria ndogo kutokueleweka vizuri na kukosa uhakika wa masharti yake kioutekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa Sheria Ndogo zenye dosari hiyo ni ***Regulations under The Atomic Energy (Protection from Ionizing and Non-Ionizing Radiation), 2023 (****TS* ***Na. 840/ 17 Novemba, 2023)***. Tatizo la uandishi lilibainika katika Kanuni ya 8(1), ambayo inaweka masharti kwamba, mtu yeyote anayekusudia kufanya jambo lililotajwa bayana katika Kanuni hizi, atalazimika kuitaarifu Tume kwa namna ilivyoelekezwa na Tume. Isivyo bahati, Kanuni hazina maelezo yanayoweka utaratibu unaostahili kufuatwa katika kutekeleza masharti ya kuitaarifu Tume kuhusu kusudio la kufanya

jambo lililobainishwa kwenye kanuni hizi. Kwa matiki hiyo dosari hiyo ya kiuandishi inasababisha kasoro ya ukamilifu wa sheria ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, ikiwa Bunge lako tukufu litafumbia macho dosari za uandishi zinazobainika kuwepo katika sheria ndogo, upo uwezekano wa dosari hizo kukwamisha utekelezaji mzuri wa sheria zinazotungwa na Bunge. Hivyo, Bunge halipaswi kuruhusu madaraka yake ya kuweka kanuni yatumike kuwezesha sheria ndogo zisozozingatia misingi thabiti ya uandishi wa sheria.

### 2.4.5 Dosari za Uandishi wa Majedwali

**Mheshimiwa Spika,** kwa kawaida majedwali katika sheria yoyote hulenga kutoa ufafanuzi zaidi na kutimiza malengo ya kifungu cha sheria kinachohusika. Kwa minajili hiyo, Jedwali sheria likiwa na dosari kwenye uandishi wake, linaweza kukwamisha ufafanuzi uliokusudiwa na hatimaye kukwamisha lengo la sheria inayohusika. Matokeo ya uchambuzi yanabainisha sheria ndogo zenye dosari ya uandishi wa majedwali.

**Mheshimiwa Spika,** dosari hizo ni pamoja na kutorejea vifungu sahihi vinavyoyaanzisha na jedwali, kutokamilika katika maudhui ya Jedwali au Jedwali kuwa na maudhui yanayokanganya. Mfano wa sheria ndogo zenye dosari za uandishi wa majedwali ni **Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 (TS Na. 39/19 Januari, 2024)**.

**Mheshimiwa Spika**, Jedwali la Kwanza linalohusu utozaji wa ada au ushuru kwa ajili ya huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri limebainika kuandikwa kwa namna inayoacha utata. Sehemu ya Kwanza ya Jedwali hilo inaweka ada ya vibali vya burudani ya kandanda kwa viwango vya shilingi 1,000/= kwa mtu mzima, na shilingi 500/= kwa mtoto, pasipo kuonesha namna ya utozaji wake. Uandishi huo unaacha utata kuhusu burudani

inayohusika kwenye ada inayotajwa. Ufafanuzi hauoneshi iwapo ada ya vibali ni kwa burudani ya viwanjani au kwa vibanda vya kuonesha kandanda. Hali hii inaweza kuleta utata na kutokueleweka kwa sheria ndogo hizi.

**Mheshimiwa Spika**, dosari ya kutoainishwa kwa namna ya utozaji wa ushuru inaweza kuwa ni chanzo cha utozaji holela na kwa kuzingatia utashi, hivyo kuathiri malengo ya ukusanyaji wa ushuru yaliyokusudiwa na sheria ndogo. Jambo hilo haliendani na nia ya Bunge. Kamwe Bunge haliwezi kukasimu madaraka yake kwa lengo la kuweka utata katika sheria za nchi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, kipimo kikuu kilichotumika ambacho kinagusa masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi, kimesaidia kubaini jumla ya sheria ndogo thelathini na nane (38) zenye dosari za namna kuu **nne** kama ilivyobainishwa kwenye **Kiambatisho Na. 01**. Mifano ya sheria ndogo hizo imetajwa ambapo sheria ndogo tano zimejitokeza kwenye mifano hiyo. Jambo muhimu kwa Bunge ni kuazimia kufanyika kwa marekebisho ili kuepuka madhara ya dosari hizo katika mfumo wa sheria na kwa maisha ya wananchi wanaowakilishwa Bungeni.

### 2.5 Majumuisho ya Sehemu ya Pili

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yote katika sehemu ya pili yanajengwa katika msingi wa masharti ya Katiba, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 na Kanuni za Bunge. Misingi hiyo imetaka uchambuzi wa sheria ndogo ufanyike kwa kuwa mamlaka ya kuweka sheria za nchi ni Bunge, na kwamba, wananchi wanaowakilishwa Bungeni wanastahili kuwa na ustawi unaowekewa masharti na sheria. Kwa maelezo hayo ruhusa ya Bunge kukasimu madaraka haina maana kwamba Bunge linaruhusiwa kung'atuka katika madaraka ya kuweka sheria za nchi. Hivyo, Bunge linawajibika kufuatilia sheria zilizotungwa kutokana na madaraka ya

Bunge kukasimiwa kwenye mamlaka nyingine. Kutokufuatia au kutojishughulisha na namna sheria ndogo zilizotungwa zinawaathiri wananchi, ni kutelekeza madaraka ya kutunga sheria. Bunge hili haliwezi kufanya kosa hilo.

**Mheshimiwa Spika,** ni wajibu wa mamlaka ya utendaji kuzingatia maazimio ya Bunge hususan maazimio kuhusu dosari za sheria ndogo. Dosari katika heria ndogo zisiporekebishwa, athari yake itaendelea kuwa mbaya kwenye dhima ya sheria za nchi na kwamba zitakwamisha azma ya Serikali na Lengo la Bunge. Aidha, hatua za utekelezaji wa maazimio ya Bunge zisizotimia zimeoneshwa na kwa kweli si hali inayofaa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa katika sehemu ya kwanza na sehemu ya Pili, Bunge ndicho chombo chenye mamlaka kamili ya kuiweka sheria ndogo na kwamba lina dhima kwa sheria za nchi. Uzuri au ubaya wa sheria za nchi ni dhima ya Bunge. Ziwe ni sheria mama, sheria nyingine za Bunge au sheria ndogo, dosari zake zisiporekebishwa, Bunge linaendelea kuwa na dhima kwa uzuri au ubaya wake. Kwa msingi huo, Kamati ina maoni na mapendekezo kutokana na matokeo ya Uchambuzi yanayobainishwa kwenye **Kiambatisho Na. 01** na **Kiambatisho Na. 02.** Maoni na mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo –

### 3.2 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa sheria ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya wananchi katika utekelezaji wake, ninaliomba

Bunge lako lipokee mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii na kuyafanyia kazi. Kwa madhumuni hayo, naomba kudhihirisha mtazamo wa Kamati unaotokana na uchambuzi kama ifuatavyo: -

(i) Dosari ya Sheria Ndogo kukinzana na masharti ya Katiba inaathiri uthabiti wa mfumo wa sheria za nchi. Hivyo, kuwa na madhara wakati wa utekelezaji, kama vile ukiukaji wa haki za kimsingi na uhuru unaohakikishwa na katiba, matumizi mabaya ya mamlaka, ukiukwaji wa uhuru wa raia na kudhoofika kwa utawala wa sheria.

(ii) Dosari ya sheria ndogo kuwa na masharti yanayokinzana na Sheria Mama au na Sheria nyingine za nchi inaweza kukwamisha azma ya sheria mama au sheria nyingine za Bunge. Hivyo, kuvuruga mfumo wa sheria za nchi, jambo ambalo halipaswi kuruhusiwa na Bunge.

(iii) Sheria ndogo kuwa na masharti yasiyo na uhalisia inasababisha mkanganyiko katika utekelezaji wa masharti hayo. Hali hiyo inaweza kuwa ni chanzo cha kukwamisha malengo ya sheria mama pia uwezekano wa mazalia ya kero kwa Wananchi.

(iv) Dosari ya sheria ndogo kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria inaathiri ubora wa sheria kwenye ufasaha, usahihi, ukamilifu na kueleweka. Hivyo, kuwa na madhara wakati wa utekelezaji, jambo ambalo halikuwa lengo la Bunge wakati wa kukasimu madaraka yake.

(v) Dosari za uandishi wa majedwali katika sheria inaweza kusababisha sheria iliyoandikwa isieleweke ipasavyo kutokana na kukosekana kwa ufafanuzi uliokusudiwa kwenye Jedwali. Hivyo, kukwamisha utekelezaji wa baadhi ya masharti ya sheria ndogo na sheria mama.

(vi) Kutokamilisha utekelezaji kwa maazimio ya Bunge kuhusu marekebisho ya sheria ndogo kunachelewesha utatuzi wa kero za wananchi. Hivyo, Bunge ambalo ni mamlaka kuu ya utungaji wa sheria, halipaswi kuruhusu ucheleweshaji huo.

### 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi wa maoni ya Kamati yanayotokana na shughuli za **uchambuzi wa sheria ndogo** na **uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge**, Kamati inapendekeza mambo saba (07) kwa mfumo wa hoja Bungeni kama inavyoelekeza Kanuni ya 61 ya Kanuni za Bunge. Mambo hayo saba na mapendekezo yanayoyahusu ni kama ifuatavyo: -

#### 3.3.1 Sheria Ndogo kuwa na Masharti yanayokinzana na Masharti ya Katiba

**KWA KUWA**, dosari ya Sheria Ndogo ya kukinzana na masharti ya Katiba, kama ilivyobainika kwenye sheria ndogo zilizochambuliwa ikiwemo **Sheria Ndogo ya (Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 (TS Na. 38/19 la Januari, 2024)**, ni ukiukwaji wa masharti ya Ibara ya 64 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

**NA KWA KUWA,** Ibara ya 64 (5) ya Katiba inakataza sheria yoyote zikiwemo sheria ndogo inayobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba,

**KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba**, Mamlaka zilizotunga sheria ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 01** cha Taarifa hii, zirekebishe dosari za sheria ndogo zinazohusika.

### 3.3.2 Dosari ya kuwa na Masharti Yanayokinzana na Masharti ya Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi

**KWA KUWA,** dosari ya sheria ndogo kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, mfano **Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2023 (TS Na. 920 22 Disemba, 2023)**, inaweza:

(i) kukwamisha azma ya sheria mama au sheria nyingine za Bunge;

(ii) kuvuruga mfumo wa sheria za nchi, jambo ambalo halipaswi kuruhusiwa na Bunge; na

**NA KWA KUWA,** matokeo ya dosari hizo yanakwamisha azma ya Bunge kutunga sheria mama na kukasimu sehemu ya madaraka yake kwa mamlaka nyingine serikalini ili ifanye ufafanuzi wa sheria mama kwa namna inayotekelezeka kwa urahisi na kiufundi,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Mamlaka zilizotunga sheria ndogo zenye kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi kama ilivyobainishwa katika **Kiambatisho Na. 01** cha Taarifa hii, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hiyo.

### 3.3.3 Dosari ya Kuweka Masharti yasiyo na Uhalisia

**KWA KUWA,** dosari ya sheria ndogo kuwa na masharti yasiyo na uhalisia kama ilivyoonekana katika sheria ndogo zilizochambuliwa ikiwemo **Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, 2024 (TS Na. 30 la 12 Januari, 2024).**

**NA KWA KUWA**, dosari hiyo inaweza:

(i) kukwamisha utekelezaji wa sheria ndogo yenyewe;

(ii) kukwamisha utekelezaji wa masharti ya sheria mama; na

(iii) kuwa chanzo cha kero miongoni mwa wananchi.

**KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba**, Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na dosari ya kuweka masharti yasiyo na uhalisia kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 01**, zirekebishe dosari hiyo ili kufikia malengo yoliyokusudiwa.

**3.3.4 Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria**

**KWA KUWA**, dosari ya sheria ndogo kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria, kama ilivyobainika kwenye sheria ndogo zilizochambuliwa ikiwemo ***Regulations under The Atomic Energy (Protection from Ionizing and Non-Ionizing Radiation), 2023*** **(TS Na. 840/ 17 Novemba, 2023),** inaathiri ubora wa sheria kwenye ufasaha, usahihi, ukamilifu na kueleweka kwake,

**NA KWA KUWA,** athari hizo mbaya kwenye sheria:

(i) zinaathiri azma ya Bunge kufanikisha utekelezaji wa hatua za serikali kisera kupitia sheria za Bunge na sheria ndogo;

(ii) zinakwamisha nia ya Bunge kuwezesha sheria kueleweka kwa urahisi miongoni mwa watekelezaji wa sheria au wanaoguswa na masharti ya sheria inayohusika; na

(iii) zinaonesha ukiukaji wa misingi isiyopaswa kukiukwa na Bunge lenyewe ambalo ndilo mamlaka kuu ya utungaji wa sheria,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba,** Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 01**, zirekebishe dosari hiyo ili kuleta tija iliyokusudiwa.

**3.3.5 Dosari za Uandishi wa Majedwali**

**KWA KUWA**, dosari za uandishi wa majedwali katika sheria ndogo kama ilivyobainika kwenye uchambuzi unaoripotiwa na kuoneshwa kwenye Jedwali Na. 01 la Taarifa hii ikiwemo **Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 (TS Na. 39/19 Januari, 2024),** inaweza kukwamisha kueleweka kwa sheria,

**NA KWA KUWA,** mkwamo huo unaotokana na dosari za uandishi wa majedwali unaweza kusababisha –

(i) changamoto katika utekelezaji wa sheria ndogo inayohusika, jambo ambalo halikuwa lengo la Bunge kukasimu madaraka ya kutunga sheria kwa mamlaka zinazohusika; na

(ii) kufifia kwa madhumuni ya Bunge kutunga sheria inayotekelezwa ikitegemea ufafanuzi unaopaswa kutolewa na sheria ndogo,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba,** Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zilibainika kuwa na majedwali yenye dosari za kiuandishi kama inavyobainishwa kwenye **Kiambatisho Na. 01**, zifanye marekebisho ili kuepusha madhara ya dosari zilizobainika.

### 3.3.6 Kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio kuhusu Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na Dosari

**KWA KUWA,** Dosari zote zilizobainika katika uchambuzi kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Uchambuzi, ambalo ni **Kiambatisho Na. 01** zinahitaji kurekebishwa inavyostahili,

**NA KWA KUWA,** kutokurekebishwa kwa dosari zilizobainika kutokana na uchambuzi ni jambo ambalo: –

(i) linakiuka misingi ya sheria za nchi na kuathiri tija na ufanisi katika utekelezaji;

(ii) litaendeleza madhara ya dosari hizo katika mfumo wa sheria za nchi; na

(iii) halistahili kuachwa na Bunge liendelee kuwepo kwa kuwa mamlaka yenye dhima na uzuri au ubaya wa sheria za nchi ni Bunge,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Mamlaka zote zinazohusika na sheria ndogo zenye dosari kama zilivyotajwa katika **Kiambatisho Na. 01** cha Taarifa hii, ziwasilishe Taarifa ya utekelezaji wa maazimio yote kuhusu dosari za sheria ndogo kwa Katibu wa Bunge ifikapo saa tisa na nusu ya tarehe 20 Disemba, 2024.

### 3.3.7 Kutokamilika kwa Utekelezaji wa Maazimio ya Kurekebisha Sheria Ndogo

**KWA KUWA,** Maazimio ya Bunge yaliyohusu kurekebisha dosari ishirini na tisa (29) katika sheria ndogo, yalilenga kuondoa madhara ya dosari hizo, ikiwemo uwezekano wa kusababisha kero kwa wananchi;

**NA KWA KUWA**, kutokamilisha maazimio ya Bunge yanayolenga kuondoa dosari za sheria ndogo ni jambo ambalo:-

(i) linalochelewesha utatuzi wa kero za wananchi wanaolitegemea Bunge kusimamia maslahi yao.

(ii) Halizingatii dhima ya Bunge katika sheria za nchi likihusika kwa sheria mbaya au nzuri nchini,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Mamlaka ambazo hazijakamilisha utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, zikamilishe mchakato wa marekebisho na kwamba, ifikapo saa tisa na nusu ya tarehe 27 Septemba, 2024 ziwe zimewasilisha kwa Katibu wa Bunge, taarifa za utekelezaji wake zenye ushahidi wa kurekebishwa kwa dosari zilizobainika katika sheria ndogo zinazohusika.

**3.4 Majumuisho ya Sehemu ya Tatu**

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu ya tatu, taarifa hii imebainisha mambo saba yaliyowekewa mtazamo wa jumla na Kamati.

Mtazamo huo unatokana na misingi iliyobainishwa katika sehemu ya pili ya Taarifa hii ambayo inahusu nafasi ya Bunge katika sheria za nchi, uhusiano wa Bunge na Wananchi, lengo kuu la Serikali kwa mujibu wa Katiba na matarajio ya Wananchi. Misingi hiyo imewekwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 na Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii pia imebainisha mapendekezo **saba** yanayotokana na mtazamo wa Kamati kuhusu mambo makuu saba yaliyobainishwa. Bunge linashauriwa kuyapokea mapendekezo hayo ili yawe maazimio ya Bunge kwa msingi wa

masharti ya Katiba, Kanuni za Bunge na Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 ya Sheria za Tanzania.

**SEHEMU YA NNE**

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika vikao vya Bunge. Kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano Kumi na Tano pamoja na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** utendaji wa kipekee wa Wajumbe wa Kamati hii katika usomaji na kufanya rejea nyingi kwa pamoja na umakini wao kwenye maandishi bila kuchoka ni mambo yaliyofanikisha taarifa hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, (Mb) – | Mwenyekiti; |
| 2. | Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan, (Mb) | M/ Mwenyekiti; |
| 3. | Mhe. Ally Yahya Mhata, Mb | Mjumbe; |
| 4. | Mhe. Amour Khamis Mbarouk, (Mb) | Mjumbe; |
| 5. | Mhe. Jacob Tarimo Priscus, (Mb) | Mjumbe; |
| 6. | Mhe. Khamis Ali Vuai, (Mb) | Mjumbe; |
| 7. | Mhe.Eng.Dkt.Leonard M. Chamuriho,(Mb) | Mjumbe; |
| 8. | Mhe. Simai Hassan Sadiki, (Mb) | Mjumbe; |
| 9. | Mhe. Abdallah Dadi Chikota, (Mb) | Mjumbe; |
| 10. | Mhe. Aloyce Andrew Kwezi, (Mb) | Mjumbe; |

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Mhe. Hamida Mohammed Abdallah, (Mb) | Mjumbe; |
| 12. | Mhe. Ally Mohamed Kassinge, (Mb) | Mjumbe; |
| 13. | Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, (Mb) | Mjumbe; |
| 14. | Mhe. Maryam Omar Said, (Mb) | Mjumbe; |
| 15. | Mhe. Zulfa Mmaka Omar, (Mb) | Mjumbe; |
| 16. | Mhe. Luhaga Joelson Mpina, (Mb) | Mjumbe; |
| 17. | Mhe. Amina Bakar Yusuf, (Mb) | Mjumbe; |
| 18. | Mhe. Latifa Khamis Juakali, (Mb) | Mjumbe; |
| 19. | Mhe. Benaya Lyuka Kapinga, (Mb) | Mjumbe; |
| 20. | Mhe. Nape Moses Nnauye, (Mb) | Mjumbe; na |
| 21. | Mhe. Ummy Ally Mwalimu, Mb | Mjumbe. |

**Mheshimiwa Spika,** Kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru Mhe. William Vanging'embe Lukuvi, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa uratibu wake uliowezesha Kamati kupata taarifa na majibu ya Serikali. Niwashukuru pia Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuchukua fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao katika vikao vya uchambuzi wa sheria ndogo na vikao vya kupokea Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Vilevile, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa huduma bora za kiutawala na uratibu wanazoipatia Kamati na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** Sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa

katika Taarifa hii ili yawe Maazimio ya Bunge katika Mkutano wake wa Kumi na Sita wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Jasson Samson Rweikiza, Mb
**MWENYEKITI**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo**
**4 Septemba, 2024**

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono. Sasa tunaanza mjadala, wachangiaji wetu tunaanza na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Kapinga na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye hoja iliyoletwa mezani leo ya Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo ambayo imeletwa mbele ya Bunge hili. Kabla ya kuanza mchango wangu naomba nichukue fursa hii kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema anazoendelea kutubariki Watanzania na hasa neema ya uhai na amani iliyopo kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nichukue nafasi kuzishukuru Serikali zote mbili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini Jemedari wetu Dkt. Hussein Ally Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais wetu Mama Samia Suluhu

Hassan. Kazi inayoendelea kufanyika ni kubwa, Watanzania tunaiona na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye mchango mahsusi unaohusiana na ripoti ya Kamati ya Sheria Ndogo kama ilivyowasilishwa, mimi nikiwa kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii nimesimama hapa leo kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali. Wamekuwa na jitihada binafsi sana za kufanya marekebisho kwenye makosa yanayofanywa kwenye sheria Ndogo ambazo zinaletwa kwenye Kamati yetu na tunazijadili na tunawaelekeza wafanye nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba Kamati ya Sheria Ndogo ambao mmetupa majukumu na mamlaka ya kukaa na kuzipitia Sheria Ndogo zote kwa niaba ya Bunge lote, Serikali imekuwa na *improvement*, inafanya maboresho kwenye Sheria Ndogo nyingi zinazokuja kwenye Kamati yetu. Kama tulivyoanza Bunge 2020/2021, makosa kwenye Sheria Ndogo yalikuwa takribani 80% mpaka 90%. Kwa mfano, kwenye sheria ndogo moja tu unaweza ukakutana na makosa zaidi ya 10, 15, 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi *improvement* imesababisha Sheria Ndogo nyingi zipungue makosa na yote hayo ni kufuata ushauri wa Kamati na kufuata maelekezo ambayo wanapewa na Kamati. Kipekee nimpongeze sana Waziri wa TAMISEMI na Wizara yote ya TAMISEMI hasa vitengo vilivyopo Wizara ya TAMISEMI vinavyohusiana na sheria. Kwa sababu Sheria Ndogo nyingi hasa za Halmashauri za Mamlaka ya Miji, za Halmashauri ya Mji za Mamlaka za Wilaya, za Kijiji ambazo zinakuja kwetu wana kitengo maalum ndani ya Wizara ambazo wao wanakaa nazo kuzipitisha kabla hazijaja kutangazwa kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekaa nao, tumefanya nao semina sasa tunaanza kuona jitihada za matunda ya yale

maelekezo yetu. Sheria zimekuwa zinapungua makosa na wanafanya vizuri. Hili tunapenda kuwashukuru sana na wamefanya jitihada za dhati kurekebisha makosa yaliyokuwa yakifanywa ambayo mengine yalikuwa *obviously* lakini sasa ili ukae na uone dosari kwenye sheria lazima ufanye kazi ya ziada ya kuzitazama sheria kwa undani na undani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo yale makosa ya kawaida yale yaliyokuwa yanatokea aidha dosari kwenye uandishi au dosari kwenye majedwali au dosari za sheria kukosa uhalisia au kukinzana na Katiba yamekuwa ni madogo, bado yanaendelea kutokea, lakini tunachoshukuru kwa niaba ya Kamati yetu na Bunge lote, makosa yamekuwa yanapungua. Kwa hiyo hicho ndicho nilitaka kuchangia kwa jumla na ni kitu ambacho Kamati tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo ulikuwa mchango wangu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kapinga, jiandae Mheshimiwa Chikota na Mheshimiwa Chamuriho.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwanza kabisa kulipongeza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lenye jukumu la kutunga sheria. Nalipongeza kwa sababu kwa namna tunavyokwenda na hasa *session* hii ya utunzi wa sheria tumeona usimamizi umekuwa mzuri na kazi inafanyika kiuhalisia kweli na sheria zinazotungwa zinatungwa kwa umakini hasa. Kwa hiyo, natumia nafasi hii kukipongeza kiti chako lakini kumpongeza sana Mheshimiwa Spika kwa usimamizi huu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze pia Kamati hii ya Sheria Ndogo. Jukumu hili ni zito na kama unavyojua sheria ni nyingi kweli kweli, lakini chini ya Kamati hii na chini ya uongozi hodari wa Mheshimiwa Rweikiza Kamati hii imejitoa na kufanya kazi kubwa

kweli kuhakikisha dosari zinazokuwa kwenye hizi Sheria Ndogo zinafanyiwa kazi. Kwa hiyo naipongeza sana Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, niipongeze Serikali hususani Serikali hii ya Awamu ya Sita. Serikali hii kwa wakati tofauti imekuwa ikitekeleza maazimio mengi ambayo Bunge lako Tukufu inayatoa, imekuwa ikitekeleza maelekezo mengi ambayo Kamati inayatoa na hivyo sasa tunaona Kanuni nyingi zinazotungwa zimepungua sana changamoto. Changamoto hizi hazipungui hivi hivi, zinapungua baada ya Serikali kutimiza wajibu wa kutekeleza maazimio ya Bunge. Kwa hiyo ninaipongeza sana hii Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niendelee kuipongeza Serikali kwa namna inavyotokeza, inavyo-*appear* kwenye Kamati na hapa niombe sana Waheshimiwa Mawaziri na Taasisi zao pale wanapoitwa na Kamati wasipuuzie, wajitokeze kwenye Kamati, kwa sababu tunapokaa kujadiliana ndipo tunapopunguza matatizo, tunapopunguza sheria zenye dosari ambazo zinawaumiza wananchi na ndipo tunapopata sheria nzuri baada ya mashauriano upande wa Kamati lakini pia na upande wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana na wale ambao pengine na wakati mwingine wanaitwa hawajitokezi wajirekebishe kwa sababu waone umuhimu wa kujitokeza kwenye Kamati ili kupunguza haya matatizo. Kwa nini? Wakati mwingine Serikali inaweza kulegea kidogo kujitokeza kwenye Kamati tofauti na maeneo mengine sisi katika utaratibu tuliojiwekea Serikali inatunga kanuni hizi inazipeleka kwenye matumizi kabla ya Kamati kuzipitia. Kwa hiyo, wakati fulani na mahali fulani sheria hizi zinawaumiza wananchi, lakini wanapojitokeza tunafanya majadiliano, tunafanya marekebisho, tunapata sheria nzuri ambayo inatumika bila manung'uniko na bila bugudha kwa wananchi. Kwa hiyo, niombe sana na nitumie nafasi hii kuiomba Serikali na taasisi zake kujitokeza pale zinapoitwa kwenye Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo niongelee upande mwingine, upande wa halmashauri. Serikali, Wizara na Taasisi huwa zinajitokeza lakini kwa upande wa Halmashauri mara nyingi wanaojitokeza ni Waziri pamoja na wataalam ngazi ya Wizara, lakini ingependeza sana kama waliotunga hizi sheria kwa maana ya Halmashauri husika wangekuwa wanajitokeza kwenye Kamati kutoa ufafanuzi ili wa-*feel facial expression* ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sawa, lakini ingependeza sana kama wale waliotunga hizi sheria, kwa maana ya halmashauri husika, wangekuwa wanajitokeza kwenye Kamati kutoa ufafanuzi ili wa-*feel the deminer* na *facial expression* ya Kamati inapoelezea kwa nini ulitunga kanuni hii, kwa nini ulitunga sheria hii na kwa nini isiwe hivi, iwe hivi. Kwa hiyo ingekuwa inafaa sana halmashauri zikaambatana na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri kuja kwenye Kamati kutoa ufafanuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusema hayo ninaipongeza Serikali, dosari nyingi zimepungua kama alivyosema mzungumzaji aliyetangulia, ambaye ni makamu wangu. Ni kweli dosari nyingi zimepungua kwa sababu hizo ambazo nimezisema hapa, lakini zipo dosari ndogo zimeendelea kuwepo kama Mheshimiwa Mwenyekiti wetu alivyowasilisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, dosari ambazo bado zipo zinaonekana, ambazo ni pamoja na kutunga sheria ambazo zinakosa uhalisia. Naomba sana wanaotunga hizi sheria; na tukumbuke kwamba wajibu wa utunzi wa sheria ni wa Bunge. Wahusika huku wamepewa dhamana tu au wamekasimiwa tu. Kwa hiyo, wanapotunga hizi sheria, watunge sheria zenye uhalisia. Kwa mfano, Sheria Na. 217, ambayo ilitengeneza ada ya ushuru katika Manispaa ya Mtwara kwenye kipengele cha sehemu ya majedwali iliweka viwango vya ushuru wa malori kuingia kwenye mji, kwamba,

malori yakiingia kwenye mji, unaweka kiasi kikubwa cha ushuru; lengo likiwa kuzuia malori yasiingie kwenye mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uhalisia ukoje hapo, unazuia lori moja kuingia kwenye mji kwa kuhofia kwamba litaleta msongamano. Lori moja hili limebeba labda tani 30. Badala ya kuingia lori moja kwenye mji unaweka kodi kubwa ili yaingie malori madogo madogo, kwenye tani 30 utaingiza malori matatu au manne. Sasa hapo unapunguza msongamano au unaongeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano hii Mtwara; twende kwenye uhalisia kabisa. Pale Mtwara ndipo kwenye bandari. Hivi malori yatakayoenda kuchukua mizigo na kupeleka mizigo kwenye bandari ni malori ya namna gani? Ni lori dogo au lori kubwa? Kwa hiyo, unaweza kuona sheria hii kwa kweli haikuwa na uhalisia. Kwa hiyo, wahusika waangalie mazingira waliyokuwa nayo ili watunge sheria zenye uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kuna sheria Tangazo la Serikali Namba 219, Kifungu cha 11 cha Sheria ya Kilimo na Usalama wa Chakula, kimeweka masharti kwamba afisa muidhiniwa anaruhusiwa kuingia kwenye kaya au ghala kufanya ukaguzi. Hakikusema muda gani afisa huyu muidhiniwa aingine kwenye kaya au ghala. Tunaweza tukawa na afisa muidhiniwa mzuri anayetimiza wajibu wake, lakini anaweza akaja afisa muidhiniwa wa hovyo, yeye akawa anataka kufanya kazi usiku tu wa manane. Yeye saa saba za usiku ndiyo anagonga nyumba ya mtu, ngo, ngo, ngo! Watu wamelala. Kwa hiyo, sheria kama hizi zinakuwa hazina uhalisia, lakini kiujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mifano hii michache, niseme tu kwamba, Serikali imekuwa ikisikiliza maelekezo na imekuwa ikitekeleza maazimio ambayo tunayatoa hapa Bungeni. Niombe sana Waheshimiwa Mawaziri na wataalam wao, ku-*appear* ili

mashauriano yanapofanyika tuweze kutengeneza sheria ambazo hazileti kero kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga, hilo ombi lako lipo katika maazimio yenu? Hiyo ku-*appear* kwenye Kamati yenu lipo kwenye azimio? Hicho unachoomba; umeomba hapa wahusika ku-*appear* kwenye Kamati yenu, iko kwenye azimio?

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijafuatilia yote, lakini wakati tunajadiliana ni mambo ambayo tulikuwa tunajadiliana kusisitiza wawe wana-*appear* kwenye Kamati.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Chamuriho, wajiandae Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki na Mheshimiwa Mhata.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninampongeza Mwenyekiti kwa uwasilishaji wa taarifa yetu vizuri. Pia, ninaungana na wenzangu kuipongeza Serikali kwa jinsi inavyosimamia maagizo ambayo yanatolewa na Wizara. Kipekee naipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, ya Mheshimiwa Lukuvi, kwa kazi ambayo wanaifanya. Wamekuwa wakiratibu vizuri Wizara na taasisi mbalimbali kuja kwenye Kamati ili kujibu zile dosari au hoja ambazo zimeibuliwa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kipekee naipongeza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. Kama alivyosema mchangiaji aliyepita, Makamu Mwenyekiti, kwamba huko nyuma kulikuwa na dosari kubwa sana, hivyo, nami mchango wangu utajikita kwenye Sheria Ndogo ambazo zinatungwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma tulikuwa na changamoto kubwa sana, lakini kwa maboresho waliyofanya kwenye *regional secretariat* na kile Kitengo cha Huduma za Kisheria pale TAMISEMI na kule kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa unaona sasa kwamba kuna maboresho mazuri ambayo yanaonekana katika utunzi wa sheria ndogo na hivyo kupunguza dosari na madhara wakati wa utekelezaji wa sheria yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kama inavyofahamika kwamba sheria zetu ndogo zinaanza kutumika kabla hazijaja Bungeni. Kwa hiyo, zikiboreshwa kule zinapunguza madhara kwa wananchi kwa sababu mwananchi wa kawaida anapoamka ofisi ya kwanza kwenda kupeleka malalamiko yake ni kwa Mkurugenzi wa Halmashauri au Mkurugenzi wa Jiji au Mkurugenzi wa Manispaa. Kwa hiyo, naipongeza TAMISEMI kwa kusimamia vizuri kitengo hicho na ni matarajio yangu kwamba wataendelea kukiboresha ili kiendelee kutoa huduma inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita kwenye dosari ambazo zimeonekana kwa sheria ndogo ambazo hazina uhalisia. Mjumbe aliyemaliza kusema ametaja baadhi na mimi nitarejea kwenye Tangazo la Serikali Na. 220 na 217 ambazo ni sheria ndogo ambazo zilitungwa na Mtwara Manispaa. Kwa kweli kuna sheria nyingine ambazo zinatungwa zinakuwa kama adha kwa wananchi na hii tuliiomba hata TAMISEMI sheria kama hizo waweze kuziondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria mojawapo, Mtwara Manispaa wameanzisha ushuru kwa ajili ya wapaa magamba ya samaki. Kwa kweli ushuru huu utakuwa ni adha kwa wananchi ambao wanafanya shughuli hiyo. Ukiangalia sana wanaofanya shughuli hiyo ni watu ambao hawana uwezo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu vilevile unapokusanya ushuru angalia kwamba tunatarajia kukusanya nini. Unakusanya shilingi 200; kwa sababu hata ukipiga hesabu ile *roll* ya karatasi ya kutolea *EFD machine* unapokusanya shilingi 200, nafikiri ile karatasi yenyewe ya risiti ina gharama kubwa kuliko kinachokusanywa. Pia, akina mama, vijana na wazee wanaoshughulika na upaaji wa samaki wanapata kipato kidogo mno. Sidhani kama halmashauri sasa zimefikia hatua hii ya kukosa vyanzo vingine, tuanze kukimbizana na wapaa samaki. Kwa hiyo, naomba ushuru kama huo ambao utakuwa adha kwa wananchi na ambao hauna uhalisia, basi tuuondoe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine nataka nichangie ni kwamba, kuna sheria ndogo ambayo imeanzishwa na Halmashauri ya Mtwara vilevile na Mufindi, kuhusu muda wa kukusanya ushuru. Muda wa kukusanya ushuru wameweka kuanzia saa 12.00 asubuhi mpaka 2.00 usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi hakuna uhalisia, kwa sababu sasa hivi kuna mabasi na kuna malori yanatembea usiku na mchana. Kwa hiyo, tusipokusanya ushuru huu, si kwamba haukusanywi, watumishi ambao siyo waaminifu wanaweza kutumia *loophole* hii wakachukua yale mapato badala ya kuyaingiza halmashauri, yakaingia kwenye mifuko yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mazingira ya sasa hakuna sababu ya kuweka kigezo kama hicho, kwamba ushuru wa halmashauri ukusanywe kuanzia 12.00 asubuhi mpaka saa 2.00 usiku. Ni matarajio yangu kwamba wanaweza kukusanya kwa muda wote. Sheria za utumishi wa umma zinasema mtumishi afanye masaa manane unaweza kuwa na *shift* ili ushuru huu ukakusanywa kwa manufaa ya halmashauri na si kama ilivyo sasa; kwamba inaweza kukusanywa usiku na watumishi ambao si waaminifu na ikaingia kwenye mifuko yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndio uliokuwa mchango wangu. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Chamuriho, wajiandae Mheshimiwa Simai Hassan na Mheshimiwa Mhata.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia mchango huu kuhusu Ripoti ya Kamati yetu. Pia ningependa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuongoza vizuri katika nchi hii, hasa kwa kuanzisha falsafa zake mpya za *4R*. Vile vile, kuendeleza utawala unaozingatia sheria ambao unajumuisha sheria ndogo ambazo ni sehemu au jukumu la hii Kamati ya Kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vile vile, kutoa shukrani kwa Mawaziri wote na Naibu Mawaziri ambao wamehudhuria katika vikao vya Kamati yetu, kwani ni sehemu muhimu sana ya majadiliano katika hoja ambazo huwa zinatolewa na Kamati. Wao hufika kutoa ufafanuzi wa sheria ndogo walizokasimiwa kuzitunga, ambazo kwa jicho la Kamati huonekana zina dosari ambazo inabidi zifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tungependa kuwapongeza na kuwashukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao huwa bega kwa bega na Kamati katika kutoa mwongozo wa kisheria na vile vile katika masuala ya kuwaongoza hao walioandika hizo sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni hizi au sheria ndogo ambazo huwasilishwa huambatana na majedwali. Majedwali haya ni muhimu sana kwani hurahisisha usomaji wa sheria ndogo na vile vile hujumuisha mambo yanayofanana na kuyaweka pamoja ili sheria iweze kusomeka na kutumika kwa vizuri zaidi. Hivyo basi, kama kuna

dosari katika haya majedwali ya sheria ndogo inaathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa sheria ndogo na kwa namna moja au nyingine huleta usumbufu katika azma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita katika dosari zilizoonekana katika majedwali hayo na kutoa mifano mbalimbali ili tuone ni jinsi gani ambavyo majedwali hayo huathiri na yanavyoweza kuboreshwa zaidi. Nitatoa mifano michache.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa kwanza ambao nitautoa ni Tangazo la Serikali Na.1 la Januari, 2024 ambalo lina-*rules under The Accountant Auditors Appeal Board* ya Mwaka 2024. Ukiangalia jedwali la kwanza (a) kuna makosa ya kiuandishi ambayo yanarejea kanuni iliyoanzisha ambayo siyo yenyewe. Sasa, hapo katika utekelezaji, mtekelezaji akifika pale na kwenda kuangalia ni wapi anatakiwa ashughulike napo anakuta sipo na inaleta usumbufu kwani anaweza akaacha kuishughulikia, kumbe pale imeelekezwa kwa makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sheria ndogo hiyo vile vile fomu (b) inatoa *notice* ya anwani za kutoa huduma ambayo ukiangalia zinapoelekeza sipo ambapo kanuni inataka kufanya hivyo. Hiyo inaleta usumbufu kwa yule ambaye anaitekeleza kwani akiangalia kanuni wezeshi anakuta kwamba siyo hiyo. Katika sheria hiyo utakuta kwamba hata fomu (c) (d) na (e) zina changamoto hiyo hiyo; hivyo unakuta kwamba umakini kidogo ulikosekana pale. Bila kurekebisha kanuni hiyo inakuwa ni kama haikukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya pili ambayo ningependa kuitolea mfano ni Tangazo la Serikali Na. 8 la tarehe 5 Januari, 2024 ambalo linahusu *regulation under civil aviation facilitation of air transport* ya Mwaka 2024. Haya nayo pia yanarejea katika jedwali la kwanza sehemu ya tatu na yanarejea kanuni iliyoanzishwa ambayo si yenyewe. Usumbufu ule ambao unakuja katika utekelezaji

unatungwa kwenye jedwali, kufika kule unakuta jedwali lile silo linalohusika. Kwa hiyo, unaweza ukadhani kwamba jedwali hilo halipo kumbe lipo. Hilo litaleta changamoto katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni Tangazo la Serikali Na. 908 la tarehe 22 Desemba, 2023, ambalo ni Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko na Magulio Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ya Mwaka, 2023. Katika sheria ndogo hiyo ya Mlimba kuna jedwali namba tatu ambalo limewekwa mara mbili lakini linaongelea maudhui tofauti. Hivyo, katika utekelezaji wake utakuta mtu ameambiwa aende jedwali namba tatu lakini akienda kule anakuta jedwali silo ambalo linatakiwa kufanya hivyo. Moja katika jedwali hilo namba tatu japokuwa hii ni kanuni ya Mlimba unakuta kwamba jedwali hilo linakuelekeza uende kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Rorya. Kwa hiyo, unakuta kwamba, makosa mengine yanaweza kuepukika kirahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni Tangazo la Serikali Na. 921 la tarehe 22 Desemba, 2023 ambalo linahusu Sheria Ndogo ya Usafi, Afya na Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ya Mwaka 2023. Jedwali hili linaelezea viwango vya ukaguzi kwa ajili ya usajili, ukaguzi, kupima afya, kupulizia dawa na kadhalika. Pia, ukielekezwa ukienda pale unakuta viwango vya usajili havipo. Kwa hiyo, ndani ya kanuni unaambiwa viwango vya usajili vipo katika jedwali hilo, lakini ukienda pale unakuta viwango hivyo havikuwekwa. Kwa hiyo, hii inaweza ikaleta usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa sheria ndogo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tangazo la Serikali Na. 96 la Mwaka 2024 linahusu Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu ya Mwaka 2024. Hii ina jedwali la tatu ambayo inaonesha fomu ya kufifilisha kosa katika makosa yanayofanyika katika halmashauri hiyo, lakini ukienda katika fomu hiyo unakuta linataja halmashauri nyingine kabisa ambayo hata haipo. Kwa hiyo,

unajikuta kwamba huduma ya kufifilisha kosa inakosekana kwa sababu ile fomu siyo husika na haiwezi kutumika katika azma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni Tangazo la Serikali Na. 209 la Mwaka 2024, ambalo linahusu Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Maegesho na Vituo vya Vyombo vya Usafi ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga ya Mwaka 2024. Katika sheria ndogo hii kuna jedwali la kwanza sehemu (b) linaweka viwango tofauti vya ushuru wa mabasi ya aina moja. Unakuta basi ambalo lina abiria wasiozidi 28 limewekewa ada tofauti na ada ya basi lenye uwezo wa kuchukua abiria 28 katika jedwali hilo hilo. Basi la aina moja lakini lina ada katika viwango viwili tofauti. Kwa hiyo, hii katika utekelezaji inaleta changamoto kubwa ambayo inaweza ikaleta usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jedwali hilo pia imetolewa ada katika sehemu (a) kipengele cha 13, ada ya shilingi 10,000 kwa ajili ya maegesho, lakini haisemi hiyo ada ni ya siku moja, wiki moja, mwezi mmoja au mwaka mmoja. Hiyo nayo inaweza ikaleta usumbufu mkubwa sana katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangazo lingine ambalo ningependa kulitolea mfano ni Tangazo la Sheria Na. 217 la Mwaka 2024 ambalo ni Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara ya Mwaka 2024. Sehemu ya pili ya jedwali la kwanza limechanganya maudhui. Unakuta katika jedwali hilo linahusu ushuru wa kituo cha basi lakini humo humo unakuta kuna ushuru mwingine ambao hauhusiki upo katika jedwali lingine ambalo ni wa kuingiza malori mjini. Kwa hiyo, unakuta mtekelezaji anashindwa kuelewa atumie jedwali hilo au lingine hasa ukizingatia kwamba viwango vinavyowekwa huko ni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano ni mingi, lakini ninaomba niishie hapo na niwapongeze sana Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa

Dkt. Jasson Rweikiza na Makamu wake Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan kwa kutuongoza vizuri katika mwenendo wa Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Simai Hassan, wajiandae Mheshimiwa Ally Mhata na Mheshimiwa Ally Kassinge.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji. Kamati ya Sheria Ndogo imekuwa ikikutana kwa vipindi tofauti kwa lengo la kufanya uchambuzi na kuangalia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyokuwa yakitolewa Bungeni hapa katika hatua mbalimbali zilizofikiwa. Ni lazima tukiri ya kwamba licha ya kuwepo kwa jitihada nyingi zinazofanywa na Wizara pamoja na Halmashauri zetu katika kutunga Kanuni hizi ili kuhakikisha kwamba Kanuni hizi wanazotunga haziendi kuleta shida kwa wananchi katika matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba yapo matatizo ambayo kila mara tumekuwa tukiyazungumza Bungeni hapa bado yameendelea kujitokeza ingawa si kwa wingi kama katika miaka michache iliyopita. Kitu cha kusikitisha zaidi ni kwamba Kamati imebaini zipo baadhi ya Sheria ndogo zimeweka masharti au maudhui ambayo yanapingana na Katiba ya nchi hii au Sheria Mama za nchi hii, jambo ambalo limekuwa likikosesha uhalali kanuni hizi katika utumikaje wake, kwa sababu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Katiba ndiyo Sheria Kuu ambayo imeweka masharti ya kufuatwa na sheria zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria zote zinazotungwa na Bunge na Sheria Ndogo zote zinazotungwa na Mamlaka yaliyokasimiwa na Bunge ni Sheria halali za nchi hii kwa mujibu wa Sheria ya Tafsiri ya Sheria Ibara ya 36(1), kwa hiyo ni lazima ziakisi Ibara ya 64(5) ya

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inazilazimisha Sheria zote za nchi hii kufuata misingi halisi ya Katiba kama ilivyokwishaelekezwa kwa kusema kwamba bila kuathiri kutumika kwa Katiba ya Zanzibar, kwa mujibu wa Katiba hii kuhusu mambo yote ya Tanzania, Zanzibar yasiyokuwa ya Muungano Katiba hii itakuwa na nguvu kwa Jamhuri nzima ya Muungano na Sheria nyingine yoyote kama itaweka masharti yatakayokinzana na Katiba hii, Katiba itakuwa na nguvu na Sheria hiyo itakuwa batili kwa kiwango ilichokuika Sheria hiyo, kwa kiwango ilichokiuka Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, utukufu wa kauli hii ya Katiba huwezi kuikuta katika Sheria nyingine yoyote ya nchi hii, kipengele hiki huwezi kukikuta hii inaonyesha ule upekee wa Katiba na inatofautisha Katiba, nguvu za Katiba na Sheria nyingine hususan Sheria Mama na Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuendelea mbali zaidi, leo hii wakati tunafanya uchambuzi wa Kanuni, Kamati hii imebaini kwamba zipo baadhi ya Halmashauri zimetunga Sheria ambazo *totally* moja kwa moja ukizisoma unajua kwamba hawakuzingatia masharti ya Katiba. Kwa mfano, unapoenda kusoma Sheria ya usimamizi na udhibiti wa mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ya 2024 iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali katika Tangazo la Serikali Namba 38 la Tarehe 19 Januari, 2024 basi ukiisomsa ile Kanuni Ibara ya 26(s) utakuta kwamba Kanuni ile inapiga marufuku kwa Watanzania vitu vya msingi ikiwemo uhuru wao wa kujishirikisha na harakati ya vyama vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeenda mbali zaidi ikapiga marufuku hata utaratibu wa mfugaji kuhusika katika harakati za kisiasa hata kupachika bendera katika maeneo yao, *totally* kwa mujibu wa Sheria ile, kwa mujibu wa Kanuni ile mfugaji hatakiwi kuhusika. Imesema kwamba mfugaji yoyote atakuwa ametenda kosa ikiwa atafanya shughuli yoyote ya kisiasa, narejea tena,

mfugaji atakuwa amefanya kosa ikiwa atafanya shughuli yoyote ya kisiasa ikiwemo kupandisha bendera maana yake nini? Hiyo kauli ukiitizama unajua mantiki yao ni nini, lakini shida ya hii *statement* haikujitosheleza, haikuainisha ni maeneo yapi ambayo mfugaji amekatazwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida inakuja na siku zote napenda kusema kwamba wakati mwingine sisi tunaotunga sheria inawezekana tukawa ndiyo chanzo cha tatizo, lakini wakati mwingine mtafsiri sheria inawezekana akwa ndiyo chanzo cha tatizo, lakini kuna wakati anayeenda kusimamia Sheria inawezekana akawa ndiyo chanzo cha tatizo. Katika yote haya umakini na uelewa wa pamoja vinahitajika kuzingatiwa kwa hali ya juu pamoja na ushirikishwaji na mahusiano ya karibu baina ya wanaotunga sheria, wanaotafsiri sheria na wanaoenda kuzisimamia sheria vinginevyo mtunga sheria atakuwa na tafsiri yake, msimamizi wa sheria atakuwa na tafsiri yake, lakini kibaya zaidi kwa msimamiaji wa sheria atakapokuwa na tafsiri yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho kitatupelekea kushindwa kufikia malengo ya zile sheria ndogo tunazozitunga. Katika mazingira kama haya unapozungumza mfugaji kwamba hatakiwi kuhusika na shughuli za kisiasa maana yake wewe moja kwa moja unaenda kumvunjia uhuru wake Kikatiba. Ukisoma Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 20(1) inamruhusu mtu yoyote kujihusisha katika harakati za kisiasa, sasa hii kanuni ilitakiwa iende mbali zaidi kwa kusema tu kwamba, labda hatakiwi kupachika bendera za siasa katika maeneo ya mifugo hapo kidogo ingekuwa imekaa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuiacha wazi kama hivi ilivyo huko kwa watafsiri sheria inaweza ikaleta shida na baadaye tutashindwa kufikia lile lengo halisi ambalo tumelikusudia na itaondosha ile misingi ya utawala bora pamoja na kwenda

kuondosha kabisa misingi ya kidemokrasia ambayo Mama yetu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kila siku anaipigania katika Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuendelea mbele zaidi tumebaini vilevile Kamati hii imebaini kwamba zipo baadhi ya Kanuni ambazo zimetungwa zinapingana na Sheria Mama. Utakapoenda kusoma Sheria Ndogo ya Mazingira ya Wilaya ya Kibondo Tangazo la Serikali Namba 920 lililotoka tarehe 22 Disemba, 2023 *section* ya 16(e), ukienda kusoma hii Kanuni ya Mazingira unakuta wamepiga marufuku kwa mtu yoyote aliyekuwa ndani ya basi atakapoingia katika stendi ya mabasi iwe nje wakati anaingia au anatoka anapokuwa katika Halmashauri tu akiwa ndani ya basi anakatazwa kutupa taka ngumu katika maeneo ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua dhamira yao nini, tunajua lengo lao nini, ni kuhifadhi mazingira, lakini sasa unapotunga Sheria kisha ukaitaja taka ngumu hiyo utakuwa unapongana na Sheria Mama ya nchi hii kwa sababu unaposema taka ngumu, ukiitaja taka ngumu peke yake umeacha ombwe kwa maneno ya Makamu Mwenyekiti wangu akitumia Kipemba unaacha ombwe, sasa ukisema kwamba ni marufuku kutupa taka ngumu, lakini je, atakayetupa taka laini utamhukumu kwa sheria gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake unajikuta umeacha taka ngumu, umeacha taka laini na taka nyinginezo kwa sababu Sheria ya Mazingira ya Nchi hii inafahamu kuna taka laini na taka laini na taka nyinginezo pamoja na taka ngumu, sasa unaposema taka ngumu peke yake maana yake bado utakuwa unakiuka misingi halisi ya utungaji wa Sheria Mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika yote niendelee kuwashukuru sana kama alivyokwishasema Makamu Mwenyekiti wangu, zamani tulikuwa tuna msururu mkubwa wa changamoto hizi za sheria

ambazo zinaletwa pale, lakini sasa hivi kusema kweli tunatumia muda mwingi, lakini makosa unayoyabaini ni machache mno na hii inaonyesha taswira halisi ya namna Wizara pamoja na halmashauri walivyokuwa *serious* katika kutekeleza yale maazimio na wakati wa kutunga hizi Sheria Ndogo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ally Mhata, wajiandae Mheshimiwa Ally Kassinge, Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mheshimiwa Hamida na Mheshimiwa Maryam Omar.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwenye Kamati yetu hii ya Sheria Ndogo. Ninaomba nitoe shukrani zangu za dhati kwanza kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inastawi na inakuwa na maendeleo makubwa, kwa kweli jambo la Kumshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ninaomba niishukuru sana ofisi yako hasa kwenye kitengo hiki cha utungaji wa sheria, kwa kweli wanaturudisha darasani. Namshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa jinsi anavyohakikisha kwamba Sheria zetu tunazotunga zinakuwa sahihi na hana haraka kwa jambo hili. Kwa jambo hili Mheshimiwa Spika tunawashukuru sana meza yote inayofanya kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kwa upande wetu sisi nawashukuru sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, hasa Mwanasheria Mkuu mwenyewe, ni kipindi kifupi amefika, lakini sisi ni mashahidi ameonesha jinsi gani yupo *committed* na shughuli hii, amejifunza kwa haraka na tupo naye sambamba, namshukuru sana. Naishukuru sana ofisi yake ambayo kwa kweli inaratibu shughuli nzima za Utungaji wa Sheria na Uandishi, vijana wake wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichangie katika maeneo yafuatayo ya hizi dosari ambazo zinakosa uhalisia. Sisi tumepitia dosari mbalimbali zinazokosa uhalisia. Kwa mfano, kwenye Tangazo la Serikali Namba 96, Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Halmashauri ya Wilaya ya Magu imetunga Sheria, imetunga Kanuni ya kuzuia watu kulima kwenye miteremko. Kanuni ile ukiiangalia inakosa uhalisia, unamzuiaje mtu kulima katika maeneo yenye miteremko. Sisi wote tumesoma hapa kuna kilimo cha tambarare, kuna kilimo cha miteremko na kuna vilimo vya aina mbalimbali, kwa hiyo Sheria hii imetungwa kuwazuia wananchi kustawi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitarajia Sheria hii itoe mbadala kama unamzuia mtu asilime kwenye mteremko alime nini endapo yeye anaishi kwenye miteremko? Jambo lipo wazi, lipo wazi na tumejifunza wengine tumesoma shule za kilimo, tunajua ukiwa kwenye miteremko unatakiwa ulime kilimo cha aina gani. Sheria za namna hii kwa kweli zinawarudisha nyuma wananchi na zinawaongezea katika umaskini. Ni matarajio yangu kwamba Sheria hii maadamu ni moja mapendekezo yetu Halmashauri ya Wilaya ya Magu wataifanyia marekebisho haraka ili tarehe 27 mwezi Septemba iletwe na marekebisho haya tunayozungumza yawe yamefanyika na kuwasaidia wananchi wetu kustawi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari nyingine ipo kwenye Tangazo la Serikali Namba 219, Halmashauri ya Wilaya ya Mafinga. Halmashauri ya Wilaya ya Mafinga wameleta Kanuni, Kanuni ya kwanza ambayo inawataka wenye vyombo vya usafiri wa umma kusimama kwenye vituo vilivyowekwa isiwe zaidi ya dakika tano. Sheria hii ina ukakasi, mtu unaambiwa usiongeze zaidi ya dakika tano, sasa sheria haisemi ninapopata dharura je, siwezi kuongeza zaidi ya dakika tano? Maana yake wote wanawachukulia kwamba ninyi ni wakosaji, kwa hiyo hata gari kama limesimama zaidi ya dakika tano, lakini lina uharibifu au lina changamoto basi wewe unachukuliwa kama ni mkosaji. Kwa kweli Sheria hii tumeigundua

kabisa kwamba haina uhalisia na utekelezaji wake na ni kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwamba Halmashauri hii ya Mafinga imetengeneza Kanuni ambazo endapo mtu atapaki kwenye maeneo yasiyoruhusiwa basi Halmashauri ya Mafinga ina uwezo wa kuja kukichukua chombo chako na kukipeleka kule kunakotakiwa kwenda kuhifadhiwa kwa gharama zako. Jambo ambalo Sheria hii inaonyesha mapungufu, kama watachukua chombo chako hicho na wakakiharibu wakati wa kukichukua sheria hii haisemi kwamba wao wapo *liable* kulipa hiyo gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka sheria ambazo zisiwe za kimabavu, umekuta chombo nimeweka *wrong parking* sawa, umekichukua, hakikisha unakichukua kwa utaratibu na ukikiharibu wewe ukigharamie uharibifu ule. Sheria hii tumeiona kwamba ina mapungufu na tunaipenda ndugu zetu wa Mafinga waifanyie marekebisho ili kama kuna uharibifu utakaojitokeza basi Halmashauri ya Mafinga iwajibike na uharibifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sheria tangazo la Serikali Namba 217 ambalo wenzangu pia wamelielezea kwa sababu mimi natokea Mtwara, nina *interest* na hii Namba 217 inayohusu ushuru wa uvuvi, ada na muda wa kukusanya ushuru. Ushuru huu najua Halmashauri hii ya Manispaa ya Mtwara inajaribu kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato lakini wamekwenda kwa kweli katika maeneo ambayo watatengeneza kero zaidi kwa watu wetu. Wanakwenda kumchaji mtu ambaye anapaa samaki, ndugu zangu kwa ninyi ambao hamjui kupaa ni wale wanaosafisha samaki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli tumefikia hatua leo tunakwenda kuwachaji ushuru watu wanaopaa samaki, unategemea kupata shilingi ngapi. Wameandika hapa mpaa samaki anatakiwa alipe shilingi 200, mwenye boti analipa ushuru,

wavuvi wanalipa ushuru, kwenye mnada pale wanalipa ushuru, mtu ukichukuwa wale samaki ukianza kuwapaa wanakwambia ulipe ushuru, sasa hii tena imekuwa *too much*, hii Hapana! Hii tunawatengenezea kero. Hawa vijana, vijana wetu wameamua kujiajiri badala ya kwenda kukabana wanafanya hizi shughuli ndogo ndogo. Hebu tuwaache vijana wetu wahangaike na hizi shughuli ndogondogo ili waweze kujipatia kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hawapati zaidi ya shilingi 1,000, kwa hiyo nasema Halmashauri huu ushuru najua mna shida sana ya mapato, lakini kwa vijana hawa kwa kweli imefika muwaachie ili waweze kufanya shughuli nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni muda wa kukusanya ushuru, huu muda waliouweka kutoka saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni, kwa hiyo baada ya saa 12 wale wote watakaotumia muda kwa sababu wameshajua kwamba halmashauri hii muda wa kukusanya ushuru kisheria ni saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni, baada ya hapo hautokusanywa ushuru, kwa hiyo kuna watu wanaweza wakatumia nafasi hii kukwepa ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi miji yetu inafanya kazi masaa 24, vyombo vya usafiri vinasafiri masaa 24, kwa nini wanaji-*limit* wao kufanya kazi muda huu, huu muda mwingine wanalala wanamwachia nani? Halmashauri iweke utaratibu wa *overtime* baadhi ya watumishi wa muda wa kazi wafanye ili waweze kukusanya mapato *24 hours*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni mchango wangu hizi dosari ndogo ndogo ambazo zimejionesha zikimalizika nina imani kwamba wananchi wetu tutakuwa tunawapunguzia kero na wanaweza wakafanya shughuli zao kwa amani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ally Kassinge, wajiandae Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mheshimiwa Hamida na Mheshimiwa Maryam.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja ya Kamati yetu ya Sheria Ndogo na nianze moja kwa moja kwa kuunga mkono hoja ya Kamati kama ambavyo imewasilishwa na Mwenyekiti wetu wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati yetu, lakini pia kupitia Maazimio ya Mkutano wa Bunge wa Kumi na Nne, baadhi ya mapungufu ambayo tumeyabaini sisi katika Kamati pamoja na mengine ni pamoja na uandishi wa Kanuni usiozingatia taratibu za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa niseme tu kwamba sheria ni eneo la kiweledi, kanuni ni zao la sheria, hivyo basi kanuni hizi au sheria ndogo hizi zikiwemo *rules, bylaws* na zinginezo zisipoandikwa kwa mujibu wa taratibu na matakwa ya kisheria zinapunguza ubora wake, zinapunguza ufasaha wa kueleweka lakini pia zinaleta mkanganyiko katika utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitatoa baadhi tu ya mifano ambayo kwenye Kamati tumebaini ambayo kimsingi imekiuka taratibu za uandishi wa kisheria. Kwa mfano, Wizara ya Fedha, ina sheria yake ya *The Accountants and Auditors Registration Act, Cap. 286* ambayo imetungiwa kanuni kwa Tangazo la Serikali Na.1 la tarehe 5 Januari, 2024 inayojulikana kama *Rules and The Accountants and Auditors Appeals Board 2024*.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya kanuni hii ni kwamba *Form A* katika Jedwali la kwanza ambayo inahusu *notice*

ya kusudio la kukata rufaa imekuwa na changamoto ya kiuandishi kwa kurejea kuanzishwa kwake, imerejea Kanuni ya 8(2)(a) badala ya Kanuni ya 7 kama ambavyo ndivyo ipo kwenye kanuni husika. Mkanganyiko kama huu, tafsiri ya kisheria maana yake ni kwamba tumetunga kanuni ambayo haiendi kutekelezeka kwa sababu kifungu hicho hakipo kwenye kanuni iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika Wizara ya Uchukuzi, ina sheria yake ya *Civil Aviation Act, Cap. 80* ambayo na yenyewe imetungiwa kanuni kwa Tangazo la Serikali Na.5 la tarehe 5 Januari, 2024 ambayo ni *Regulation under the Civil Aviation Certification, Licensing and Registration of Air Drones 2024*. Changamoto ya uandishi wa Kikanuni katika kanuni hii tunaibaini katika Kanuni ya 64(3) ambayo inamtaka mhusika aliyepewa *notice* ya kusitishwa cheti, leseni au usajili kuwasilisha utetezi wake kwa mamlaka ndani ya siku 14, lakini imefanya makosa kwa kurejea kanuni ndogo ya (2) ambayo haipo katika kanuni iliyotungwa. Hii kadhalika inafanana na kanuni ile ya mwanzo ambayo nimeitolea mfano. Tafsiri yake ni kwamba kanuni hii haitaenda kutekelezeka kwa sababu wamerejea kifungu ambacho hakipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni hizi ambazo zimebainishwa na Kamati yetu ambazo zina mapungufu ya uandishi wa kikanuni au wa kisheria ni nyingi; lakini nimalizie na Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ya Mwaka 2024 ambayo imetungwa kwa Tangazo la Serikali Namba 38 la tarehe 19 Januari, 2024. Katika sheria ndogo hii Kifungu cha 3 kimeweka tafsiri ya neno Mkurugenzi, lakini katika ufafanuzi wa tafsiri ya Mkurugenzi sheria ndogo hii imetafsiri Mkurugenzi kuwa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Moshi, kule ndani unapochimba katika kanuni. Kule juu katika tafsiri sheria au kanuni au sheria ndogo hii imetafsiri Mkurugenzi ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika kanuni hiyo hiyo moja au sheria ndogo hiyo hiyo moja juu kule unapotafsiri Mkurugenzi unatafsiri kuwa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, lakini ndani kule unapokuja kumtaja Mkurugenzi kuwa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Moshi, hii kisheria maana yake ni kwamba haitaweza kutekelezeka kwa sababu kuna *legal technicality* ndani yake. Hivyo, basi kwa sababu madhumuni ya kanuni hizi ni kwenda kutekelezwa na kuleta tija kwa jamii yetu, tutoe rai sisi kama Kamati, kwamba mapungufu haya ya uandishi wa kikanuni ni vizuri Wizara husika ziende kuyarekebisha ili kanuni hizi ziendane na matakwa ya uandishi wa kisheria, lakini pia ziweze kutekelezwa bila kuathiri taratibu za mkanganyiko katika kutafsiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tarimo, wajiandae Mheshimiwa Hamida na Mheshimiwa Maryam.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia. Pia niungane na wenzangu na hasa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Sheria Ndogo kuanza kabisa kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wenzangu wamekwenda kwenye *case specific,* mimi nitakwenda kwenye mambo ya jumla ambayo tunafikiri yataweza kusaidia katika utungaji wa sheria hasa kwenye halmashauri zetu na kwa kuanza kabisa najua Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mwandishi wa Sheria pamoja na Wizara wanafanya juhudi kubwa sana kuhakikisha hizi kanuni au hizi sheria ndogo zinaleta tija. Sasa kwa sababu ya makosa ambayo tumeshayaona mara nyingi, nitoe ushauri wa jumla kwanza. Ni vizuri sheria zote za halmashauri zinazokuja hapa kabla

hazijaingia kwenye Kamati Ndogo au wakati zinaingia Wabunge wa maeneo husika pamoja na kwamba ni Madiwani wapewe zile sheria na wao wazipitie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivi kwa sababu zipo sheria ambazo *either* kwenye mchakato wake wa kutengenezwa kuna maneno yameingia katikati ambayo yanaenda kusababisha kero kwa wananchi; na Mheshimiwa Mbunge anaonekana yeye tayari ni Diwani na amezijadili wakati kiuhalisia Mheshimiwa Mbunge anakuwa hapa Bungeni kwa zaidi ya miezi saba kwa mwaka mzima na hivyo huenda kikao kilichopitisha sheria hizo yeye hakuwepo. Zikienda kuleta kero kule tayari na yeye zinamgusa moja kwa moja

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeyaona hayo kwa sababu baadhi ya Waheshimiwa Wabunge tuliowa-*consult* kwamba kuna sheria hii inataka kupita kwenye halmashauri yako tunaona iko hivi, unaona kabisa kwamba Mheshimiwa Mbunge hana taarifa. Kwa hiyo huo ni ushauri wa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa pili ni halmashauri ambazo zina mchanganyiko wa maeneo yenye miji pamoja na maeneo yenye asili au yanayokuwa yana asili kama ya vijiji. Tumeona kwenye sheria za mifugo, sheria za kilimo pamoja na sheria za mazingira. Unakuta kuna halmashauri, hata Dar es Salaam, kwa mfano Temeke, kuna sheria ambayo ilikuwa inaelezea kuwa na *limit* ya mifugo na mifugo iwe na kitambulisho nadhani; lakini kuna maeneo katika halmashauri hiyo hiyo yana asili ya kijiji ambayo sheria hiyo ikienda, inaenda kusababisha matatizo. Kwa hiyo, ni vizuri sheria zisiwe *generous* hivyo ili ziweze kuleta tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi wameongelea ile sheria iliyokuwa inatoza kodi kwa wapaa samaki, wale wanaokwarua, wanakwangua au, wapaa samaki, sijui Kiswahili sahihi; ambapo walikuwa wanawa-*charge* shilingi 200 kwa kila mtu.

Sasa ukiangalia zipo sheria zinazoelezea asilimia ya gharama za ukusanyaji wa kodi yoyote. Ukiangalia tu hawa hapa wa samaki ambao walikuwa wanatakiwa walipe shilingi 200 ukiangalia kale ka-*rim* kakuweka kwenye mashine ya *EFD* kale kashilingi 2,000 kanatoa risiti 100, kwa hiyo risiti mia moja kwa shilingi elfu mbili ukigawanya kale kakaratasi peke yake katakula shilingi ishirini. Hapa hatujapiga mahesabu ya wino, hatujapiga mahesabu ya mkusanyaji, hatujapiga mahesabu mengine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utaona kabisa hii kodi ambayo wenzetu walikuwa wanataka kuileta si tu wanaleta usumbufu kwa wale watu wa chini bali pia gharama yake ya ukusanyaji inaweza ikapita hata hiyo shilingi 100, shilingi 200, kwa hiyo, itakuwa haina hata tija kwenye makusanyo ya halmashauri hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na makosa ya jumla; kwa mfano, halmashauri inaleta kodi kwenye eneo ambalo haihusiki tena katika kusimamia. Kwa mfano, sheria ile iliyoletwa na halmashauri ya Mtwara Mikindani ya ku-*charge* lori kubwa kuingia mjini, si tu kwamba ilikuwa inaleta usumbufu zaidi kuliko wao walivyokuwa wanafikiria kupunguza msongamano, lakini ni dhahiri kwamba barabara za mijini nyingi ni tani 10, haya malori wanayoongelea ni tani 30, wao wanatoa tozo kwenda kukusanya hiyo hela wakati barabara ziko chini ya *TARURA*. Kwa hiyo, unaona kwamba wanakusanya kwenye eneo ambalo si lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni kuhusu sheria ya ukataji barabara kwa ajili ya kupitisha miundombinu. Halmashauri inataka kukusanya lakini barabara ni mali ya *TARURA*. Kwenye hilo la lori kubwa ni kwamba wanakusanya kodi kwenye uvunjaji wa sheria na wala si faini. Maana yake ni kwamba mtu mwenye lori la tani 30 atalipa hiyo hela wanayotaka aingize lori lenye tani 30 likaumize barabara wakati sio mamlaka yao na barabara zimeshahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine, kuna halmashauri zinaleta sheria za ukusanyaji ushuru wa mauzo kwa mfano ya nafaka halafu wanasema bei itakayokuwa inatumika ni bei ya soko bila kuonesha ni bei ipi; ya soko, inayotolewa na Wizara, inayotolewa na Benki Kuu au inayotolewa na halmashauri yenyewe. Wanasema tutakusanya asilimia tatu kwa kilo kwa bei ya soko, lakini bei ipi ya soko inayopatikana kupitia chanzo gani. Kwa hiyo, haya yote yanaenda kuleta mkanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho lililokuwa na mkanganyiko; halmashauri nyingi zimeleta sheria ya ukamataji mifugo na wanasema mifugo itakamatwa kwa siku kadhaa na kama *fine* haitalipwa watapiga mnada. Hata hivyo, kwa huo muda ambao wanakuwa na hiyo mifugo, hawakuonesha wajibu wa halmashauri kwenye kuhudumia hiyo mifugo, chakula, maji na baada ya hizo siku sita kama watakwenda kwenye mnada na mnada ukashindwa kufanyika kwa sababu bei ya soko haikufikiwa, ni nani ataendelea kusimamia hali ya hiyo mifugo kwa kipindi chote. Kwa hiyo, hayo ni mapungufu ambayo kiujumla yameonekana na yatakapoendelea kuboreshwa yatasaidia hizi sheria ndogo zije zikiwa na uhalisia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hamida Abdallah, jiandae Mheshimiwa Maryam Omar.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Mwenyekiti wetu kwa kuwasilisha taarifa hii

ya Kamati ya Sheria Ndogo, lakini pia niwapongeze Kamati ya Sheria Ndogo kwa kufanya kazi nzuri ya uchambuzi wa sheria pamoja na kanuni ili kufanya shughuli za kila siku za taasisi mbalimbali, Wizara na halmashauri ziweze kutekelezeka kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kusimamia majukumu yake ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika nchi yetu kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ambayo tumejiwekea. Tumeona tumepiga hatua kubwa sana katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inasonga mbele. Pia nimpongeze kwa dhati kabisa Mwanasheria Mkuu, amekuwa msaada mkubwa katika usimamizi na uchambuzi wa sheria hizi na kuharakisha michakato mbalimbali na kufanya sheria hizi ndogo ambazo zinatungwa na kanuni kuelekea katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejifunza mengi katika Kamati hii ya Sheria Ndogo na nimeona kwamba mambo yote ya utekelezaji tunayokwenda nayo kila siku ni lazima yazingatie sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ambayo tumejiwekea ili kuharakisha maendeleo, lakini kuleta ustawi wa wananchi wetu, pia kuongeza ajira katika sekta binafsi pamoja na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo halmashauri ambazo zilileta sheria ndogo na tumezipitia na tumeona kuna changamoto mbalimbali. Wasijisikie vibaya ndugu zetu wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara kwa sababu sheria yao tayari ilikuja kwetu na tumeipitia tumeona mapungufu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Sheria Ndogo ya Kilimo na Usalama wa Chakula wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani, Sheria ya Tangazo la Serikali Namba 219 ukiangalia

Kifungu cha 15 kinaweka utaratibu wa namna ya kushughulikia mifugo inayotembea kiholela. Tatizo ambalo tumeliona kimakosa ni utoshelevu wa masharti yanayohusu namna ya kushughulikia hiyo mifugo, maana baada ya mifugo hiyo kushikwa kinachoendelea hapo hakijasemwa na kinaleta utata kwa mwenye mifugo yake ambayo imekamatwa. Kwa sababu halmashauri wanapokamata mifugo na kuweka katika eneo ambalo wanaweka na kumpa mwenye mifugo yake labda siku saba aende akalipe faini, maana yake ni kwamba mfugo ule hakuna mtu anayeutunza kwa kumpa malisho ya chakula, maji pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inapotokea kukosekana kwa haki ya mwenye mfugo unaokamatwa baada ya mfugo wake kufa anakosa haki kwa sababu sheria haijakaa vizuri. Kwa hiyo, ndugu zetu wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara waendelee kujipanga vizuri kuhakikisha kwamba sheria hii inakuwa wazi na inaweka kipengele hicho wazi kuhakikisha kwamba kila mmoja anakuwa haki; na mwenye mifugo yake pale inapotokea mfugo wake unakufa, basi aweze kupata haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona pia mambo mengine katika uandaaji wa majedwali yetu haya. Tunajua kwamba kuna utaratibu wa kisheria wa uandaaji wa majedwali, lakini inapotokea kuwepo kwa *typing error,* neno tu likibadilika tafsiri yake kwenye utekelezaji wake inaleta shida na inakuwa ngumu sana. Kwa hiyo, niombe waandaaji wa majedwali haya wazingatie tafsiri ya maneno inayoendana na utekelezaji wa jambo lile husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwamba tumefanya kazi kubwa kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba tunalisaidia Bunge letu kuweka sheria hizi ndogo ziweze kwenda kwenye utekelezaji vizuri na kuendelea kuleta ustawi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Maryam, wajiandae Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mheshimiwa Lukuvi.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kusema neno katika hoja iliyoko mezani ambayo ni hoja ya Kamati yangu, Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia nikaweza kusimama hapa muda huu. Nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuhakikisha Taifa letu la Tanzania tupo pazuri. Pia nimpongeze Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Mwinyi kwa kazi nzuri pia anayoifanya katika kuhakikisha Zanzibar inasonga mbele na inapata maendeleo yanayofaa. Nimpongeze pia Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja nawe Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kazi nzuri wanazofanya kuhakikisha Kamati tunafanya kazi zetu ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sitokuwa msemaji sana kwa sababu wengi waliopita wameyazungumza mengi tu ambayo yanaonesha namna Kamati tulivyo makini katika kuhakikisha kanuni zinasimamiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaunga mkono moja kwa moja wanakamati wenzangu katika kuhakikisha kwamba kanuni hizi zinasimamiwa ipasavyo. Kwanza, ukizingatia hizi kanuni zinatungwa na kwenda kutumika moja kwa moja kabla ya kuja kwetu. Hapa ndipo mwananchi anapoanza kuumia na ni vizuri sana Wizara zikazingatia kwamba wanapokuja kwenye Kamati waje na watu wa halmashauri, wataalam wetu wa sheria wa halmashauri kwa sababu

wao ndio wanaozitunga hizi sheria. Mara zote mtu akiwepo pale tukiwa tunajadili itatupa urahisi zaidi katika kuhakikisha haumii anayetumia hizi kanuni, anayezisimamia, wala haumii mwandishi wa hizi sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi hapa wamezungumza namna gani Halmashauri ya Mtwara, nami niungane moja kwa moja na wenzangu kupinga Sheria Namba 217 inayohusu Halmashauri ya Mtwara, inayohusu mpara samaki. Mwenzangu mmoja hapa, Mheshimiwa Mhata amesema, chombo cha uvuvi kina leseni, kinalipa kodi, mvuvi analipa kodi, pale kwenye mnada kuna ushuru unatolewa, leo jamani na mpara samaki? Tukienda hivi na kesho tutasema kuwa kila anayekula samaki atoe ushuru. Jambo hili si sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naaibu Spika, nilifikiria nikasema, kwa mfano hii sheria inakuja kule kwetu Zanzibar na ikaja moja kwa moja Kaskazini ambako ndiko Jimbo langu lilipo, kule wapara samaki wengi ni wazee na ukienda siku za wikiendi utakuta ni watoto wadogo walioona ngoja nikatafute pesa yangu ya kutumia shuleni Jumatatu, ndivyo tulivyozoea, kiasi ambacho hata wewe mnunuzi wa samaki ukishanunua ukimpa yule mtoto kupara, mwisho wa siku pengine umempa shilingi 500, akakwambia mimi nitakuparia kwa shilingi 200, unaona huruma unamwachia na ile 500 yote na hudai chenchi. Leo hii Serikali pale tukaweke mkono tudai tena ushuru? Hili si sawa na tuachane nalo, wala tusilijadili sana. Hii Sheria tuachane nayo kabisa na Halmashauri ya Mtwara wasione kwamba tunawaonea, hii ni hali halisi na uhalisia ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini sheria kama hizi ambazo hazijafika huku kwetu ziko nyingi na ziko huko zinatumika. Wizara na Mwanasheria Mkuu wa Serikali tuongeze umakini katika kuhakikisha kwamba tunazisimamia hizi sheria tukizingatia kwamba zinakwenda kutumika ndipo zinakuja kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema mengi hapa kuhusu makosa ya kiuandishi. Hebu mathalani jamani kwenye makosa ya kiuandishi, sheria hii imeanza kutungwa na Halmashauri pale kwa mtu wa sheria, ikaenda kwa Mwanasheria Mkuu ikaenda kutungwa mpaka inafika kwenye Kamati, kosa la kiuandishi jamani? Tuwe makini katika kuhakikisha kwenye hizi sheria tutapunguza haya makosa kama si kumaliza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitaki niseme mengi kama nilivyotangulia kusema, wenzangu waliopita wameyazungumza mengi na mimi ni katika kukazia tu yale yaliyozungumzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mwanasheria Mkuu dakika tano, ajiandae Mheshimiwa Lukuvi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Taarifa hii nzuri. Pili, nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Dkt. Jason Samson Rweikiza pamoja na Wajumbe wa Kamati wote kwa kazi kubwa na nzuri waliofanya na kwa hii taarifa nzuri ambayo inatupatia picha halisi ya changamoto ambazo tunazo katika uandaaji wa Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuelezea kidogo hali ilivyo kwa sasa katika zile Sheria Ndogo ambazo zimefikishwa kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ajili ya uhakiki ili baadaye ziweze kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati imeziainisha na ziko tatu. Pia, ingekuwa ni vema leo nikatoa hali halisi ilivyo sasa. Sheria

Ndogo ya kwanza ilikuwa ni zile Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelekaji na Usambazaji wa Umeme za Mwaka 2023 ambazo zilifika kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako kwamba, Kanuni hizi tayari zilishahakikiwa na zimeshatangazwa kwenye Gazeti la Serikali kwa matoleo mawili, Toleo la Kiingereza kupitia *GN. No. 677* na lile Toleo la Kiswahili *GN. No. 679)* na Toleo hili lililotoka 9 Agosti, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna kanuni za *The Accountants and Auditors Training and Examination Bylaws, 2023*, naomba kulipa Bunge lako Tukufu kwamba, kazi hizi sasa ziko katika hatua za mwishoni, tumemaliza uhakiki na tunatarajia kutangaza siku ya tarehe 5 Septemba, 2024 kwenye Gazeti la Serikali kwa maana ya kesho Ijumaa. Kanuni zitakazosalia ni zile za ukusanyaji na uchakati wa taarifa binafsi ambazo ziko kwenye hatua za mwisho na nina imani kabisa kwamba, ndani ya muda uliowekwa na Kamati, kanuni hizi zitakuwa zimekwishatangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema tu kwamba, kimsingi Kamati hii imekuwa ikifanya kazi nzuri na kutokana na taarifa zao zimekuwa zikitusaidia kama Serikali katika kupunguza dosari na idadi ya Sheria Ndogo ambazo zimekuwa na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba, katika taarifa hii idadi ya Sheria Ndogo ambazo zinakinzana na masharti ya Katiba zimepungua kutoka 13 na sasa ziko mbili. Kwa hiyo, hiyo ni dalili nzuri kwamba tukiongeza bidii katika kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa na Kamati, idadi ya Sheria Ndogo zinazopingana na masharti ya Katiba zinaweza kupungua kabisa kutoka mbili na kuwa sifuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya Sheria Ndogo zinazokinzana na Masharti ya Sheria Mama na zenyewe zimepungua. Zilikuwa 27 wakati huo mara ya mwisho na sasa tunazo 10 tu. Vilevile, Sheria Ndogo zenye masharti yasiyoakisi uhalisia hapo bado tunahitaji kuongeza bidiii kwa sababu zilikuwa sita wakati ule na sasa ziko 22. Kwa hiyo, tunahitaji kujiuliza kuwa kwa nini zinaongezeka? Pia, Sheria Ndogo zinazoakisi makosa ya kimsingi ya uandishi huko tumeendelea kufanya vizuri maana zilikuwa ziko 70 na sasa ziko 13 tu. Kwa hiyo, hiyo ni dalili kwamba tunafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Ndogo zinazoakisi suala zima la utengenezaji wa majedwali, kwa mujibu wa sheria hizi zimeongezeka kutoka saba kwenda 13. Kwa hiyo, tunahitaji kuongeza bidiii zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeandaa mkakati mahsusi. Kwanza, ni kutengeneza Mwongozo kwa Mawakili wote wa Serikali nchini ili uweze kuwasaidia wanapotengeneza hizi Sheria Ndogo. Vilevile, watakuwa na orodha au *checklist* ambayo itakuwa inaainisha hayo mambo ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kufanya mafunzo kwa Mawakili wote wa Serikali nchini, lakini na mafunzo kwa Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali. Mafunzo Mahsusi kwa ngazi ya *Diploma* na ngazi ya *Masters* ili Mawakili wa Serikali waweze kuwa vizuri na tunaamini kwamba kwa kufanya hivyo, changamoto hizi tutazipunguza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii, ninakuahidi na niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, mapendekezo yote tutayafanyia kazi kwa lengo la kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Lukuvi dakika tano, jiandae mtoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema. Pili, nitumie fursa hii kutoa pongezi na shukrani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mwenyekiti wa Kamati hii na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Makamu Mwenyekiti, Wajumbe wote wa Kamati hii na Sekretarieti kwa kuratibu vizuri sana zoezi hili la Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ni muhimu sana na ni nyenzo muhimu ya Bunge letu Tukufu katika kufuatilia utekelezaji wa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo yanayokabidhiwa kwa mamlaka mbalimbali Serikalini kama ambavyo tumezisikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ilifuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo 22 zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa 12 na 13 wa Bunge. Serikali tayari ilifanyia kazi taarifa kama ambazo nyingine tumezisikia kutoka kwa Mwanasheria Mkuu na Kamati yenyewe, Sheria Ndogo 19 kama ilivyopongezwa na Kamati, Sheria Ndogo tatu zilizobaki zipo katika hatua za mwisho ambapo kwa sasa zipo katika hatua za uhakiki. Maelezo ya uhakiki na hatua za Kamati kwa Sheria hizi tatu tumeyasikia hivi punde kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na nyingine tumeambiwa inakwenda kutangazwa leo. Narudia kuwapongeza sana Kamati kwa usimamizi mzuri kabisa ambao umesababisha kuondoa kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyobainisha Mwenyekiti wa Kamati, wamechambua Sheria Ndogo Ndogo 179 zilizowasilishwa

kwenye Mkutano wa Bunge wa Kumi na Nne na Sheria 163 zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge. Kazi ya uchambuzi wa sheria hizo imekuwa ikifanywa na Kamati hii kwa weledi mkubwa bila kuchoka kwa sababu inafahamu kuwa inatenda yote hayo kwa manufaa ya wananchi, hasa wale wananchi maskini wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, kazi inayofanywa na Kamati hii kwa kweli inafanya kazi nzuri sana hasa kwa niaba ya Wabunge wote kwa sababu na sisi tumechaguliwa na wananchi ili kulinda haki na heshima yao. Pia, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, siku zote amekuwa anajipambanua kwamba hapendi kabisa wananchi wanyanyaswe au wakose huduma au kusumbuliwa, kubughudhiwa kwa namna nyingine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya sheria hizi tumezisikia ni kweli zinaleta usumbufu na taharuki kwa wananchi. Hapa mwisho tumemsikia Mheshimiwa Mbunge juu ya wapara samaki wa Mtwara. Ninaamini kule hata kama wanazitumia, wataacha leo, maana sheria kama hizi zinaleta bughudha na maudhi kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wenzetu wengi wale wanaotunga tunga sheria kama hizi, kama wanasikia basi wajifunze kazi njema inayofanywa na Kamati na wajue hii Kamati haijalala. Sheria zote ambazo zitakuwa zinaleta usumbufu, kero kwa wananchi, zitafutwa na hii Kamati na Bunge hili linaridhia kazi ya hii Kamati. Kwa hiyo, Sheria kama hizi zinaleta usumbufu, kwa hiyo, tumsaidie Mheshimiwa Rais ili akiyasema na wenzetu kule wanaoanza kutunga hizi sheria, wamsikie na waache kabisa kutunga hizi sheria ambazo zinaleta taharuki kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu tutafuatilia na kusimamia wahusika wote kuzingatia maagizo ya Bunge lako Tukufu. Aidha, tayari tumetoa maelekezo kwa mamlaka zote kwamba, katika uandishi wa Sheria zao Ndogo, ni lazima wamshirikishe Mwanasheria Mkuu. Pia, Mwanasheria Mkuu amefika juzi na nafurahi kwamba Wabunge wengi wamempongeza kutokana na utulivu wake na umakini aliouonesha kwa muda mfupi huu uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kuwa tuko hapa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mmemsikia akisema kwa nia njema, basi wanasheria walio chini yake huko kwenye Halmashauri wazingatie nia njema ya Mwanasheria ambaye ndiye kiongozi wao ili sheria zinazokuja kuanzia sasa ziakisi nia njema ya huyu bosi wao. Vilevile, mjue yuko makini sana. Kwa hiyo, najua Sheria kama hizo hazitakuja tena kwenye Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kumshukuru sana tena Mwenyekiti na Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi, lakini nakuhakikishia kwamba, tunafurahi kazi hii, tunasema sasa Serikali inafanya vizuri, hivyo tunafurahi sana na kwamba TAMISEMI ambao wana mlundikano wa sheria hizi ndogo nao sasa wanafanya kazi vizuri. Sisi tutaendelea kuwabana ili kuhakikisha kwamba, zisiwepo kabisa sheria zinazokuja kutangazwa ambazo zina maudhui yanayokwenda kunyanyasa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nirudie taarifa njema aliyoisema mdogo wangu David Kihenzile ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano huko China alipo, kwa kazi kubwa aliyoifanya leo na taarifa hii tumeisikia kutoka kwa Naibu Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa David Kihenzile juu ya kusaini huu mkataba wa *TAZARA*. Hii ni kazi njema iliyotukuka ambayo kwa kweli Watanzania wote tunapaswa kumpongeza kutokana na mwanzo mzuri wa ziara hii ya kimapinduzi. Tumekuwa na reli hii ambayo

imekuwa inasuasua kwa muda mrefu, lakini leo kwa kusaini mkataba ule inakwenda kutuondoshea shida, kupunguza na kuongeza mapato ya wananchi kutokana na usafirishaji utakaoboreshwa kutokana na reli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ni muhimu sana na nzuri sana kwetu kuisikia hivi leo. Baada ya maelezo haya nakuhakikishia kwamba, Serikali hailali na itahakikisha kwamba, jambo hili linaratibiwa lakini sheria ndogo ndogo zote zitakazokuwa zinatangazwa, zitatangazwa kwa namna ambayo zinakidhi malengo na matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mtoa hoja.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuja kuhitimisha hoja yangu, nakushukuru sana. pia, nami nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuongoza nchi hii vizuri na kuhakikisha kwamba anaileteа nchi hii maendeleo kwa kasi kubwa na tuna utulivu na amani ya kutosha kufanya shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru wachangiaji wote ambao wamechangia hoja yangu kwa umakini na ufasaha mkubwa, jumla tumepata wachangiaji 14 na wote wameunga mkono hoja, kufafanua na kuongeza nyama kwenye hoja yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa maelezo aliyoyatoa, lakini siyo tu maelezo aliyoyatoa

hapa bali hata mchango wake kwenye Kamati yetu. Kazi za Kamati zinakwenda vizuri kwa sababu ya msaada wake anaotupatia na uratibu mzuri sana. Vilevile, nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi hiyo, ofisi yake imekuwa msaada mkubwa kwenye Kamati yetu na watumishi chini yake wamekuwepo muda wote kwenye Kamati, tunakuwa nao kwenye uchambuzi kujadili mambo mbalimbali na wanatusaidia sana kwa utaalam na uzoefu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru na kuwapongeza Sekretarieti ya Kamati ambayo inafanya kazi masaa 24, Ofisi ya Katibu wa Bunge ambayo nayo inatusaidia kwenye uratibu wa shughuli za Kamati. Kipekee niwashukuru Wabunge wote ndani ya Bunge hili kwa kuunga mkono kazi za Kamati yetu, mmeona hapa michango iliyotoka Wabunge wote wanatuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ni chombo cha Bunge hili. Ni chombo cha Bunge hili cha kutazama ubora wa sheria zinazotungwa na mamlaka nyingine na watu wengine huko tuliowakasimu kazi hiyo na kuchuja na kuona kama ziko bora na kukidhi viwango vya sheria zinazotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapopata sheria hizi zinapowekwa mezani hapa, tunaanza kuchambua. Tunachambua na tunaona kama ziko sawa, baada ya hatua hiyo tunawaita wahusika, tunajadiliana nao, tunawasikiliza, tunawauliza maswali na wenyewe wanatuuliza maswali, tunakwenda pamoja na tunawashirikisha vizuri. Baada ya hatua hiyo tunachambua tena kwa niaba ya Bunge hili, lakini sisi ni Wabunge kutoka kwenye maeneo mbalimbali ya nchi hii, tunakuwa na mawazo ya wapiga kura wetu na tunaangalia maslahi ya wapiga kura wetu. Kwa hiyo, tunafanya kazi hiyo kwa kuzingatia hasa maslahi makubwa ya wananchi tunaowawakilisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hizo zote tunaleta taarifa yetu hapa Bungeni na Wabunge nao wanapata nafasi ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa kama walivyofanya leo, mmeona hapa na baada ya hatua hiyo Bunge linatoa maazimio ya kutekelezwa na wahusika wa kutunga zile Sheria Ndogo na wanapewa maelekezo hao waliotajwa hapo ambao ni watunga sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuondoa usumbufu kwa wananchi ili wananchi wapate sheria ambazo ni nzuri zinazotekelezeka vizuri, kusiwe na kero yoyote kwa wananchi au uonevu. Mmesikia michango ya Wabunge hapa, kuna baadhi ya sheria zina uonevu kama ile ya kupara samaki, unamtoza ushuru, kwa kweli ni uonevu kwa wananchi. Kwa hiyo, lengo letu sisi ni kuondoa kero hizo ili wananchi wasiwe na uonevu au usumbufu wa aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapochambua na kuangalia utekelezaji, tunazingatia kama Sheria zinakidhi misingi yote ya utungaji wa sheria, hazikinzani na Katiba ya Nchi, hazikinzani na Sheria Mama iliyotoa mamlaka ya kutunga sheria hiyo ndogo na hazikinzani na sheria nyingine yoyote, zinakuwa katika muktadha wote wa Sheria zote za Nchi. Hazikinzani na Sheria Na.1, Sura Na.1 *(CAP.1)* Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kwa ujumla hazikinzani na maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sheria ni nyingi sana kama walivyosema wenzangu hapa Wajumbe wa Kamati, kazi ni kubwa lakini tunaifanya kwa umakini mkubwa na tunasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jukumu hilo kwa kweli ni la Bunge, kama nilivyosema hii Kamati inafanya kazi hiyo kwa niaba ya Bunge na tunachambua kwa umakini mkubwa na tunasonga mbele. Sasa, Bunge lina wajibu wa kutunga sheria nzuri ambazo

zinatekelezeka, zina uhalisia, majedwali yako vizuri na lazima liwe na wivu wa kazi yake. Sheria zikiwa nzuri sifa ni kwa wale waliotunga na Bunge pia, lakini zikiwa mbaya lawama ni kwa Bunge, wale wanasahaulika na lawama zinakuja kwa Wabunge kwamba, hili Bunge vipi linatunga sheria mbovu kama hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba wote waliopewa maelekezo mahsusi, kwa mfano tumesema hapa kuna baadhi wameambiwa hapa tarehe 27 mwezi huu Septemba saa 9.30 mchana walete kwa Katibu wa Bunge, kuitikia maelekezo ya Kamati na maelekezo ya Bunge. Wengine wamepewa maelekezo mahsusi tarehe 20 mwezi Desemba saa 9.30 mchana wawe wameleta majibu hayo kwa Katibu wa Bunge ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusiana na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano pamoja na taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Wote mmeafiki, nawapongeza sana Kamati kwa kazi nzuri mliyoifanya. *(Makofi)*

*(Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru *AG* kwa majibu mazuri na *Chief Whip* dosari zilizoainishwa na Kamati mkazifanyie kazi na kama mlivyoambiwa inatakiwa *by December* mwaka huu ziwe zimeshawasilishwa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6.44 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 5 Septemba, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*